**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3. Thuwaibah Edington Kissasi | Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake. |
| 4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 7.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 8.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni. |
| 9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |

| | |
|---|---|
| 19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 15.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 16.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 17.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 18.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |

| | |
|---|---|
| 21.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 22.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |
| 23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 24. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 26.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 28.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 29.Mhe. Zahra Ali Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 31.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando. |
| 32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |

| | |
|---|---|
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Omar Ali Shehe | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43. Mhe. Abass Juma Muhunzi | Jimbo la Chambani. |
| 44.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |

| | |
|---|---|
| 45.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 46.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |
| 47.Mhe. Ali Moh'd Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 48.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 49.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 50.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 53. Mhe. Asha Moh'd Hilal | Jimbo la Magogoni. |
| 54.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 59.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 61.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 63. Mhe. Juma Duni Haji | Uteuzi wa Rais |
| 64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |
| 67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Uteuzi wa Rais |
| 70.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 71.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 73.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 74.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 75.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 76.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 77.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |

| | |
|---|---|
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.** |

**Kikao cha Kumi – Tarehe 23 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Thuwaybah Edington Kissasi) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka 2010/2011.

Naomba kuwasilisha *(Makofi)*.

**Mhe. Haji Mkema Haji (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka 2010/2011.

Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Zakiya Omar Juma (Kny: Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora):** Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya msemaji wa Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni ya Hotuba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka 2010/2011.

Naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 97**

**Utaratibu wa Uhamisho kwa Wafanyakazi**

**Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu –** Aliuliza:-

Kwa kuwa kuna wasi wasi kuhusu uhamisho wa wafanyakazi wa sehemu ya Hesabu (*Account Section*) katika Shirika la Umeme, *Internal Auditors* na

wafanyakazi wengine, wametolewa kwa upendeleo na kuwa taratibu na Kanuni za Utumishi Serikalini (*G.O*) haukufuatwa na kwamba uhamisho huo umetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika.

(a) Je, Mhe. Waziri ni nani anayehusika au mwenye mamlaka ya kutoa uhamisho kwa watumishi wenye kada inayohusika?

(b) Kama uhamisho wa wafanyakazi hao umefanywa kwa maelekezo ya Bodi ya Shirika la Umeme au kwa idhini ya Idara ya Utumishi Serikalini, kwa nini Wahasibu wote waliohamishiwa Shirika la Umeme watoke Mamlaka ya Bodi ya Mapato na sio taasisi nyengine?

(c) Hata kama taratibu zote za uhamisho wa Wahasibu na Wakaguzi wa hesabu (*Auditors*) hao waliohamishwa zimefuatwa. Huoni kwa mtazamo huu bado kuna dhana ya kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme, anatumia mamlaka yake kwa nafasi yake ya Uenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme na madaraka yake ya kuwa Kamishna wa Bodi ya Mapato kuwaweka watu anaowataka yeye mwenyewe kwa ubinafsi na kwa kumlinda yeye?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Shirika la Umeme la Zanzibar limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2006, ambapo kwa mujibu wa kifungu Nam. 10 kimeeleza majukumu yatayopaswa kutekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo.

a) Kwa mujibu wa utaratibu, Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kupitia Sheria ya Fedha Nam. 12 ya mwaka 2005, ndio yenye mamlaka ya kutoa uhamisho kwa wafanyakazi wa Kada ya Uhasibu;

b) Naomba kumthibitishia Mhe. Mwakilishi kwamba kwa muda huu hakuna mfanyakazi wa Kada ya Uhasibu aliyepewa uhamisho wa kazi kutoka Bodi ya Mapato ya Zanzibar na kuendelea na kazi katika Shirika la Umeme la Zanzibar.

Kilichofanyika ni kwamba, kwa sababu ya kuimarisha shirika hili, basi yupo mfanyakazi mmoja tu ambaye ameazimwa kwa muda,

ambao ni utaratibu wa kawaida katika serikali pamoja na mashirika yake.

Mkaguzi huyo anayepelekwa anayo Shahada ya *Masters* katika fani hiyo tofauti na yule aliyekuwepo; na

c) Kwa mujibu wa utekelezaji wa majukumu ya shirika hilo katika kusimamia na kuimarisha utendaji wa kazi kwa kusimamia mapato. Shirika limelazimika kuazima mfanyakazi mmoja kwenye Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu kama nilivyosema hapo awali.

Mkaguzi huyo hivi sasa ameazimwa kwa muda wa kipindi cha miezi mitatu na anategemewa kukamilisha na kuwasilisha ripoti yake kwa uongozi wa Shirika hilo, baada ya hiyo miezi mitatu. Kwa hivyo, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kimsingi mtumishi aliyeazimwa anategemewa kuondoka baada ya kuwasilisha ripoti yake.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Wafanyakazi hao ambao wametajwa katika suala hili ni watu wenye nafasi zao kwenye sehemu zao za kazi. Kutokana na uaminifu wao huwa unatosha kuratibu hesabu zao pamoja na mambo mengine kuhusu mapato katika sehemu hizo.

Je, kwa kuwa pametokea mfanyakazi mmoja kuazimwa, hao waliokuwepo hawana uwezo zaidi kuliko yeye pamoja na kwamba anayo shahada ya *Masters* labda hao wengine hawana?

Kwa hivyo, wizara ina mpango gani wa kutafuta hawa wenye viwango vya juu na kupewa dhamana na wengine wawe chini yao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumegundua kuna matatizo kidogo kama alivyosema Mhe. Mjumbe na ndio maana tukasema kwanza tupate mtu wa kuazimwa aende kwa muda kidogo, kwa ajili ya kutathmini pamoja na kufanyakazi na wale waliopo kuona hali iko vipi.

Baadaye ataandika ripoti na kuleta mapendekezo yake, kwamba nilipokwenda kufanyakazi nimekuta mapungufu moja, mbili, tatu. Kwa hivyo, ushauri wangu

ni huu na ushauri mzuri naamini utakuwa, yaani kama alivyoshauri Mhe. Mjumbe kwamba wale waliopo tuwaongezee nguvu. Kwa maana hiyo, tutashirikiana na shirika kwa ajili ya kuwasomesha wale waliopo, ili na wao wawe katika viwango vizuri kwa lengo la kuleta ufanisi katika shirika na hiyo ndio azma yetu.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa sababu Mhe. Waziri amekiri kuwepo huyo mfanyakazi japokuwa ni mmoja kutoka huko Bodi ya Mapato na kwenda *ZECO*.

(a) Je, atakubaliana na sisi kwamba hiyo ndio ishara ya upendeleo?

(b) Kwa nini asitoke sehemu nyengine yoyote mpaka atoke huko?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, unapotaka msaada wa kwenda kusaidia kazi maalum, basi lazima utafute mtu ambaye umeshawahi kufanyakazi naye, unamuamini tena unamjua, hii nasema ni kama *consultant*, yaani ni kazi ya muda tu. Kwa hivyo, huyu ambaye amepelekwa kule baada ya kutizamwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Umeme, kwa sababu ni miezi mitatu tu na anaweza kutoka sehemu yoyote na wala sio lazima atoke sehemu maalum.

Lakini Mwenyekiti wa Bodi ameona anaye mtu wa karibu zaidi na tayari ameshajua mpango wa kazi ulivyo kwenye Bodi yake, basi huyu anaweza kumuazima kwa muda na kule kusiharibike.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kamati ya *PAC* ilipotembelea Shirika la Umeme iligundua udhaifu wa udhibiti wa ndani wa fedha. Mapendekezo ya Kamati Mhe. Mwenyekiti ni kuitaka wizara pamoja na shirika kurekebisha hali hiyo.

Je, kumuweka mtu kwa muda wa miezi mitatu ndio kweli kutarekebisha hali hiyo. Kwa nini asitafutwe mtu wa kudumu katika nafasi hii ya *Internal Auditor* dhana ambayo ni muhimu sana katika kuangalia kwamba kuna *Internal Controlling System* ya Fedha?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na yeye kwamba ni kweli vizuri baada ya kuona matatizo pakawekwa *permanent staff* kwa nafasi ile, kwa ajili ya kurekebisha hali hiyo.

Lakini kama tulivyosema na tumeshauri kabla ya kumleta huyo *permanent staff* hizo *changes* ziwe vipi. Kabla ya kuzifanya hizo *changes* kuazimwe mtu kwa muda, kama *consultant* aende pale kwa muda miezi mitatu kwa ajili ya kufanya kazi na kuona hali halisi (*Situation Analysis*) na wewe mtaalamu Mhe. Said Ali Mbarouk, baadaye ataandika ripoti.

Hiyo ripoti ndiyo itakayotupa hayo mambo tufanye nini. Kwa hivyo, nakubaliana na wewe kweli ni vyema tukapata mtu wa kudumu, lakini kwa muda wa miezi mitatu tumuache atuandikie ripoti.

**Nam. 63**

**Uvutaji Sigara Sehemu za Mikusanyiko**

**Mhe. Hija Hassan Hija –** Aliuliza:-

Mara kwa mara Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) hutoa taarifa na tahadhari za kiafya juu ya madhara yanayopatikana kutokana na uvutaji wa sigara, uvutaji huo husababisha maradhi mbali mbali na hatimaye vifo.

(a) Ni maradhi gani yanayosababishwa na uvutaji wa sigara?

(b) Ili kupunguza kasi ya vifo na madhara ya sigara, nchi nyingi duniani zimechukua hatua za kisheria, ikiwemo kupiga marufuku uvutaji sigara katika mikusanyiko ya watu (*Public Places*). Je ni lini SMZ itachukua hatua ya kupiga marufuku uvutaji wa sigara katika mikusanyiko?

(c) Ni lini wizara yako itashirikiana na Idara ya Anga, ili kuweka vyumba maalum (*smoking-room*) katika viwanja vya ndege (Unguja na Pemba), ili kuwafanya wasafiri wavutao sigara kuwa mbali na abiria wengine?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) hutoa taarifa na muongozo na kutoa tahadhari ya jinsi ya kujiepusha na uvutaji wa sigara hasa kwenye maeneo ya mkusanyiko wa watu (*Public Places*).

Maradhi yanayosababishwa na uvutaji wa sigara ni haya yafuatayo:-

Kikohozi cha muda mrefu (*Chronic Bronchitis*);

- Maradhi ya Moyo;
- Saratani na Kiharusi;
- Kupungua nguvu za kiume;
- Kupata matatizo ya kupumua, mtu hupumua kwa shida; na
- Matatizo ya viungo vya mwili.

Mhe. Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kupiga vita matumizi ya sigara ni hizi zifuatazo:-

- Wizara ya Afya na Ustawai wa Jamii tayari imekamilisha Mswada wa Sheria za Afya na Mazingira, ambapo suala la uvutaji sigara kwenye mkusanyiko wa watu limezingatiwa;
- Kuelimisha jamii kupitia kwenye Vyombo vya Habari;
- Kutumia Siku Maalum, ya Kupiga Vita Matumizi ya Tumbaku Duniani tarehe 31 Mei, kwa kuelimisha Umma; na
- Kutumia fursa kuzitaka Taasisi za Serikali na vyombo binafsi kuweka vibao au alama maalum kwenye majengo au maeneo ya kuonesha sehemu ilioruhusiwa na isiyoruhusiwa kuvuta sigara.

Aidha wizara itatumia muda huu wa ujenzi wa Uwanja mpya wa Ndege, kuwashawishi wahusika kuweka sehemu maalum za kuruhusu uvutaji wa sigara. Pia wizara husika ya Uwanja wa Ndege wanatakiwa kutenga sehemu maalum ya wavutaji sigara kama unavyofanyika katika sehemu nyengine duniani kwenye viwanja vya Kimataifa vya Ndege (*International Airports*).

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na pia namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka kuuliza swali langu lenye vifungu (a) na (b).

(a) Katika majibu ya maswali mama amesema madhara yanayosababishwa na uvutaji wa sigara ni pamoja na upungufu wa nguvu za kiume. Je, kwa upande wa wanawake hawana athari yoyote?

(b) Watafiti wa Afya Duniani wanasema kwamba vijana wengi wanaovuta sigara ni katika umri wa miaka 15 na kuendelea, huwa ni chanzo cha uvutaji wa bangi na hatimaye kuelekea kwenye unga. Je, kuhusiana na hili wizara yako imelifanyia utafiti?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, kwa utafiti uliofanywa mpaka hivi sasa suala linaonekana kwa upande wa wanaume tu ndio wanapungua nguvu za kiume. Kwa upande wa wanawake bado halijabainika suala hili *(Makofi).*

Uvutaji wa sigara unapelekea uvutaji wa bangi na hatimaye kwenye matumizi ya unga. Kuhusiana na suala hili bado hatujafanya utafiti kwa. Lakini nadhani hivi sasa kuna haja ya kulifanyia utafiti suala hili, kwa ajili ya kujulikana kweli hali hii ya uvutaji wa sigara, unapelekea uvutaji wa bangi na hatimaye kwenye unga, basi tutafanya utafiti huo.

**Mhe. Asha Moh'd Hilali:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mtu anapovuta sigara kwenye mwili wake huingia *nicotine*, ambayo ni sumu. Je, kuna dawa yoyote ya kuondoa hiyo *nicotine*?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kwenye sigara kuna kitu kinachoitwa *nicotine* na miongoni mwa sababu zinazosababisha maradhi ambayo nimeyaeleza, basi moja ni hii *nicotine*. Kwa hivyo, kwa kuondolewa moja kwa moja *nicotine* ndani ya mwili uwezekano huo haupo. Lakini kinachofanyikana ni kutibiwa kwa mgonjwa mwenye maradhi yanayomsumbua.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa alikiri kwamba sigara zinaleta madhara na husababisha maradhi.

(a) Je, serikali kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imechukua hatua gari kuishauri serikali kuzuia uletaji wa sigara nchini?

(b) Kama haiwezekani Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imechukua hatua gani kuishauri Wizara ya Fedha na Uchumi kuongeza ushuru mara kumi ya ule uliopo kwa uingizaji wa sigara?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, sisi hatujashauri serikali kuwa wasilete kabisa. Lakini nakubaliana na yeye kama suala la kuongeza ushuru wa kuingizaji sigara, kwa ajili ya kupunguza kasi za uvutaji wa sigara.

Nadhani ni vyema tukaangalia pande mbili, hivi tutakaposema sigara zisiletwe, kweli watu hawatavuta. Nafikiri watazitafuta kwa njia nyengine zozote hata kama hapa nchini kwetu hazitaletwa, kama kimagendo kwa utaratibu wanaoujua wao na kama bado watu wanahamu ya kuvuta basi wataendelea kuvuta.
Kwa kweli suala hili limeshaelezwa sana kwenye vyombo vyetu vya habari na sisi Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tunatoa elimu hiyo pamoja na *WHO*

wanalieleza hilo. Kwa hivyo, hata kwenye matangazo ya kuvuta sigara, wanakwambia tumia sigara, lakini uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya yako.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba sigara tunazipiga vita, nadhani ni vyema tuende taratibu na watu watafahamu. Kwa kweli tatizo kubwa ni maradhi, kwa hivyo wataamua kuacha kutokana na matokeo ya maradhi wanayoyapata.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwenye majibu mama Mhe. Naibu Waziri alisema wanafanya suala la sheria kwa ajili hii na bado nakuwa mgumu kuona kwamba suala la uingizaji wa sigara upigwe marufuku.

Je, Baraza lako tukufu analieleza lini sheria hiyo itakuja hapa, ili wale ambao wanaathirika bila ya kutaka, kwa sababu wasiovuta wanaathirika zaidi kuliko wanaovuta wakati utoaji wa moshi. Kwa hivyo, lini sheria hii italetwa ili watu wapate kupona?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kulikuwa na sheria ikiitwa *Public Health Decree Cap* 73. Sheria hii ilikuwa ikitumika kabla ya Mapinduzi na mwaka 2006 sheria hii tumeifuta na tumekuja na Sheria mpya inayoitwa Chakula, Dawa na Vipodozi. Kwa hivyo, kuna mambo ambayo tumeyaacha kutoka kwenye *Public Health Decree Cap* 73, mambo mengi.

Kwa maana hiyo, tunakuja na sheria mpya ambayo itakuwa ikihusiana na masuala ya Mazingara na Afya ya Jamii (*Environmental and Public Health Act*). Hivi sasa mswada wake tayari tumeshautayarisha, ambayo unahusisha masuala ya sigara kanuni pamoja na miongozo yake, inahusisha masuala ya *quarantine* na maradhi ya miripuko.

Vile vile inahusisha mambo ya mazishi na makaburi, mambo ya ngoma na hata kusema ngoma wakati gani isipigwe pamoja na mambo mengine mengi. Kwa hivyo, tutaileta haraka iwezekanavyo mara baada ya Uchaguzi Mkuu 2010. Kwa maana hiyo, atayejaaliwa kuwepo katika Baraza tukufu letu hili wataijadili na kuipitisha sheria hii.

**Udokozi wa Mizigo Bandari ya Malindi**

**Mhe. Ali Denge Makame –** Aliuliza:-

Mhe Waziri, kwa kuwa katika miaka ya karibuni limekuwepo tatizo la udokozi wa mizigo katika Bandari ya Malindi Zanzibar. Je, wizara yako imechukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo.

**Mhe. Naibu Waziri Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 57 kama ifuatavyo:-

Naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa hivi sasa tatizo la udokozi wa mizigo Bandarini limepunguwa sana, kutokana na kuwa mizigo mingi inaletwa ndani ya makasha (Makontena), ambapo si rahisi kwa mtu kufanya udokozi, kadhalika usimamizi na ulinzi katika maeneo ya bandari umeengezwa maradufu.

Aidha wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inaendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo, ili kumaliza tatizo hilo.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kwa kiwango kikubwa imedhibitiwa hali ya udokozi wa mizigo na hasa kwa sababu inakuja kwenye makontena *(Makofi)*.

Lakini kuna masikitiko au malalamiko mengi kwamba wale watu wenye bidhaa za magari wanaibiwa sana *power window*, vioo *step ring* na *battery*. Je, wakati yanapotokea haya kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana ya bandari mteja akalalamike wapi na baada ya kulalamika kwa muda gani anafanikiwa kurejeshewa gharama ambazo zimepotea bandarini *(Makofi)*.

**Mhe. Naibu Waziri Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na malalamiko ya wizi mdogo mdogo hasa katika masuala ya magari. Kwa kuthibitisha hilo hata mimi mwenyewe binafsi wakati nilipoagiza gari yangu, basi ile ngao yake haikuwemo. Lakini matatizo haya kwa wakati ule yalikuwa yakitokea kutokana na zile meli ambazo zilikuwa

zikipita pengine Nairobi, Dar-es-Salaam na baadaye ndio kufika hapa. Kwa hivyo, hilo pia lilikuwa ni tatizo lakini nafikiri kwa hivi sasa hilo tatizo limepungua na kadri ambavyo siku zinazidi kuendelea tutajitahidi kuona kwamba hali hiyo inaondoka kabisa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri hujajibu swali wakalalamike wapi wanaopata matatizo haya.?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti malalamiko kwa vyovyote yana njia mbili kwanza inategemea kwamba hicho chombo kiliibiwa kutoka wapi na kama kiliibiwa kutoka bandarini maana yake bandari moja kwa moja itakuwa imehusika.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazrui:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza Nairobi bandari hakuna lakini la pili juzi hivi katika bandari yetu makontena yaliporomoka kutoka juu mpaka chini na hasara iliyopatikana ni kubwa kwa wafanya biashara, mpaka sasa hivi Mkurugenzi wa Bandari anawazungurusha zungurusha na mali ameshazivunja.

Je, kuna utaratibu gani wa wafanya biashara kupata haki zao?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa na mshukuru Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kunikumbusha kwamba Nairobi hakuna bandari, nilipokuwa nazungumzia mambo ya bandari ya Nairobi nilikuwa nakusudia Mombasa.

Lakini suala la makontena kukanguka na pengine watu kutokulipwa vifaa vyao suala hili tumelichukua na tutalifanyia kazi kwa sababu ni moja katika masuala yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Waziri kusema linachukuliwa na kufanyiwa kazi lakini ningeshauri na kuomba sana hili suala alilozungumza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ningeomba sana wafanya biashara wetu wakate bima kwa bidhaa zao unajua ni kitu kizuri sana na hujui rizki wakati gani itatokea, lakini ni vyema kwa mizigo kama hiyo mingi ni kuikatia bima sasa inakuwa kampuni ya bima wanachukua dhamana mpaka unakabidhiwa mizigo yako, nafikiri ni ushauri mzuri tuwashauri wafanya biashara wetu.
**Mhe. Haji Mkema Haji:** Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Wizi katika bandari yetu hasa hii ya Unguja hapa Malindi ni kero kubwa kwa wafanya biashara na watu wengine vile vile, lakini Mhe. Naibu Waziri anatwambia wizi huo umepungua mimi nitaamini umepungua ikiwa pale tuna wafanyakazi wazuri.

Je wale wafanyakazi wote wimbi linaloingia na kutoka watafanyiwa upekuzi kabla ya kuajiriwa pale?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Kweli nakiri kwamba wizi ni kero , ni tatizo mwenye mali yake inachukuliwa na baada ya kuchukuliwa maana yake unamtia hasara, ushauri wake tutauchukua kwamba tuhakikishe watu wote tunaoanza kuwaajiri pale tunawafanyia uchunguzi kujua kwamba rikodi zao za nyuma hazionyeshi kwamba kuna matatizo kabla ya kuajiri.

**Nam. 6**

**Mpango wa Benki Kuu wa Ujenzi wa Nyumba Nafuu**

**Mhe. Hijja Hassan Hijja (Kny: Mhe. Abass Juma Muhunzi ) –** Aliuliza:-

Hivi karibuni Benki Kuu ya Tanzania *(Bank of Tanzania – BOT)* imetangaza kutekeleza mpango wa ujenzi wa nyumba nafuu za makaazi kwa wananchi.

(a) Kwa kuwa Benki Kuu ni Taasisi muhimu ya Muungano ambapo Zanzibar kama nchi ni mbia, Je, nchi hii ya Zanzibar imepangiwa kujengwa nyumba ngapi katika mpango huo?

(b) Je, katika hiyo kasma ya Zanzibar ya mradi wa nyumba hizo, Serikali imeshatenga maeneo ya ujenzi wa nyumba hizo. Maeneo hayo ni yepi?

(c) Kwa misingi ya kuwa Zanzibar ni wabia kama nchi, na kwa kuwa Baraza la Wawakilishi ndilo linalosimamia mipango na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Je, Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili Mradi huu wa BOT utatekelezwa kwa muda gani na utagharimu kiasi gani cha fedha?

**Mheshimiwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi –** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 63 (a),(b) na (c) .

Kabla ya kumjibu swali hilo Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo.

Ni kweli Benki Kuu chini ya Programu ya Mageuzi ya Kifedha ya Karne ya pili *(Second Generation Financial Sector Reform)* imeweka kwenye mtandao wake taarifa inayohusiana na mradi wa kuendeleza soko la mikopo ya kujengea nyumba *(Housing Finance Projec*t) ambao unategemewa kuanzishwa hivi karibuni. Taarifa hizi ni moja ya hatua muhimu ya kupata mkopo ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari ipo kwenye majadiliano na Benki ya Dunia kupata mkopo huo.

Mkopo huu utakuwa na thamani ya dola za kimarekani milioni 40, ambapo sehemu kubwa itatumika kuanzisha chombo kitakachotoa mikopo kwa taasisi za fedha ili ziweze kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Benki Kuu itaunda chombo kitakacho kopeshwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 30 ikiwa ni kianzio cha kukiwezesha kutoa mikopo kwa taasisi za fedha zitakazokuwa zinatoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi. Sehemu ya pili ni kwa ajili ya kuendeleza utoaji wa mikopo midogo midogo ya kujengea nyumba. Madhumuni yake ni kuendeleza upatikanaji wa mikopo nafuu ya kujengea nyumba hasa kwa wenye kipato cha chini kwa utaratibu huo huo.

Sehemu ya tatu itakuwa ni kusaidia upatikanaji wa nyumba za kununua. Sehemu hii ya mradi itasaidia waendelezaji wa makazi binafsi na Mashirika ya Nyumba nchini kutengewa kiasi fulani cha mkopo huu ambacho zitasaidia kutoa elimu kwa waendelezaji makazi, pamoja na kufanya utafiti wa ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa kutumia vifaa vya bei nafuu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya mafupi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

a) Kutokana na maelezo niliyoyatoa hapo juu ni dhahiri kuwa Benki Kuu haina mpango wa moja kwa moja kutekeleza ujenzi wa nyumba za bei nafuu kwa Zanzibar au kwa Tanzania Bara. Benki Kuu chini ya programu hii ya Mageuzi ya Fedha *(SGFSR)* itatumia mkopo wa Benki ya Dunia katika kuipatia taasisi maalum itakayoundwa ili hatimae Taasisi hio izipatie Benki za ndani mikopo ambayo itakopeshwa kwa watu na Makampuni yatakayokuwa tayari kujenga majumba ya bei za juu na bei nafuu;

b) Kutokana na utaratibu huu ambapo Serikali haihusiki moja kwa moja katika ujenzi wa nyumba hizi, Serikali haijatenga maeneo yoyote kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi kwa sababu nilizozieleza hapo awali; na

c) Mradi wa kuendeleza soko la mikopo ya ujenzi wa nyumba ni wa muda wa miaka mitano. Mkopo unaotafutwa kutoka Benki ya Dunia ni wa masharti nafuu *(IDA Credit)* wa thamani ya dola za kimarekani milioni 40, na utalipwa kwa muda wa miaka 30, hii ni baada ya miaka 10 ya kipindi cha mpito kabla ya urejeshwaji mkopo *(grace period).* Taasisi zitakazoanzishwa au kuhusika chini ya mradi huu zitakuwa endelevu.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa dhana yangu kwamba mpango huu wa Benki kuu kujenga nyumba au kukopesha pesa kwa kujenga nyumba nafuu ni moja kati ya mambo ya kupunguza umasikini na kupunguza umasikini sio kumpa mtu pesa mkononi tu lakini kunakuwa na utaratibu maalum. Lakini nilishtuka pale Waziri alipokuwa akijibu kwamba haina mpango wa moja kwa moja wa kujenga nyumba nafuu wakati tunaowalenga ni masikini.

a) Hivyo haoni kwamba kama hatofanya hivyo ule umasikini hatoweza kuupunguza?

b) Hivyo kama kuna mradi huu na serikali imeliona kwa muda mrefu tatizo hili haoni kwamba Mhe. Waziri angakuwa tayari kuona kwamba *feasibility study* inafanywa na kujua maeneo gani yanastahiki kujengewa nyumba hizo ili kuwasaidia wale wananchi ambao wamo katika magumu hasa Micheweni na Kijini Wilaya ya Kaskazini Unguja?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Nakubalianana Mhe. Ame Mati Wadi kwamba mojawapo ya malengo ya mradi huu ni kupunguza umasikini nchini, sasa utaratibu au mikakati hiyo ya kupunguza umasikini ziko pana sana kuna mikopo mikubwa mikubwa ya kujengea, ipo mikopo midogo midogo ya kuwawezesha wananchi na ipo mikopo mingine ya kwenda benki moja kwa moja. Sasa huu uliokusudiwa hapa Mhe. Ame Mati Wadi ni wa kuwawezesha mabenki kujenga nyumba na huu ni mkopo.

Mimi nakubaliana na yeye kwamba kweli tunalenga kupunguza umasikini lakini unapokwenda kukopa lazima ujidhatiti jinsi ya kulipa, kwa hivyo tathmini itafanyika ionekane vipi watawaweza kulipa?

Suala lake la *feasibility study* mimi nakubaliana nae kwamba mambo yakishawiva basi tutajitahidi huku tunatengeneza mambo kupitia mabenki na maeneo tutayatafuta tuanze kuyatenga kwa ujenzi kama alivyoshauri Kijini na Micheweni maeneo ya kujenga nyumba kama hizi yapo na naamini kwa kushirikiana na Wizara mama tutalifanikisha hilo.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa siku za nyuma kulikuwa na mikopo ya mabenki kwa wajasiria mali yaani SMS na kwa kweli wenzetu wa bara wajasiri mali wao walipata mikopo ya mafedha mengi ya mamilioni ya biashara huku Wazanzibari wao hawakufaidi chochote.

Je, kwa utaratibu huu ambao BOT inatoa mikopo kwa taasisi za fedha bila ya kuona kwamba ile 4.5 ya mikopo hii kutoka nje Wazanzibari nao wanafaidika. Je, Serikali katika hili inawaangalia vipi maslahi ya wananchi wa Zanzibar ambao na wao wanataka mikopo hii?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti suala la kuwasaidia wajasiria mali wadogo wadogo kwa mpango huu wa SMS bado upo ule tunao utaratibu kwa kupitia mpango wetu wa mpango wa *best*, Wizara ya Biashara Viwanda na Uwekezaji wanaukarabati na kuuratibu mpango huo na sisi pia Wizara ya Fedha na Uchumi tunashirikiana nao ni mpango wa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya ufadhili wa benki ya dunia.

Mhe. Mwenyekiti  nafikiri mikopo hii haihusiani na ile ya 4.5 aliyosema hii ni mingine kabisa ni ya ndani na zinawezeshwa benki zetu kutoa mikopo kwa kujengea makaazi bora, hii ni mbali na ile lakini suala la kuwasaidia wajasiria mali wetu wadogo wadogo lipo na tutalisimamia vizuri.

**Mhe. Asha Moh'd Hilali:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Ardhi sasa hivi ni mali na hatuna nyingi kama alivyosema ya kutosha, sijui nyumba hizi zitakuwa za ghorofa au za chini?

c) Mpango huu sijui mkataba wake utakuwaje?

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Nyumba zitakuwa za horofa au za chini mimi nafikiri hapo tusubiri mpaka huu utaratibu mzima utakapokuwa tayari, halafu inategemea mtu mkopo wenyewe anaotaka uko je anataka nyumba ndogo ya vyumba viwili, au vyumba vitatu au ya ghorofa. Lakini sasa mpango mzima huu utaratibuwa na Wizara yetu husika na makaazi na nyumba Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na ninaamini wao watazingatia uwezo wa ardhi yetu iliyopo na eneo liliopo haitokuwa kila mmoja atafanya atakavyo, lazima tutasimamia na kuratibu vilivyo na wataalam wetu wa mipango na miji tunao.

Kwa hivyo Mheshimiwa naomba kumtoa wasi wasi kwamba na wasi wasi wakati ukifika pamoja na huo mkataba aliosema itaandaliwa vizuri ili mambo yaende kama yalivyopangwa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Vikosi vya SMZ kwa mwaka wa fedha 2010/2011

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa na afya njema na salama.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nianza kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na watendaji wake wote, niwapongeze wakuu wa Wilaya ya Micheweni na Wete na kusini Pemba pia niwapongeze Wakurugenzi na maafisa mbali mbali wa Wizara ya Idara ya vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti mimi niende moja kwa moja kwenye mchangio wangu nianze Halmashauri ya Micheweni hapa nimpongeze katibu wake kwa kuweza kutekeleza majukumu yake na kutekeleza miradi mitano ya maendeleo, kwa sababu Halmashauri ya Micheweni ni changa sana na mapato yake ni kidogo lakini hapo hapo amejitahidi na Mwenyezi Mungu amzidishie. Nikibakia hapo hapo Halmashauri ya Micheweni hapa namuomba Mhe. Waziri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni japokuwa ni kichinjamimba lakini namuomba Mhe. Waziri zile nafasi ambazo kulikuwa na mfanyakazi mmoja ambae amekufa sijui kama ameshaingizwa mtu, lakini namuomba ile nafasi kwa heshima na

taadhima amuingize mtu ili Katibu wa Halmashauri afanye kazi zake vizuri na ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti nibakie kwanye Wilaya ya Micheweni Mhe. Waziri kule kuna jengo la Wilaya ya Micheweni limezungurushiwa ukuta ile afisi yake, lakini sijui kama waliingiziwa pesa za kutosha za kumaliza ukuta ule? Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe vizuri nifahamu ili nijue na mimi nikiwa ni muwakilishi wa Mkoa ule wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Mwenyekiti niende kwenye mji Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ambao uko Wete na kuna miji midogo Konde na Micheweni, namuomba Mhe. Waziri na sisi kwenye Mkoa wetu wa Kaskazini Pemba lisije likatokezea tatizo kama lile la juzi lililoulizwa swali ukasema kama utajenga eneo la *packing* ya magari mkabala na Mava, na mimi pia nakuomba utenge sehemu maalum kwa sababu mji sasa hivi ni mdogo na utakapokuwa utakuwa maeneo hayapo itabidi twende kwenye miji midogo ya Konde na Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti niende kwenye wilaya hiyo hiyo ya Micheweni huku kuna ukumbi wa mikutano nao ni ukumbi wa Serikali ukumbi ule ulijengwa zamani sana na ukajengwa kwenye mazingira ambayo watu wakati huo walikuwa ni kidogo, nakumomba Mhe. Waziri ukumbi ule na pesa zako sio kidogo ulizoingiziwa ujengwe ukumbi ambao una hadhi ya Kimicheweni, Micheweni ya leo sio Micheweni ya jana.
Mhe. Mwenyekiti kwa sababu muda wako ni mdogo ulionipa naomba nijali muda wako mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsate sana. *(Makofi)*

**Mhe. Juma Duni Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi na mimi nisichukue muda mkubwa na mimi nishirikiane na wenzangu kumpongeza Waziri na namtafuta naona simuoni.

Mhe. Mwenyekiti mimi nina masuala machache tu kwa sahibu wangu tumesoma wote tukicheza mpira mimi *write wing* yeye *center half*. Tatizo langu mimi ni moja tu na nasikirika Mheshimiwa kwamba nilikuwa nachukua takwimu hapa katika mjadala nikagundua asilimia sabini au sitini ya mjadala wa jana ukizungumza matatizo ya vitambulisho, wenzetu kule walikuwa wanatoa maoni na sisi huku tulikuwa tunatoa maoni, hii inathibitisha kwamba vitambulisho vina matatizo na ni kawaida mtu yoyote yule akifanya kosa ukimwambia kafanya kosa atajitetea ndio ubinaadam.

Lakini vile vile katika masuala kama haya ya kitaifa kuendelea tu kukana au kupinga au kutetea wakati kuna kila ushahidi kwamba kuna matatizo hasara inakuwa sio ya mtu inakuwa ni ya taifa, kwa sababu muda ni mfupi

nisingependa niende mbali sana lakini tumekuwa tukikutana kwenye makongamano, kwenye semina, kwenye mijadala mbali mbali tunaeleza suala la vitambulisho.

Nianze kwa kutizama ukurasa wa 13 kifungu cha 27 pale Mhe. Waziri ameeleza kwamba kwa mujibu wa makisio ya takwimu za Zanzibar waliopaswa kupata vitambulisho ni 575,225 na maelezo haya yanasema yamezingatia wingi wa watu wa Zanzibar 2010 kwamba ni 1,273,834, na sisi vile vile tuna maarifa kidogo ya takwimu. Kuna tofauti kidogo hapa ya takwimu hizi za jumla ya watu na wanaostahiki kuandikishwa 2010. Ili uwajue watu wa 2010 inabidi ufanye makadirio ya kutumia sensa ya 2002 sasa sisi tulichofanya ni kwamba watu wa Zanzibar mwaka 2010 unapata kwa njia mbili, kwa kutumia ukuaji wa kitaifa ambao kwa Zanzibar ni 3.1 au unawapata kwa kutumia ukuwaji wa Mikoa yaani unachukua Mikoa mbali mbali, kila Mkoa una ukuwaji wake.

Mhe. Mwenyekiti nisipoteze muda zaidi kwa sababu ni manamba haya nawengi hawayapendi kwa kitaifa ni 3.1 lakini kwa Wilaya au Mikoa. Mkoa wa Kaskazini  Unguja ni 2.5 Mkoa wa kusini ni 2.1 Mjini Magharibi ndio unakuwa watu zaidi ni 4.5 Wete 2.2  Micheweni 2.2 ni sawa sawa na ile mikoa ambayo ni 2.3. Sasa kwa kutumia fumula za kitaalam za kukua kwa watu sisi tumepata kwa kutumia uwiano wa kitaifa unapata 1,257,014 na kwa Kutumia Mikoa unapata 1, 267,190 tofauti hiyo sio kubwa sana kati ya kuzingatia wingi wa watu. Lakini unapozingatia wale wapiga kura unapochukua wale aliowapa vitambulisho laki 560 kwa maelezo yake hapa na ukagawa kwa wingi wa watu kachukua 45% lakini *general formuler* ya kukisia wingi wa watu wanao umri wa miaka kumi na nane na kuendelea ni asilimia 48 au 49.

Kwa hivyo matokeo yake ni kwamba sisi tumepata wapiga kura kwa kuzingatia asilimia 48% ya watu wazima na maisha nchi yoyote ile watoto wadogo wenye miaka ziro mpaka kumi na nane ni wengi kuliko watu wazima, sasa kama na yeye angetumia asilimia arubaini na nane angepata wapiga kura laki 611,440 angetumia arubaini na nane. Mimi nina makisio yangu ambayo yake yeye ni madogo.

Lakini suala ni kwamba vitambulisho hivi vilishatolewa na yeye kasema ameshafika tisini na nane kwa mia lakini wanavyo nani Mhe. Nassor Ahmed Mazrui nadhani alifanya uchambuzi wa kutosha tu kueleza kwamba kuna watu wengine ambao wana uraia mbili na bado wana vitambulisho, sasa nilichofanya niliweka tu hawa watu walioandikishwa kwa mujibu wa dafrari la ZEC, hawa watu waliopewa vitambulisho, hawa watu waliostahiki kuwa watu wazima mwaka huu sasa ukiziweka data hizo kuna mgongano mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti naomba nitoe mfano Jimbo la Dimani watu waliopewa vitambulisho ni 18,394 lakini watu wanaokisiwa wawepo kwenye jiombo la Dimani ni 13,286 wawe wapiga kura, kwa hivyo utagundua kwamba kuna vitambulisho visivyopungua elfu tano vimetolewa jimbo la Dimani zaidi kuliko ilivyostahiki. Nitoe mfano wa Kiembesamaki waliostahiki kuwa watu wazima ni 14,000 na wapiga kura kinachoshangaza walioandikwa pale ni watu 4,700 tu. Lakini waliopewa vitambulisho na shehe Mkurugenzi ni watu 7,178, mfano kama huu unaukuta Chambani na mwengine mwingi.

Kwa hivyo, ukizioanisha hizi takwimu unakuta kuna vurugu. Kuna kiasi watu 152,000 kwa mujibu wa takwimu zake wana vitambulisho hawakuandikwa. Swali linauliza, hawa ni nani wenye vitambulisho ambao hawakuandikishwa. Sababu tunazopewa na wataalamu hawa wa ZEC na afisi ya vitambulisho, kwamba kujiandikisha ni jambo la hiari. Lakini jamani siasa za Zanzibar kujiandikisha jambo la hiari na tunaona ilivyokuwa wakati kutafuta vitambulisho, sio vizuri kurudia.

Aidha, vitambulisho hivi viko mahali haviko au wamepewa Wazanzibari wasiostahiki kuwa Wazanzibar, ndio maana yake. Sasa tukanyamaza kimya tukasema tusubiri muda. Juzi wamemaliza kuandikisha NEC, Tume ya Taifa na Tume ya Taifa ilipoulizwa swali. Je, inakuaje mimi Mzanzibari wa miaka 70 sikupewa kitambulisho, kwa hivyo simo kwenye daftari la Zanzibar. Lakini pia ninyimwe kupiga kura ya Muungano, wakati mwenzangu wa Kigoma anapiga kura ya Muungano bila kuzuiliwa kwa kitambulisho.

Tume ya Taifa ikasema sisi wote wale ambao ni Watanzania basi tunastahiki kuwaandikisha. Sasa hapa nina karatasi *latest* na tulitaka kufanya hivi kusudi ili tusionekane tunabwabwaja. Ninawaomba wenzangu waliomo humu na wananchi wanaonisikiliza. Sisemi hivi kwa sababu mimi ni CUF, nasema hivi katika kulinda haki ya Mzanzibari. Anaweza kuwa ndugu yangu au ndugu yako. Walioandikishwa katika Jimbo la Nungwi na NEC ni 2,479, Jimbo la Nungwi tu. Hawa wengi wao ndio wale walionyimwa vitambulisho kwa vizingiti visivyokuwa na msingi.

Mhe. Mwenyekiti, kurugenzi hii tulipokuwa tukiiambia, na nakumbuka sitaki kumsema mwenzangu kwa sababu hana njia ya kujitetea. Niliwahi kukutana naye nikamwambia mheshimiwa, kama wewe umekwenda shule na sisi tulisharudi, tunayokueleza ni mambo ya kitaalamu. Jibu lake akasema mimi siwezi kubisha na wanasiasa. Sasa hii hapa 2,479 Jimbo la Nungwi wameandikishwa kwa NEC, tulikuwa tunakusanya na majimbo mengine. Sasa ukichukulia 2,000 tu kwa wastani mara 50 ni ngapi, ni 100,000. kwa hivyo, Wazanzibari 100,000 wamenyimwa vitambulisho bila sababu na hizo kwa kutumia *data* za mabosi.

Sasa Mhe. Waziri nisichukuwe muda isipokuwa tatizo tulilonalo ni kwamba Wazanzibari wengi wamefanya kila juhudi wapate vitambulisho, ili washiriki uchaguzi basi wamevikosa kwa sababu ya masharti yaliyokuwa hayana msingi. Kwa hivyo, hili ni tatizo ambalo tusilitizame katika msimamo wa kuvutana kuwa labda mimi nitapata mwengine akose. Tulitizame kwamba hawa walikuwa na haki nyengine zaidi kuliko zile za kupiga kura.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nakuomba umalizie mheshimiwa.

**Mhe. Juma Duni Haji:** *Inshaallah*. Naomba nimalizie kwa jambo moja Mhe. Mwenyekiti, naomba unistahamilie.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu walipewa vitambulisho mwaka 2004 kulikuwa hakuna masharti magumu, wakapiga kura mwaka 2005. Hakuna sheria ya uchaguzi inayosema mtu aliyeko kwenye daftari la kupiga kura atolewe, isipokuwa labda aonekane mwendawazimu. Tuliwasiliana na wanaohusika kwamba hawa munawatafsiri vipi. Wakasema ni kweli ni haki yao, kwa sababu kubadilisha kitambulisho sikutaka mimi nimeambiwa na tume. Wakaitwa waende mawilayani mwao wakaandikishwa kwa haraka haraka, lakini hawapungui 3,000. Wakaambiwa watatayarishiwa utaratibu ili wapate vitambulisho ili waandikishwe kwenye daftari, wakatangaziwa kwenye redio. Walipokwenda hawakuandikishwa wala hawakupewa kitambulisho na leo wamebaki wanauliza sasa sisi jamani tuna haki gani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kumwambia Mhe. Waziri kwamba suala la vitambulisho lina matatizo na linahitaji kutizamwa katika misingi ya kulinda haki za Wazanzibari, badala ya kulitizama kisiasa. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mkongwe Nassor Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na mtume aliyetuwezesha kufika hapa katika hali ya uzima na salama.

Pia nakushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu mdogo. Vile vile naipongeza hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu kwanza naanza kwa kuzipongeza Halmashauri za Wilaya zote za Pemba na Unguja, kwa jinsi kazi zao ngumu wanazofanya. Pia nazipongeza Halmashauri za Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja kwa jinsi kazi ngumu wanazofanya, za kusaidia miradi ya jamii na kuchangia mapato mbali mbali.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga jengo la Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ni ni jengo la kileo. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mkokotoni haliridhishi, kwa hivyo tunaishukuru serikali kwa kutujengea jengo lile.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea navipongeza na Vikosi vya SMZ vyote kwa kazi ngumu sana wanazofanya za kila siku. Nakipongeza na Kikosi cha KMKM kwa kazi ngumu wanazozifanya na kujenga jengo la afya pale Kibweni. Mhe. Mwenyekiti, jengo lile haliwafai wao tu maaskari, bali linatufaa sote jamii wa mashamba na wa mjini. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hawakuweka kizuizi pale, mgonjwa yeyote anaweza kwenda kupata huduma. Kwa hivyo, kwa suala hili mimi nawapongeza moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, nalipongeza Baraza la Manispaa. Baraza hili kidogo wamejitahidi, mtu mwenye haki yake hupewa. Ilikuwa Mhe. Mwenyekiti, ukipita sehemu ile ya Darajani panapoegeshwa zile gari za teksi, pale ukipita ni lazima uzibe pua kwa ile harufu inayotokea pale. Lakini kwa kipindi hiki namshukuru Mwenyezi Mungu harufu ile kidogo imeondoka.

Mhe. Mwenyekiti, pia nawapongeza Baraza la Manispaa kwa kuondoa ule mtiririko wa ng'ombe na punda. Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa ukifika sehemu ya Maruhubi ng'ombe wametandawaa na punda na hawa ng'ombe Mhe. Mwenyekiti, walikuwa wameshatuletea ajali. Mimi ninaye kijana wangu alipofika pale usiku alikutana na ng'ombe, kwa bahati akaanguka na vespa, basi aliathirika jino la mbele. Kwa kipindi hiki tunashukuru wale ng'ombe kidogo wamewazuia.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua waliyochukua ya kuwasomesha masheha na madiwani kwa kuwapa semina na mafunzo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kama unavyonielewa leo kidogo hali yangu sio nzuri, basi siwezi kupoteza muda wako. Kwa hayo machache mimi naunga mkono hotuba hii mia juu ya mia. Ahsante sana.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kwa asubuhi ya leo kutoa machache kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Kwanza namshukuru *Allah* kwa kutuweka hai na wazima na tukapata fursa ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu. Pili, namshukuru Mhe. Waziri kwa kujitayarisha na kutoa kitabu kizuri na kikubwa, pamoja na hotuba yake nzuri

ambayo kwa uwezo wa *Allah* amempa afya akaweza kuimaliza hotuba yake na leo tunayo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka nianze na vikosi. Kuna vikosi viwili, kimoja kinaitwa Valantia na kimoja kinaitwa Zimamoto. Kidogo mimi nilikuwa na wasi wasi labda kulitokea mabadiliko, labda katika uchapishaji wa kitabu au sikufahamu vizuri. Kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa katika kitabu, basi hiki Kikosi cha Zimamoto kina malengo mengi na makubwa zaidi ya utendaji wa kazi. Pia kina kazi kubwa ambayo kama maelezo au maneno mawili yake yanavyosema, yaani kuzima moto na bahati nzuri au mbaya inaripotiwa kwamba moto hutokea katika kila fani, hata katika kitabu hiki imeelezwa na pia hutokea matokeo ya kuokoa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa mujibu wa bajeti iliyowekwa katika kitabu hiki, Kikosi cha Valantia kimepewe bajeti kubwa zaidi kuliko hiki cha Zimamoto na Uokozi. Sasa sijui ni makoseo au vipi. Lakini la kushangaza zaidi ni kwamba kulikuwa na zana nyingi zinahitajika kama ambavyo nitaeleza katika muda mchache ujao, lakini Kikosi cha Zimamoto kimepewa bajeti ya matumizi ya kawaida tu ya bilioni 1.789. Wakati kile cha Valantia kimepewa bajeti mbili, moja ya matumizi ya kawaida 2.182 bilioni na milioni 100 kwa kazi za maendeleo. Sasa namuomba Mhe. Waziri aje anitatulie hiki kitendawili hapa, maana yake kwangu mimi ni kitendawili sikufahamu vizuri je, ni sawa sawa ilivyoandikwa au ni vyenginevyo.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama tunaweka kikosi, basi mimi nafikiria kingekuwa na nguvu zaidi, ikiwa kikosi kile kitapata mafunzo ya kuzima moto kweli ndani na nje ya nchi na baada ya kupata mafunzo ya kuzima moto, kitaweza vile vile baadhi yao kupewa mafunzo ya kufanya uokozi.

Mhe. Mwenyekiti, leo tuko karibu mwezi mmoja au miwili kabla ya skukuu tunayoita baada ya Ramadhani. Skukuu ya baada ya Ramadhani yaani Iddi iliyopita, katika jimbo langu kuna kijiziwa kidogo hivi au dimbwi lenye kuweka maji, basi Mhe. Mwenyekiti, alizama mtoto pale wa miaka kama 12 hivi. Alikwenda kuoga yeye na mwenzake, lakini yeye akateleza na kuingia kwenye maji mengi hakuonekana tena. Kwa hivyo, kwa bahati nzuri wale aliokwenda nao wakenda kupeleka habari, basi kikaja hiki Kikosi cha Zimamoto, lakini bahati mbaya ni kwamba hakina watu wenye ujuzi wa kuokoa yaani wa kuzamia. Kwa hivyo, ikashindikana kwa kupitia wao kupatikana yule mtoto aliyezama pale. Kuna vijana kama watatu hivi waliagizwa kutoka Kiuyu Maziwa ya Ng'ombe, ambao ni wazamiaji baharini. Walipokuja walichukua kama dakika 10 tu au 15 hivi, basi walimpata yule mtoto, keshakufa lakini alipatikana. Kwa sababu ilikuwa ni kizazaa ni siku ya skukuu kama tuijuavyo na wazee wote wamekusanyika. Sasa ikaonekana

dhahiri pale kwamba Kikosi hiki cha Zimamoto kipo, lakini hakipewi utaalamu unaotakikana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kile ni kidibwi tu, lakini sisi tumezungukwa na bahari. Wakati mwengine kunatokezea matokeo ya baharini. Kwa hivyo, kikosi kile kingepaswa kwenda na kuweza kuokoa maisha ya watu. Kwa hivyo, tunaomba sana tusivitaje kwa majina tu kama ni Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, lakini kivitendo kiwe kinafanyakazi inayotakiwa. Sasa bajeti kama hizi zikipangwa namna hii huwa hazileti taswira nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na vikosi. Mimi nina neno moja tu la kumalizia, kwa sababu tunakwenda katika utawala bora na utawala wa demokrasia, kwa hivyo sio vizuri kutumia baadhi ya maneno katika vikosi vyetu au katika shughuli zetu ambazo tafsiri zake zinakuwa ni kubwa zaidi. Mengi nilifikiria vikosi vyote hivi vimekusudiwa ni walinzi, lakini sio wapiganaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi sipendi sana litumike neno wapiganaji, kwa sababu ikiwa hana wa kupiga atampiga raia sasa, kwa sababu keshaitwa mpiganaji. Kwa hivyo, mimi napenda sasa kwamba hivi vikosi vyetu hili neno wapiganaji tuliondoshe, kwa sababu katika lugha zote za kimataifa kuna neno kwa Kiingereza wanatumia neno *defence* yaani walinzi. Kwa hivyo, hakuna neno hili , hivyo tuwaondowe katika lugha hizi ambazo zinawafanya labda wajielewe vyengine kwamba wao ni wapiganaji. Kwa hivyo, wakipewa kazi ya kupiga au kama hawakupewa basi watapiga tu kwa sababu wao ni wapiganaji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakwenda kwenye sehemu ya pili ya manispaa zetu hizi. Mimi hasa nataka niende katika jiji la Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, mji huu kwa kweli uko katika hali ya kizaazaa kuhusu utaratibu mzima wa upangaji wa gari, *parking areas* na *stand.* Huwezi kujua hapa ndio gari zinawekwa kwa *car park* au hapa ndio *stand.*

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kutokana na hali ya mji ulivyo tusifanye maamuzi ya haraka, tukae kitako kwa kina kabisa tulifikirie. Kwa sababu mtu yeyote anapokwenda mjini. Mimi niliziorodhesha baadhi ya haja, ama anakwenda sokoni, au anakwenda hospitali, au anakwenda kutafuta huduma za safari, au anakwenda benki, au anakwenda kununua biashara nyengine kwa jumla. Sasa ukimuweka kilomita 100 kutoka pale anapokwenda ukamwambia hapa gari ndio imefika *stand*, basi utakuwa hujamfikisha katika huduma yake ambayo ameichukulia na wale wenye magari wanakata leseni kwa ajili ya kuchukua watu kuwapeleka katika haja zao.

Kwa hivyo, hili jambo sio rahisi kama linavyofikiriwa kuwa tujenge Mava Mbarouk, au tujenge Tibirinzi au tujenge Chanjaani. Tukae kitako kwa kina kabisa tuwashirikishe na wananchi, ili tuweze kutoa picha moja. Kwa sababu kuna gari za aina mbili, ziko za Mkoani na ziko za Wete pamoja na Konde na Micheweni. Tunaweza tukapata maamuzi ya vituo mbali mbali kwa hizi gari, lakini zimeshawafikisha watu katika maeneo yao ya haja zao.

Kwa hivyo, mimi nafikiri sio jambo rahisi kama linavyofikiriwa. Kwa sababu *stand* iliyokuwepo ni ndogo na haitoshi, lakini haikutayarishwa kwa sababu haina sehemu ya kuingilia na ya kutokea, kwa sababu gari zinaingilia hapo hapo na zinatokea hapo hapo, pia hilo ni tatizo. Ile ile ingefaa na ingesaidia, lakini ingekuwa gari zinapoingilia na zinapotokea ni sehemu tofauti.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri pamoja na yote uliyojibu juzi kwamba utakwenda kuliona eneo la Mava Mbarouk, lakini nakuomba sana suala hili uje na jibu la kuona kwamba ni muda gani mtakaokaa kitako pamoja na wetu anayehusika ili kuweza kupata ufumbuzi wa uhakika na wa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka kulizungumza katika bajeti hii …..

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa ufupi kabisa.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Kwa ufupi sana, sawa sawa. Nakushukuru kwa ruhusa yako hiyo. Ni kwamba jambo lolote katika dunia, kwa sababu sisi ni viumbe wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu alivyotuumba alituumba kwa kutujua, hakuna mtu ambaye hana makosa. Lakini kinachotakiwa katika kutekeleza jambo lolote ni nia njema. Wazungu wanaita *goodwill.*

Sasa suala lililozungumzwa kwa kirefu mimi sitaki nilirudie kama walivyozungumza wenzangu limeshatolewa ushahidi. Ni kwamba vitambulisho tunataka kuona Mhe. Waziri aje atuelezee hapa ni njema gani iliopo kwa Wazanzibari kuhusu hivi vitambulisho. Tusingevipigia kelele.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi niliwahi kuzungumza hapa nikasema kwamba huko nyuma ilikuwa ukitayarisha *passport,* basi ulikuwa unaruhusiwa kutia majina ya watoto wako mule katika ile *passport* yako na ziko nchi zinazofanya hivyo. Sasa leo baba ambaye kafunga ndoa yake ya kihalali Msikitini au kwenye baraza na mashahidi walipatikana na cheti cha ndoa kikapatikana. Lakini shahidi anayekubalika ni sheha na sio baba. Mimi nafikiria tungekuwa na nia njema, baba angetosha kutoa ushahidi wa mwanawe na hii ingetusaidia sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe malizia.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuzungumza machache kuhusiana na bajeti hii ambayo ina umuhimu wa pekee katika nchi yetu na kwa sababu muda ni mchache nitakuwa nagusia kila eneo kidogo kidogo, lakini la muhimu niseme lile ambalo nilikusudia kusema.

Kwanza kabisa mimi nimeshangazwa sana na jinsi ambavyo ajenda haijazingatiwa katika wizara hii, tukiangalia katika watendaji wetu wote nafikiri kuna wanawake watatu au wanne. Hilo ni moja la Mhe Waziri kulizingatia kwa siku tunazokwendea usoni huko.

Jengine pia ninashangazwa kuona kwamba wenyeviti wa mabaraza au Halmashauri za Mabaraza kuwa hawalipwi katika kikao hiki, ni muhimu tungekuwa nao. Labda kama wanawalipa hawaji tutakuja kuelezwa tutakapomaliziwa katika bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuongea juu ya Idara ya Sera na Mipango, katika lengo lao moja wapo ni kuendelea kusimamia utekelezaji wa mchakato wa mageuzi ya Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, hili suala limekuwa ni la muda mrefu, nimekuwa nalisikia toka nimeanza kuwa ndani ya hili Baraza na ninaendelea kusikia. Kwa bahati miaka mitano hii inamalizika suala hili halijakamilika. Kwa hivyo, niombe tu kuwa suala hili lina umuhimu wake na kama marekebisho na mchakato mzima huu wa mageuzi ya serikali za mitaa halijakamilishwa, kwa kweli ufanisi katika utendaji wa shughuli zake utakuwa haujapatikana. Kwa hivyo niombe kwamba msisitizo uwepo katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo napenda niliunganishe hapo hapo, ni suala zima la masheha. Tunaelewa kuwa masheha hawa ndio viongozi wa *central government* ambao wako katika ngazi ya chini kabisa huko ambako wako wananchi, yaani katika ngazi ya shehia, ukitoka shehia utakwenda jimbo, wilaya mkoa na kadhalika. Lakini bado hatujawa na utaratibu mahususi wa jinsi gani ya kuwapata hawa masheha. Lakini vile vile jinsi gani sheha anaweza kuondoshwa kwenye madaraka yake, anaweza kufukuzwa kwa kufanya kitu gani. Haya mambo  hayako wazi na kwa kweli bado yanatupa mtihani.

Katika kipindi cha nyuma tulizowea kusikia humo wawakilishi wakidai kuwa wananchi wanataka masheha wachaguliwe na wananchi wenyewe ili wawe ndio hasa wale wanaowatumikia na watu ambao watakuwa sahihi, lakini kwa sababu hawa ni sehemu ya serikali, yaani *central government*, inakuwa ni

ngumu. Tunao madiwani ambao wanachaguliwa na wananchi, basi ni vizuri serikali ikaona huo umuhimu wa kuwachagua masheha ambao watakuwa na mahusiano mazuri ndani ya jamii, kwanza. Vile vile watakuwa na uelewa wa zile shughuli ambazo watakuwa wanafanya.

Mhe. Mwenyekiti, tuna suala zima la vitambulisho na mambo ya uandikishaji upiga kura, mambo ya migogoro ya ardhi inayotokea. Mara nyingi humu ndani hatuwezi kuzungumza chochote bila ya kuwataja masheha. Masheha wanakuwa wanahusika. Kwa hivyo, tukubali kwamba bado tuna matatizo kwa masheha ambao tunao, sisemi wote lakini wengi wao. Kwa sababu kila tatizo linalojitokeza hapa wa kwanza kabisa anakuwa ni sheha.

Kwa hivyo, niiombe serikali ione umuhimu wa kujipanga vizuri, labda iwe kabisa na utaratibu, nani atakuwa sheha na vigezo vyake ni vipi. Ili awe ni mtu ambaye anakubalika kote, kwenye serikali lakini pia kwenye jamii ambayo ataitumikia. Sio vizuri kuwa na sheha ambaye hana *public relation* nzuri na jamii yake, kwa kweli ufanisi utakuwa mdogo, kwa sababu hawa ndio tunao watumia katika kupiga vita malaria ndio hao hao tunao watumia. Sasa kama utakuwa na mtu ambaye katika jamii hakubaliki, kwa kweli ufanisi katika masuala hayo yatakuwa ni magumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la vikosi. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, kwa bahati nzuri wizara hii ni moja katika kazi zetu, tumepitia na vikosi vyote, tumeviangalia mahesabu yao. Ukiwacha matatizo madogo madogo ambayo yamo ya kifedha, kwa ujumla hesabu zao hazina matatizo sana za mwaka uliopita. Kuna suala zima ambalo limelalamikiwa na mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu za serikali na hili linahusiana na uwazi juu ya kuonesha yale mahesabu wakati mkaguzi anakagua. Tumewahi kulalamikiwa na mkaguzi kwamba wenzetu hawa wa vikosi wanakuwa hawako wazi katika kutaja mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sifikiri kama mishahara ni kitu cha siri, wakati mkaguzi anataka kukagua basi ni vizuri tuwe wawazi tumuoneshe, kwa sababu hiyo haina siri yoyote. Mimi nakubali kabisa kwamba kuna mambo ndani ya vikosi ni ya siri, wenyewe wanaita *classified information*. Mambo ya silaha, mambo ya vifaa ambavyo vikosi vinanunua, hayo ni mambo ambayo kuna njia zake za kufanyia usahihi wake kama mahesabu yamekwenda sawa au sio.

Lakini suala rahisi, mkaguzi anapokwenda katika kikosi akasema nioneshe orodha ya mishahara ya wafanyakazi ndani ya kikosi chako, jambo hili halina tatizo kabisa kwa nini lisioneshwe. Ningewaomba wenzetu hawa wa vikosi washirikiane na afisi hii ya wakaguzi ili wawe wawazi kabisa ili hesabu ziwe wazi zisiwe na mashaka.

Jengine ambalo tumeshawahi kulizungumza humu ndani ya Baraza na Mhe. Waziri atakuwa anakumbuka na Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi pia atakuwa anakumbuka. Kulitokea upotevu wa mishahara kwa Kikosi cha Zimamoto, nafikiri sasa ni miaka mitatu na kuendelea. Lakini kukawa na tatizo kwamba wale walioibiwa mishahara yao mpaka hivi karibuni tumelizungumza humu ndani ya Baraza hajalipwa fedha zao. Sasa ikiwa mimi sihusiki na wizi ule, lakini mimi ni muathirika nina kosa gani nisilipwe mshahara wangu. Tulitaka humu ndani tuhakikishiwe kuwa watu hawa wamelipwa fedha zao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwamba suala hili limekwisha au bado waathirika hawa wanaendelea kuathirika kwa kosa ambalo halikuwa lao wote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo napenda kulizungumza ni suala zima la vitambulisho na nisingependa kurudia kwani mengi yameshazungumzwa katika suala hili. Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema “hakuna sikio lisilosikia la wengi”. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba wenzetu wamesikia kuwa suala zima la vitambulisho, uandikishaji na *ownership* yake lina matatizo. Mhe.Mwenyekiti, kama leo tunaambiwa na ushahidi unaletwa ndani ya Baraza kwamba kuna mtu ambaye ni raia wa Msumbiji ana paspoti ya Msumbuji lakini wakati huo huo ana kitambulisho cha Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi mwenyewe nilikwenda nikaiona hiyo hati ambayo imeletwa humo ndani kuthibitisha. Kweli nikakuta kwamba yule ambaye anaambiwa ni mtu wa Msumbuji hata alipochukua hicho kitambulisho cha Mzanzibari hakupeleka cheti cha kuzaliwa, kwa sababu pale penye tarehe ya kuzaliwa pameandikwa XX/XX/ mwaka wa kuzaliwa. Kwa maana huyu yeye ni mgeni hakupeleka cheti cha kuzaliwa, lakini bado amepewa kitambulisho cha Uzanzibari, na huku kuna malalamiko kwamba wazee wa nchi hii wengi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa wamenyimwa haki hiyo.

Kwa hivyo, naomba niseme sentensi moja tu katika hili kwamba wenzetu wana kazi kubwa ya kujipanga katika suala zima la kuhakikisha kwamba wenye haki zao katika kupewa vitambulisho hivi vya Mzanzibari ndio wanaopewa na wale ambao hawastahiki tuone tunawanyima kwa sababu athari yake baadaye itakuwa ni kubwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda niwe wazi kabisa nisingependa siku moja kuona niko Zanzibar anayekuwa Rais wa Zanzibar ni mtu kutoka Burundi au Rwanda.

Mhe. Mwenyekiti, kesho kutwa Julai tuna-*sign* Soko la Pamoja katika *East African movement* ya watu wanaotoka Burundi, Rwanda, Kenya na Uganda. Tutakuwa tunaingiliana sana katika mizunguko na ufanyaji wa biashara na

watu watakuwa huru. Kwa hivyo, nina wasi wasi kama Idara ya Vitambulisho haitajipanga vizuri basi tutakuja kumpa mtu hapa Uzanzibari hatimaye aje agombee Urais tuanze zogo huko tuseme siye huyo, huyo alikuja wakati wa Soko Huru. Jamani hayo mambo hayapendezi Idara ya Vitambulisho kazi mnayofanya ni nyeti, na unyeti wake unajionesha katika kila njia ile ni sawa sawa na haki ya raia katika nchi yake. Kwa hivyo, ningeomba walishughulikie sana hili.

Mhe. Mwenyekiti, pia utakumbuka wakati tunazungumzia bajeti kuu niligusia suala zima la kifungu kidogo cha bajeti kinachohusiana na mambo ya takrima. Niliuliza swali hapa katika kifungu hiki cha takrima. Takrima tafsiri ninayoijua mimi ni mambo yanayohusiana na viburudishaji, una mgeni umemkirimu au umemuweka hoteli na mambo kama hayo. Lakini nimeiangalia bajeti yote ukiacha ile ya Baraza la Wawakilishi ambayo inafahamika unyeti wake vile vile. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa 501 kifungu chao cha takrima mwaka jana kifungu hicho kimeitwa matumizi ya kazi zisizotazamiwa. Yaani kama litatokea lolote tu hivi basi fedha hiyo ndio imewekwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo ndio watu wanapoiba, utaambiwa linawekwa fungu kazi zake hazijuulikani. Kama itatokea tatizo lakini sasa hili linashtusha. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana katika bajeti fungu hilo katika kifungu cha takrima ambalo tumeliita matumizi ya kazi zisizotazamiwa lilikuwa na milioni 32 tu tumeidhinisha humu. Mwaka huu ni milioni 222 kuna nini?

Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda afisi zote nimetoa mfano hapa wakati wa bajeti Afisi ya Waziri Kiongozi, nimetoa mfano Mhe. Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi na afisi yako ambayo wewe ndio una wageni wengi na mambo tele, hakuna fedha hii mheshimiwa tunataka tuelezwe hii fedha ya nini. Kama milioni 222 tuambiwe labda kompyuta imeruka, lakini hili mimi siikubali. Kwa hivyo, ningeomba maelezo ya kina kabla ya kuikubali bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo ningeomba pia tuelezwe kwa nini bajeti nzima ya Idara hii ya Vitambulisho ime-*short* kutoka mwaka jana milioni 371 mpaka milioni 910 hivi kuna nini? Hapa pia tunataka tuelezwe jamani kama ni shughuli za maendeleo lina fungu lake. Kwa hivyo, hapa kuna shughuli gani zilizofanya mambo yapande namna hiyo wakati tayari taarifa tunaambiwa kwamba Wazanzibari waliokuwa *register* tayari asilimia 84 zimeshapita kwa hivyo aliyebaki ni mmoja mmoja na labda vitambulisho vya wafanyakazi na mambo kama hayo.

Lakini kwa kweli hii fedha ni nyingi na zaidi katika kifungu cha takrima, huku naweza nikapewa maelezo. Kifungu cha takrima matumizi ya kazi zisizotazamiwa milioni 222 hayakubaliki, hayapo popote kwenye kitabu chetu

cha bajeti tunataka hapa tuelezwe hasa ni yepi, labda kuna mambo ambayo sisi hatuyajui.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la mwisho ni suala zima la watoto wetu ambao wanakuwa jela. Kwa kweli mimi pia nimeguswa mno na hili suala si mara ya kwanza kulisikia humu ndani ya Baraza. Mwaka jana katika bajeti kama hii limezungumzwa na jana limezungumzwa tena na watu wengi na kwa uchungu sana kwa kweli linaumiza. Kwa hivyo, ningependa Mhe. Waziri aje na majibu nini atafanya kuwalinda watoto wadogo chini ya miaka 20 ambao wanakwenda jela kwa sababu ambazo pengine sisi wenyewe kama serikali hatukuweza kuwadhibiti wakafika kule. Ni kwamba tuweze kuwalinda watoto wetu na mambo maovu ambayo yanafanyika kule. Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri uje utusaidie katika hilo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia machache. Mhe. Mwenyekiti, nianze pale alipopaacha Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo vya mafunzo mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitoa jina hili akiwa na dhana muhimu sana, lakini kama tujuavyo Mzee Karume aliipenda sana Zanzibar na Wazanzibari wake ndio maana muda mfupi Mwenyezi Mungu aliomjaalia kuwa na sisi aliyafanya mengi makubwa na mazuri, miongoni mwao ni maakazi bora, televisheni za rangi kwa watu wazima na watoto walipewa nafasi yao kwa muda uliokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, Mzee Karume alijenga viwanja vya kufurahishia watoto, hii ni haiba kubwa dhamira yake ilikuwa ni kubwa sana kwa Wazanzibari na maendeleo yao. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa uchungu mkubwa na nimekasirishwa mno, jana nilipomsikia Mhe. Zahra Ali Hamad na taarifa walioikuta Chuo cha Mafunzo ni kwamba kuna vitendo vya kinyama vibaya visivyoweza kuvumiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri mwenye dhamana hii namuomba sana utakaposimama utupe majibu mwanana yatakayoliridhisha Baraza hili na Wazanzibari wanaonisikiliza ni hatua ipi dhidi ya wale wote watakaoonekana wanahusika na hili jambo baya linaloendelea kutendeka ndani ya vyuo hivi. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hilo hatuwezi kuidhinisha fedha hii itumike ndani ya chombo hiki kwa kuendelezwa vitendo hivi ambavyo havistahiki hata kutajwa machoni mwa watu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hili ni Serikali za Mitaa na Serikali Kuu zimesaidia mafanikio ya maendeleo kwa wenzetu Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti,

Tanzania Bara ni kubwa tunavyoielewa lakini inasikitisha sana kwamba hadi leo Zanzibar tumeshindwa kuliweka suala hili mahali stahiki. Mhe. Mwenyekiti, Serikali za Mitaa zinabanwa mno na Serikali Kuu kupata mapato yake hatimae tunasema kwamba Mabaraza ya Manispaa Unguja, Mabaraza ya Miji kwa Pemba na Halmashauri za Wilaya Unguja na Pemba kwetu sisi huwa ni serikali za mitaa.

Kwa hivyo, mimi nasema sidhani kama tunazitendea haki Serikali hizi za Mitaa na matokeo yake ni kushindwa kumudu shughuli zake ambazo tunawapangia, majukumu tunayowapa matokeo yake ni kuwakamua wale masikini, wavuja jasho, wapika uji na maandazi walipe kodi na kodi zenyewe hazipo kwani hawana pakupata fedha ilimradi ni vurugu na mwisho na wao wanashindwa kufanya wajibu wao kama ambavyo wangepaswa kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, mji wetu wote umejaa uchafu na inakithiri wageni tunawaita waje kwani Zanzibar ni njema atakaye aje, tunautangazia utalii kwani ni sekta yetu muhimu sana kwa maendeleo yetu ya kiuchumi. Lakini tunashindwa kujipanga angalau pale wanaposhuka katika viwanja vyetu vya ndege basi wakafika katika soko letu kuu la Unguja kwa kweli hali hairidhishi, Mji Mkongwe unanuka lakini la kushangaza ni kwamba watendaji ni wengi mno lakini kinachofanyika tunashindwa kufahamu na kuelewa juu ya jambo hilo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri mwenye dhamana hii alishughulikie jambo hili, kwani anao vijana wazuri kakae nao tena mupange jinsi gani ya kuutunza mji huu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni lile la kutoa mirathi kwa yule asiyestahiki hiyo ni dhima nzito. Mhe. Mwenyekiti, hili litamkugusa Mhe. Waziri kwa hiyo nakuomba sana uyasikie yale yote yaliyotolewa na ushauri uliopata ni kwamba watendaji wako wa afisi hii walione hili lina umuhimu wake la kumyima mtu yake ukampa asiyestahiki, hilo ni kosa. Kwa hivyo, sisi tumo katika mashirikiano na wenzetu Afrika ya Mashariki na Kati, hivyo si vyema hata kidogo kama walivyotangulia kusema wenzetu kuja kuiona Zanzibar tumeikodisha kwa wale wasiostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko ule wa takrima iliyoshtusha macho yetu kule kwenye afisi hii ningeshauri sana itolewe ama ipunguzwe Mhe. Waziri afikirie ni jinsi gani ataitumia fedha hii kuweka mustakbal mzuri kule kwenye Vyuo vya Mafunzo ili vijana hawa chini ya umri wa miaka 18 wapate nafasi yao ya kukaa waweze kupata mafunzo stahiki badala ya hali mbaya iliyoko sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako nakushukuru sana. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kupata wasaa huu kujaribu kumsaidia Mhe. Waziri kwa yale masuala ya fedha yaliyoguswa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri yeye mwenyewe ni mtaalamu wa fedha mengine atakuja kuongezea.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya hapo mimi niseme tu kwamba kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Dimani tunaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100, naomba sana waheshimiwa wenzangu tuwape fedha wizara ili wazidi kuimarisha shughuli zao za ulinzi. Pia waimarishe shughuli za maendeleo katika Halmashauri za Wilaya na Mipango Miji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ukikisoma kitabu hiki hasa huku kwenye majadueli na vitabu vya mwaka uliopita, ni kwamba kitabu cha mwaka huu kinaonesha mafanikio mazuri. Kwanza kinaonesha jinsi ya miradi katika Halmashauri ilivyotekelezwa, pia mipango yawe ya baadae kwa kweli inatia sura nzuri sana. Mimi niungane mkono na waheshimiwa waliozungumza kwamba iko haja ya kuwasaidia wenzetu kuwawezesha katika masuala ya mipango na fedha. Hili sio wao tu lazima tukiri kwamba sisi Wizara ya Fedha katika nyanja ambazo bado tunatilia mkazo sana ni suala la fedha kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba utunzaji wake, uwekaji kumbukumbu na matumizi hili ni suala gumu si kwa Tawala za Mikoa tu lakini kwa kweli niseme katika serikali nzima. Kwa hivyo, haya ni masuala ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo na sisi tutajitahidi kusaidiana na wenzetu wa Tawala za Mikoa tuwawezeshe katika nyanja hizi. Kwa hivyo, naungana sana fikra na mawazo ya waheshimiwa waliotoa kwamba tuwasaidie sana kuwawezesha wenzetu katika nyanja hii.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kufafanua mambo mawili tu. Kwanza ni ni hili suala alilouliza sasa hivi Mhe. Fatma nataka niunganishe na Mhe. Said Ali Mbarouk jana nae aliuliza hili suala kuhusu Afisi ya Mkurugenzi wa Usajili wa Vitambulisho kwamba anatumia zaidi kanuni kuliko sheria, kanuni ambayo ndio imeweka kigezo cha cheti cha kuzaliwa na sheria mama.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuhakikishia Mhe. Said kwamba kwa mujibu wa taratibu kanuni ni sehemu ya sheria ambayo utungaji wake huwa sheria mama lazima inaoneshwa, hivyo kanuni ya usajili wa Mzanzibari mkaazi imetungwa chini ya kifungu Nam. 16 cha sheria Nam. 7 ya mwaka 2005 ili kuleta utekelezaji mzuri wa sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la kiwango cha matumizi ya pesa cha shilingi mia tisa na kumi milioni. Naomba kumjuilisha kwamba kwa mwaka jana afisi

hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi mia tatu sabiini na moja milioni laki tano na thamanini. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hizo fedha zilizotajwa tofauti yake ni shilingi mia tano thalathini na nane milioni laki nne na ishirini.

Fedha hizi zimeongezwa na Wizara ya Fedha na Uchumi kwa makusudi kwa matumizi ya ulipaji wa Mikataba ya Ushauri wa Kitaalamu wa Masuala ya Teknolojia (*ICT*) tuna mikataba mizito pale na wenzetu tusiwafinye hilo ni kweli kabisa tunashirikiana na wenzetu wa upande wa Israil wanatusaidia na kweli wanafahamika. Mhe. Mwenyekiti, mradi wetu huu ni mzuri na unakubalika ulimwenguni, wewe kitambulisho chako kitoe popote kinakubalika.

Kwa hivyo, mheshimiwa nataka kukuhakikishia kwamba hawa wenzetu wanajitahidi na kitu wanachokifanya ni cha uhakika na cha kimataifa, sio kama kitambulisho cha Mzanzibari ni cha hapa hapa tu lakini huko kwengine utatakiwa pengine paspoti na umeisahau nyumbani basi wewe kitoe kitambulisho hicho wewe unapita bila ya wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, kazi kubwa zaidi na hawa wenzetu ma-*contractor* kwa mikataba yao ya ufundi pamoja na ununuzi wa malighafi, najua kuna vifaa hapa inabidi u-*replenish* mara kwa mara. Juzi nitatoa mfano waliniomba *block exemption* kwa vitu vinavyokuja mara kwa mara, nikawaambia ata *block exemption* huwa hatutoi sisi, inabidi kila muda mnapoagiza vitu basi mniombe msamaha tupitishieni, huo ndio utaratibu wetu. Kwa hivyo, hilo inaonesha kwamba ile kazi yao ni ya mwaka mzima inaendelea na wanahitaji fedha ziwe pale kwa muda wote.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ununuzi wa malighafi, lakini mheshimiwa hizi pesa ilibidi tuzitawanye ndio maana nyengine zikatiwa kwenye fungu la takrima alilozungumza Mhe. Fatma ameziona pesa nyingi zimewekwa huko. Kwa kweli tumezihamisha katika vifungu vyengine tumeona hivi vyengine visibaki. Hiyo hasa ndio sababu kubwa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nigusie suala alilouliza Mhe. Salmin Awadh Salmin suala la misamaha. Mhe. Mwenyekiti, suala hili nafikiri tulizungumza kwanza kwenye kamati, pili kwenye bajeti ya serikali tulipoipeleka kwenye kamati na hatimae Mhe. Salmini nikamkutanisha na mtendaji mkuu wa wizara wakakaa zaidi ya masaa mawili wanafahamishana, kama hakuwa *convinced* Mhe. Salmin mimi ninachosema ni kwamba tunamkaribisha yeye kama mwenyekiti sisi milango yetu iko wazi, tuje tukae nae na wizara pamoja na Halmashauri wenyewe tuone.

Lengo ambalo nataka kulisema sana Mhe. Salmini ni kwamba hii *concept* nzima inaelekea misamaha labda *personal* yeye haitaki au haipendi. Nafikiri ikiwa kitu kiko *correct* kinakukereketa wewe tu, hilo haikubaliki hivyo, nchi imeamua kwamba sera yetu ya uwekezaji tuweke jambo la kuwavutia wawekezaji, jambo hilo hatufanyi sisi Zanzibar peke yetu hilo ni jambo la dunia nzima.

Mhe. Mwenyekiti, aliondoka hapa mtu alikuwa na kiwanda chake cha mafuta pale Sebleni aliomba tumpe *monopoly* ya miaka 10 kuzalisha mafuta, tukasema ata hatukupi *monopoly* hatuitaki. Mhe. Mwenyekiti, basi anasema kuondoka tu kenda Malawi amepewa miaka 10 *exemption*. Sasa hivi ni sera tulizoziweka wenyewe, kama sera tumeziweka wenyewe basi tuziheshimu.

Kwa hivyo, tunaposema kwamba misamaha imejiri ada tunakosa mapato mengi. Hilo si kweli nafikiri Mhe. Salmin kidogo hapa aliteleza aliposema mafuriko ya misamaha imezidi mno, tunapotosha mapato serikali hilo sio kweli hapa kuna buku hili kila mwezi *TRA* wanaitoa hii ya uwazi kabisa kuhusu kodi zote. *ZRB* nao wanatoa ripoti za kila mwezi inaonesha *performance* yetu kwenye kodi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mwezi wa pili makusanyo yetu yalikuwa bilioni 7.6 hili nililisema wakati nawasilisha bajeti yangu. Mhe. Mwenyekiti, makusanyo haya nilitoa mfano miaka 10 iliyopita ilikuwa labda makusanyo ya karafuu kwa mwezi mmoja tu. Mhe. Mwenyekiti, hii *investiment* ya kodi tunayoikusanya sasa hivi tumeipata kwa *investiment* kubwa iliyofanywa ndani ya nchi. Jambo hili lazima tulikumbuke kwa hii sera safi ya uwekezaji ambavyo vivutio vyake ni misamaha ndio maana tukapata *more investiment* katika nchi yetu. Hili suala naomba sana tulikumbuke na tulizingatie.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana 2009/2010 kulikuwa na miradi ya uwekezaji 34 yenye thamani ya shilingi dola za Kimarekani 270.4 iliidhinishwa. Mwaka huu wa fedha 2010/2011 tunategemea kufanya tathmini ya miradi mipya 60. Hii yote inaonesha vile tunavyojitanua na kuwakaribisha wageni ndio maana inakuja miradi mingi. Kwa hivyo, unaposema kwamba misamaha mingi tuiachie tu hawa hawatokuja watakimbia tu, hizi sera lazima tukumbuke kwamba hizi ndio sera za kisasa za kutanua uchumi.

Kwa mfano, wewe mheshimiwa leo labda unapigisha taarab unataka watu wengi waje, basi ukiweka kiingilio cha shilingi 5000 basi uhakikishe haingii mtu, lakini weka shilingi 2000 tu ukumbi utajaa wote. Kwa hivyo, leo tukikaza mikanda yetu, tukiomba misamaha, zuia hivi hivyo itakuwa haji mtu hapa na hatutopata fedha za kuendeshea serikali. Mhe. Mwenyekiti, hili nimeomba

nilitilie mkazo sana na kama nilivyosema sisi tuko makini sana, hatusinzii na tunajitahidi sana.

Lakini ikiwa kesi moja kwenye kesi 1000 basi sisi tunakubali, na hayo aliyoyaona Mhe. Salmin sisi hatukuzipata kwa undani, sisi barua katuandikia Katibu Mkuu wa Wizara anaiombea Halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, naomba wafahamu sana kwamba misamaha yote inayoombwa ndani ya Wizara ya Fedha basi barua huwa anaandika Katibu Mkuu yeye ndiye aliyekuwa na dhamana na tunamuamini kwamba anaandika kuomba msamaha. Mhe. Mwenyekiti, miradi yote inayokuja ndio hivyo hivyo barua zote huwa anaandika yeye. Mhe. Mwenyekiti, huo ndio utaratibu ulivyo.

Kwa hivyo, kama kuna matatizo kwenye utekelezaji huko tunakubali na tutalifuatilia hilo na tuna kitengo chetu kule kwenye kodi. Kwa hivyo, tutawapa kazi wafuatilie ili tuone tatizo ni lipi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kitabu chetu mwaka huu cha hotuba tumekiri kwamba kweli kuna mianya na hii tukatoa mfano tukasema kwamba lengo letu mwaka huu ni kuona kuwa kabla ya kuongeza kodi juhudi zinachukuliwa kwanza katika kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na uajibikaji wa ulipaji kwenye vianzio vilivyopo. Miongoni mwa maeneo yatakayoangaliwa ni uimarishaji zaidi wa usimamizi wa mapato yasiyo na kodi na ufuatiliaji wa matumizi ya misamaha ya kodi. Lengo ni kuhakikisha kuwa misamaha inayotolewa inatumika kwa dhamira inayokusudiwa. Hili tumelisema wazi wazi katika hotuba yetu ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo mimi namuunga mkono sana Mhe. Salmin anaposema tuzidishe juhudi zetu, tuimarishe na tujitahidi kwa hii misamaha. Mwenyekiti, tunakubali hakuna aliyekamilika isipokuwa mwenyewe Mwenyezi Mungu lakini kama nilivyosema kesi moja sisi watu wa takwimu kwenye kesi 1000 hilo ni jambo dogo tu. Kwa hivyo, namuahidi Mhe. Salmin tutashirikiana mimi namuomba hivyo vianzio vyake tukae pamoja na yeye tutashirikiana na hawa watu wa *investigation* kuna kitengo maalum kwenye *ZRB* na *TRA* wanafuatilia msamaha uliotolewa umetumika ndivyo. Kwa hivyo, hili tutashirikiana pamoja tuone kama kuna tatizo basi tutachukua hatua ipasavyo, hatukatai Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa kuunga mkono hoja na naomba sana yakitokezea kama haya tuambizane. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kabla sijamwita Mhe. Waziri nawaomba wale waheshimiwa ambao niliwaita wakawa hawapo watanisamehe kwa sababu ya muda tunatakiwa sasa hivi tusikilize majumuisho kutoka kwa Mhe. Waziri kwa

kujibu hoja zetu na baadae tuweze kupitisha vifungu ili hoja hii tuimaliza asubuhi.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niongeze kidogo kwa yale ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ameyazungumza kuhusu suala zima la kodi. Kwa haraka haraka kutaka kujua *tax exemption* ina umuhimu gani katika *investiment* nenda ukanda wa pwani wa Mashariki utayakuta majengo ambayo kwa vyovyote kwa Mtanzania yeyote asingeweza kuyajenga. Unapotaka kuwaita *investors* lazima uwe na kivutio na kivutio ndio muhimu na kivutio cha kwanza kinakuwa ni suala la *exemption*. Kwa hivyo, unakuja kujenga unapewa *total exem*ption ya vifaa vyote ambavyo unataka kujengea hapa. Akishamaliza kujenga lile jengo hakuna hata siku moja ambapo mtu anaweza akaliweka mgongoni akaondoka nalo. Sasa utaikuta nchi namna inavyobadilika kutokana na *tax exemption.*

Hiyo ni kwa haraka haraka na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha kalielezea vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakwenda kwenye ufafanuzi wa hoja ambazo kwa kweli zimekuwa nzuri na zenye kuchangamsha. Niseme kwamba nimeridhika kwa michango ambayo imekuwa ikitolewa. Michango yenyewe waliotoa kila mtu alitumia ufundi wa kuweza kuyaeleza yale ambayo wizara itabidi ijieleze ili ipate kuidhinishiwa pesa ambazo zinahitajika kwa matumizi ya wizara mbali mbali au Wizara yetu ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wote waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara yangu. Karibu waheshimiwa si chini ya 20 hivi wamechangia wakiongozwa na Mhe. Haji Mkema Haji (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) pamoja na Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ).

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale ambao wamepata bahati ya kuchangia ni kama hawa wafuatao:-

1. Mhe. Haji Mkema Haji (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala)
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Waziri Kivuli Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ)
3. Mhe. Omar Ali Jadi
4. Mhe. Said Ali Mbarouk

5. Mhe. Ali Denge Makame
6. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
7. Mhe. Salmin Awadh Salmin
8. Mhe. Najma Khalfan Juma
9. Mhe. Haji Faki Shaali
10. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji
11. Mhe. Zahra Ali Hamad
12. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
13. Mhe. Ali Moh'd Bakari
14. Mhe. Salim Abdalla Hamad
15. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
16. Mhe. Zakiya Omar Juma
17. Mhe. Abass Juma Muhunzi

**UTARATIBU**

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mtu wa tatu kuchangia lakini kwa bahati mbaya sikusikia jina langu ili kuweka *hansard* vizuri.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** kwa hivyo ninaendelea.

18. Mhe. Omar Ali Shehe
19. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
20. Mhe. Juma Duni Haji
21. Mhe. Mkongwe Nassor Juma
22. Mhe. Rashid Seif Suleiman
23. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
24. Mhe. Assaa Othman Hamad
25. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi
26. Mhe. Ali Suleiman Ali

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla Waheshimiwa wote waliochangia wameipongeza wizara yangu na sehemu nyengine wamesema wanataka maelezo na pia taasisi zote za wizara yangu zinaendelea kufanywa. Kaw hivyo, kuanza naanza na Mhe. Haji Mkema (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala) katika michango yake kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza nimshukuru kwa kuunga mkono hoja baada ya kutupongeza kwa utendaji mzuri wa kazi na ushauri wake tunaupokea. Pia kuzingatia maslahi ya askari wa vikosi vyetu vya SMZ na tayari maslahi hayo tumekuwa tukifanyia kazi katika bajeti ya mwaka huu. Ili kuepuka Kikosi cha KMKM kuendelea

kutumia jengo la Afisi ya Wilaya ndogo Tumbatu katika bajeti ya mwaka huu, kikosi hicho kinakusudia kusimamia ujenzi wa kituo cha askari wa huko Tumbatu na jumla ya shilingi 85 milioni fedha hizo ambazo utakuta katika bajeti hii zimeombwa kwa kazi hiyo.

Aidha, kikosi cha Chuo cha Mafunzo pia kitasimamia ujenzi wa afisi ya Kamanda wake huko Wete Pemba, halikadhalika Serikali za Mitaa zitajitahidi kupanua wigo wa njia za mapato kama alivyoshauri Mhe. Haji Mkema.

Hapo hapo Mhe. Haji Mkema ametoa ushauri wa kwamba wizara yetu itashirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kuhakikisha kuwa wilaya zinapatiwa fedha kwa kupitia mpango wa *sub voucher.*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Juma Abdalla alitaka kujua suala la sheha anachaguliwa vipi na sheria nambari moja ya mwaka 1998 ni moja ya sheria ambayo imemuweka sheha na kwamba pia ni mdau katika afisi ya vitambulisho hususan katika kutambua makaazi hayo. Hivyo kazi yake kuu ni kumtambua mkaazi yeyote pasi na kujali ni wa chama gani.

Sheha ni mtu anayekubalika katika mji na kiutendaji na ni mtu anayeaminika kwamba si mtu ambaye ana kauli za uongo uongo. Ni kauli nzito anazokwambia kwamba umezaliwa nyumba fulani, pahala fulani na mara nyingi masheha huchukuliwa kutokana na eneo ambalo amekuwa akiishi toka utotoni mwake mpaka kufikia umri wa uzee. Kwa hivyo, mengi anayoyasema ni kwamba anayajua na ameyaona na anaweza kuyathibitisha. Lakini akitokea mtu yeyote sheha ambaye ni mbaguzi anababaisha babaisha, basi serikali haichelewi kumuondoa sheha huyo na kumtafuta sheha mwengine mwenye maadili mazuri ya utendaji kazi ambayo yenye dhamana kubwa katika shehia yake.

Mhe. Abdalla Juma (Waziri Kivuli wa wizara yangu) pia katika kumtambua mkaazi ametaka kufahamu ikoje. Kwa hivyo, kutokana na kuishi kwake kwa muda mkubwa katika eneo hilo kwake yeye inakuwa si tabu kubwa sana kuweza kumtambua kwamba huyu ndiye au siye.

Kuhusu Mzanzibari halisi na Uzanzibari ni sheria iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi na sheria ya nambari 5 ya mwaka 1985 imetoa tafsiri ya Mzanzibari. Hivyo Idara ya Usajili na Utoaji wa Vitambulisho hutumia sheria hizo katika kutoa vitambulisho kwa muhusika.

Kuhusu tatizo la ujenzi duni wa Afisi ya Wilaya Ndogo Kojani, wizara imeliona na kumtaka mkandarasi arekebishe kasoro zilizopo na ndio maana hajalipwa fedha zake zote. Hata hivyo, wizara italisimamia suala hili

kuhakikisha mkandarasi anatekeleza makubaliano na kupata haki yake na kumaliza mkataba kama tulivyokubaliana. Kwa kuwa wizara imeliona suala la ukosefu wa umalizikaji wa hilo jengo, wizara itakuwa karibu sana na kuhakikisha kwamba ukamilishaji wa jengo ambalo limechukua muda mrefu pale kwamba unakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la KMKM kukosa rada. Chombo cha kuweza kuona mbali ni chombo muhimu katika ulinzi wa nchi na ni chombo ambacho kama hakikupatikana inakuwa ulinzi wa nchi yako haukukamilika. Kwa hivyo, kwa kuwa wizara imeliona suala hilo la ukosefu wa rada katika Kikosi cha KMKM, katika ibara ya 119 ya hotuba yangu nimeeleza hatua zitakazochukuliwa na kasoro hiyo iliyotokea ambayo tunaendelea nayo kwa muda kidogo.

Rada zilikuwepo bahati mbaya zilikuwa zimeharibika ambazo tulipata msaada kutoka Ujerumani. Kwa hivyo, hatua zipi zitachukuliwa, ni kuliona suala hilo na kuendelea kufanya utafiti wa kutosha ili suala zima la ulinzi liweze kukamilika.

Kuhusiana na utumiaji wa kanuni kuliko sheria, kwa mujibu wa sheria ni kwamba kanuni ni sehemu ya sheria mama ambayo utungwaji wake huwa sheria mama lazima ioanishwe. Hivyo kanuni ya usajili wa Uzanzibari Mkaazi imetungwa chini ya kifungu nambari 16 cha sheria nambari 7 ya mwaka 2005. Kwa hivyo, hii huleta utekelezaji mzuri wa sheria hiyo.

Kuhusu kiwango cha fedha za matumizi ya kawaida shilingi 910 milioni, bajeti ya mwaka jana afisi iliidhinishiwa shilingi 371 milioni. Hili ameshalitolea ufafanuzi Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Namshukuru kwa pongezi na namshukuru kwa kuunga mkono hoja. Michangio yake imegusia kuhusu suala la taa za barabarani eneo la ng'ambu. Baraza la Manispaa limeshafunga mkataba na Benki ya Dunia kwa kuweka taa katika eneo lote la Mji kwa gharama za Dola milioni mbili.

Aidha, fedha zinazokusanywa kutokana na maegesho ya magari ya usiku, gari huwafuata vituoni mwao na kuwapelekea ofisini kuziweka kabla ya kwenda majumbani mwao. Hata hivyo, serikali imepokea malalamiko ya wafanya biashara mbali mbali na watumiaji na tunaendelea kulifanyia utafiti na kuona vipi tutakwenda baada ya majadiliano ya hapa na pale ambayo *the end of the day* naamini masikilizano ya eneo hili yatafanikiwa.

Pia serikali imepokea malalamiko ya wafanya biashara wa Soko la Mikunguni juu ya ongezeko la ada na linafanyiwa kazi. Soko hilo kwa muda wote huu

limekuwa wafanya biashara wengi waliokuwemo ndani wametoka nje. Kwa hivyo, umuhimu wa soko hili ambalo limejengwa la kisasa limo katika kufanyiwa kazi ili wafanya biashara walioko nje waweze kurudi ndani na kuendelea na biashara zao.

Kuhusu tatizo la taka katika mitaro hili ni suala zito, kubwa na ni suala linalohusu jamii nzima. Lazima Manispaa ipate ushirikiano wa wananchi wote kwa ujumla ndio litafanikiwa. Kwa sababu taka zinatupwa na wapiga kura wetu na huwa zinatupwa wakati wa mvua. Mvua inanyesha huku watu wanatupa taka matokeo yake yeye mwenyewe ndiye anayekuja kuathirika. Ndio maana nikasema hili sio tatizo la Baraza la Manispaa peke yake, lakini linahitaji mashirikiano yetu sote kuanzia viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla. Hatuna budi kuelimishana juu ya umuhimu wa usafi na utunzaji wa mazingira.

Kuhusiana na usambazaji na ulipaji wa bili za umeme. Halmashauri ya Wilaya ya Kati ndio itakayogharamia usambazaji na kulipia bili za umeme huo.

Mhe. Mwenyekitri, michango ya Mhe. Omar Ali Jadi kuhusiana na suala la Kojani hili limeshafafanuliwa. Lakini ushauri wake kupata vifaa vya kazi na usafiri Kikosi cha KMKM tumelipokea na tutalifanyia kazi. Mifuko 60 ya ujenzi wa vyoo Kojani lilitolewa kwa awamu mbili, mifuko 30 ya kwanza ilitolewa mwaka wa fedha 2008/2009 na mifuko 30 ya awabu ya pili yenye thamani ya shilingi 420,000/- ilitolewa mwaka 2009/2010.

Vitambulisho maalum vya wageni vinatolewa kwa wasiokuwa Wazanzibari na hawana sifa za kupiga kura.

Mchango wa Mhe. Said Ali Mbarouk Mwakilishi wa Jimmbo la Gando alitaka stendi ya magari iimarishwe. Kwa mwaka huu 2010/2011 tumetenga milioni tatu kwa ajili ya stendi hiyo.

Kuhusu vyoo vya mji wa Wete kwa mwaka huu wa 2010/2011, tuna azma ya kuvifufua vyo vyetu vitatu viliopo Mtemani Sokoni na Bandarini Pwani na kuboresha choo cha soko la matunda.
Kuhusu kuanzishwa bustani nyengine nje ya Wete, ushauri tumeuchukua na tutaufanyia kazi. Na mtaro wa Kizimbani kuangaliwa tena, ushauri tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Ali Denge Makame namshukuru kwa pongezi na kuunga mkono hoja yangu. Ushauri wa wauza samaki Darajani na kukipatia zana kikosi cha KMKM na masheha kupatiwa maslahi tutachukua tukifanya kazi pamoja hayo yashatolewa ufafanuzi.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui Idara ya Vitambulisho haifanyi kazi kisiasa. Kazi inayofanya ni zile tu zinazopitishwa na Baraza letu tukufu. Sheria ya vitambulisho imepita katika Baraza letu tukufu na mengi yaliyochangiwa ndio yameingia katika kitabu hicho na kufanyiwa marekebisho na hivi sasa yamekuwa yakitumika vile sheria na kanuni zilivyopitishwa na Baraza hili. Sehemu yoyote ambayo itakuwa inakwenda kinyume na sheria, basi hatua za kiutaratibu za kwenda kwa vyombo vinavyohusika ili uweze kupata haki yako uliokuwa umenyimwa kwa muda mkubwa inatumika. Kwa hivyo, idara hii haifanyi kazi kisiasa wala haimpendelei mtu inafanya kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa.

Kuhusu vitambulisho 12,000 vilivyotolewa Jimbo la Donge na raia wa Msumbiji kupewa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Wizara yangu haitaliacha suala hili na italifuatilia na Mheshimiwa tutaomba kupata ushirikiano wako ili kuweza kulikamilisha suala hili kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Salmini Awadh Slamin yeye amekubaliana nasi kwa vitambulisho vinavyotolewa vya usajili kuwa ni bora na vinakwenda na wakati tulionao. Inatumia *2D barcode* ambayo hubeba taarifa muhimu za kuwawezesha kutambua mtu kama alama za vidole, picha, majina na kadhalika. Lakini vitambulisho vya taifa ni utaalamu mwengine ambao hutumia *chipped* na ni gharama zaidi na hata kimatumizi.

Kuhusiana na msamaha wa saruji Wilaya ya Kati umetolewa kwa mujibu wa sheria. Halmashauri kupitia muhisani wake, imepata pesa za kuagiza saruji na wao watampatia eneo la kujenga maduka kwa mkataba maalum. Saruji hiyo itatumika kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi kama umalizaji wa ujenzi wa ofisi ya Halmashauri, ujenzi wa soko la samaki Chwaka, kuendelea na ujenzi wa skuli mbali mbali za Wilaya ya Kati na pia makubaliano hayo yamepitishwa kisheria katika kikao cha Baraza la Halmashauri. Miradi hii ni 24, ni ya 2010/2011 na yenye thamani ya shilingi milioni mia moja kama inavyooneshwa kwenye kiambatanisho 12 ‘J’.

Mhe. Najma Khalfan Juma namshukuru kwa ushauri alioutoa na indhari alizotoa juu ya vikosi vyetu vya SMZ na hatua za uboreshaji wa mazingira Unguja na Pemba. Aidha ushauri wa kubadilisha Miji, Manispaa na Halmashauri linategemea vigezo maalum kimataifa na kwa sasa miji yetu haijafikia vigezo hivyo kikamilifu. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya watu, miundombinu, pamoja na huduma za jamii.

Kuhusiana na soko la matunda la mji wa Chake Chake. Soko hilo ni kweli ni dogo, kongwe na halikidhi haja kwa watumiaji kwani soko hilo limejengwa tangu mwaka 1925 wakati watumiaji wa soko hilo walikuwa ni wachache sana.

Kwa hivyo, Baraza la Mji limeamua kujenga soko jengine sehemu ya Machomane na la zamani kulifanyia ukarabati. Pia Baraza hilo lina azma ya kujenga soko jengine la matunda na samaki katika mtaa wa Madungu Mwanamashungi. Kuhusu soko la zamani la samaki la Chake Chake litaendelea kukarabatiwa ili wachuuzi waendelee kulitumia.

Kuhusu magari katika mji wa Chake Chake kuzagaa ovyo kwa sababu ya steni ya Chake kuwa ndogo. Baraza la Mji sehemu ya ChakeChake lina mpango madhubuti wa kujenga steni mpya katika eneo liliopo karibu na mava ya Mbarouk Chake Chake. Suala hili nilisema nitaliangalia na nitakwenda kuliangalia na sehemu hii nilikwenda siku ya Jumamosi na nimekwenda kuangalia eneo hilo ni *opposite* ukitokea Machomane Skuli ya Michakaeni upande ule ule wa kushoto.

Wanatazamia kupata msaada na baadhi ya fedha kidogo zimepatikana na kuweza kuwapa fidia wale wenye vipando vyao au mazao yao katika sehemu hii. Sehemu ni nzuri, kubwa ya kutosha kabisa, kwa hivyo *departments* zote za maduka, barabara, soko, zote zinaweza kuingia katika eneo hili.

Mhe. Haji Faki Shaali Mwakilishi wa Jimbo la Mkanyageni. Suala la mapungufu katika serikali za mitaa uliobainishwa na utafiti ulioutaja sio mageni sana kwa wizara. Tafiti nyingi kabla ya hapo zimefanyika na kubainisha hayo ndio maana serikali ikaanzia na mchakato wa mageuzi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ushauri uliotoa kuhusu ubovu wa afisi za Wakuu wa Wilaya na ukamataji wa magendo ya karafuu utazingatiwa na kufanyiwa kazi. Tunakushukuru sana kwa mchango wako.

Kuhusu madai kwa mujibu wa utaratibu na usajili kila Mzanzibari mwenye sifa za kisheria anasajiliwa. Ni kwamba anatakiwa afike katika afisi ya usajili akiwa na barua ya sheha ambayo ni muhimu na cheti cha kuzaliwa kuthibitisha taarifa zake kuwa ni sahihi. Na asiyekuwa na cheti cha kuzaliwa, kiapo cha Mahakama kinaweza kutumika.

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji namshukuru kwa kuvipongeza vikosi vyetu vya SMZ. Tumepokea pongezi yako na kuwa Afisi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Masheha kwa kusimamia vizuri uandikishaji wa wapiga kura.

Kuhusiana na mifuko ya *plastic* nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa mifuko ya *plastic* bado ni tatizo. Lakini kama nilivyosema hapo mwanzo bado tunahitaji kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha suala hili la mifuko halirudi tena. Na kwa sehemu ambayo mifuko hiyo imekuwa haipo macho yanaangalia

katika eneo hilo linaridhika kwamba sehemu kubwa sasa hivi ya mifuko haipo au imetoweka.

Kwa hivyo, juhudi ya pamoja inahitaji kulishughulikia suala hili, kati ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji, Idara ya Mazingira, Baraza la Manispaa, Wafanyabiashara wenyewe na wananchi kwa jumla wote wanahitajika kulivalia njuga suala hili la mifuko, ili *end of the day* tuweze kuwa na mji safi na unaotazamika. Kwa hivyo, mifuko hiyo lazima tuichukulie hatua kwa pamoja ndio tutaweza kufanikiwa katika zoezi hili.

Mhe. Zahra Ali Hamad viti maalum, nimepokea hoja ya wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Chuo cha Mafunzo imefanya mabadiliko ya makaazi kwa mahabusu watoto. Tumeshauriana watoto watengwe mbali na kuhusu huyo askari amechukuliwa hatua za awali za kukatwa robo ya mshahara wake kwa kosa la nidhamu na yupo chini ya uangalizi wa mwenendo wake na hatua zaidi zitachukuliwa.

Suala la Mhe. Zahra ni suala zito na sio suala ambalo ni la kufanyia masihara. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa asubuhi kabla sijaja huku nimepita Chuo cha Mafunzo kuangalia maelezo yanayofanana na yale ambayo Mhe. Zahra Ali Hamad aliyatoa hapa. Kama tujuavyo jengo lile limejengwa tokea mwaka 1930 na hivi sasa limeshachoka. Kwa kuwa bado uwezo wa kujenga gereza jengine hatuna lakini nia bado ipo. Hatutosita kuendelea kutumia mbinu mbali mbali ili tuhakikishe tunapata Chuo cha Mafunzo kipya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi kuna idadi ya watu sita ambao ni vijana waliofungwa kwa makosa mbali mbali. Sehemu wanayolala ni nzuri kwa sababu hapo zamani ilikuwa imetengwa kwa watu mashuhuri.

Eneo ambalo kati ya watoto hapo wanapoishi na huko sehemu ambayo tunatarajia kwamba watakuwa ni wahalifu wa kuweza kuwadanganya watoto iko mbali. Chuo cha Mafunzo kina wakati wake wa kulala, ina maana wanaingizwa ndani saa kumi na moja mpaka asubuhi. Sasa swali la kujiuliza, hayo mengine ambayo yalikuwa yamezungumzwa inatokana na wapi.

Hata hivyo, tutaendelea kulifanyia uchunguzi lakini suluhisho hasa ni kuwahamisha sehemu ile wawe katika eneo la kuishi vijana peke yao. Pasiwe na mlango wa aina yoyote wa kupita au wa kutoka, ni eneo *totally* litakuwa ni la vijana wetu. Ningekuombeni kwa pamoja tushirikiane tuhakikishe bajeti hii ya Idara ya Mafunzo inapitishwa ili ukarabati na uwekaji sawa wa jengo la vijana uwe unakamilika kwa haraka.

Kwa hivyo, mimi nitakuwa nalo jengo hilo kwa muda wote uliobakia na kuhakikisha kwamba hilo ulililoliona Mhe. Zahra Ali Hamad halitokei tena. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Ali Moh'd Bakari pia wamelizungumzia suala hilo. Lakini kuna suala la mradi wa maji safi kijiji cha Kanambe ni shilingi 200,000/=, ujenzi wa skuli ya Shumbaviamboni shilingi 360,000/=, ujenzi wa skuli ya Kinoe shilingi 200,000/=, uwekaji fusi Kwa Mbarawa Haji huko Tumbe shilingi 240,000/=, jumla ni shilingi 1,000,000/= kama kiambatanisho Nam. 12 (l) kinavyoonesha.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni pia ilisaidia wanafunzi wanaosoma katika mazingira magumu na majanga kama ifuatavyo:

1. Mwanafunzi Ramadhan Ali Shariff wa Micheweni anayesoma skuli ya Micheweni alisaidiwa shilingi 20,000/=.
2. Mwanafunzi Ziada Salim Maalim wa Tumbe anayesoma Chuo cha Kiislam Kiuyu alisaidiwa shilingi 60,000/=.
3. Mwanafunzi Rahma Kassim wa Wingwi Meli tisa anasoma Chuo cha Kiislam Kiuyu alisaidiwa shilingi 53,000/=.
4. Ndugu Omar Ali wa Sizini ambaye nyumba yake ilianguka kwa mvua alisaidiwa shilingi 180,000/=.

Jumla ni shilingi 313,000/= kama kiambatanisho Nam. 12 (l) kinavyoonesha.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wa Mhe. Salim Abdulla Hamad wa Mtambwe jitihada tulizozifanya kwa muda huu tumewaomba wenzetu wa *World Bank* ambao wametukubalia kutupatia gari mbili, moja ya taka ya tani tano, ya pili ni ya maji machafu na vipando vidogo vidogo kama vespa. Suala hili la upungufu wa watumishi wenye ujuzi tumeliona na hivyo tumewaomba wenzetu wa Idara ya Utumishi kutupatia nafasi za ajira kwa wafanyakazi hao na wametukubalia. Pia ni kweli kwa ofisi zetu zote za Pemba hasa Mabaraza ya Miji hawana mwanasheria. Mwanasheria atapatikana ataripoti Pemba tarehe 1 Julai, 2010.
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kuhusu ruzuku ya shilingi milioni 140 za Baraza la Mji Mkoani tumeshatumia shilingi milioni 112, zimebakia shilingi milioni 28. Hizi haziwezi kutumika kwenye miradi kwa sababu ni mishahara ya mwezi wa Mei na Juni, 2010 kwa watumishi wa Baraza la Mji. Pesa zinazotumika kwenye miradi ni zile zilizokusanywa na Baraza ambazo shilingi 13,305,900/=. Kuhusu mishahara ya Tawala za Mikoa iliyoibiwa, suala hili Mhe. Waziri wa Fedha amelitolea ufafanuzi zaidi.

Mhe. Abass Juma Muhunzi na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kuhusu rasimu ya awali ya Mpango wa Utengenezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa itakamilika

mwezi wa Oktoba, 2010. Utekelezaji wake ni sehemu ya program kubwa ya mageuzi ya utumishi wa umma Zanzibar. Matumaini yaliyopo kazi hii itamalizika ndani ya kipindi cha bajeti ya mwaka 2010/2011.

Kuhusiana na eneo la Darajani la wafanyabiashara linafanyiwa matengenezo kwa nia ya kuimarisha usafi na kuongeza mapato. Nia ni kuongeza usafi katika eneo na hapo hapo nia ni kuongeza mapato. Kwa hivyo, wale waliokuwepo pale zamani au wakongwe wa eneo lile basi wao ndio watakaopewa kipaumbele cha kuhakikisha wanawekwa na wale watakaokuja baadae wafuate baadae. Kwa hivyo, hili suala tutalifanyia utulivu wa kuweza kugawa zile sehemu ambazo wale waliokuwa wametangulia kwa siku nyingi wanapata nafasi mwanzo.

Kuhusiana na bustani ya Jamhuri imekodisha sehemu ya kuchezea watoto ili kuimarisha mazingira safi na kutunza eneo hilo. Suala la askari wa Kikosi cha Valantia Zanzibar ni wengi kuliko Zimamoto. Kutokana na sababu hiyo basi, ndio maana fedha zinatofautiana katika maposho.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la vikosi vyetu kwamba wanaitwa wapiganaji. Kwa hivyo, kutokana na neno hilo ni kwamba wanachangamka zaidi katika suala la upiganaji kuliko suala la ulinzi. Ukweli ni kwamba askari lazima awe mkakamavu, achangamkie kazi yake, awe muadilifu na wakati wote lazima awe yuko tayari kuilinda nchi yake na taifa lake. Mhe. Mwenyekiti, askari hafuati jina anapokwenda vitani, suala la jina mtafanya nyinyi wanasiasa. Lakini askari anakwenda kwa kazi aliyopewa, anakwenda kuifanya kazi akimaliza anakuja kuripoti nimeshakamilisha kazi uliyonipa anarudi katika kambi yake.

Kwa hivyo, tusikae tukaanza kujadiliana tu tuwape jina hili, jina hili labda linawapa utulivu, jina hili silo. Tuangalie kazi zao wanazozifanya sawa hivyo inatosha.

Kuhusiana na suala la sokoni, stendi hizi za gari tumeshalitolea ufumbuzi. Lakini ushauri mwengine ilieleza kwamba kuna baadhi ya mambo huwa tunashirikiana nao wananchi kabla ya kupata uamuzi. Hata uamuzi wa mambo ya *parking* za gari pia ni suala ambalo tutakaa tushauriane nao wananchi tena, ili kuangalia kwamba hakuna mkwaruzano kati ya wananchi wetu na askari.

Suala la namna ya kupata masheha waadilifu ambalo lilizungumzwa na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji sheria imepitishwa na utaratibu mzima wa kuwapata masheha hao. Yule ambaye anafanya kazi yake kwa uadilifu ataendelea kuwa sheha na kwa yule yeyote ambaye tunahisi anafanya kazi kinyume cha sheria hatua kali ya kumuachisha na kumchagua mwengine inatolewa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe mtu yeyote ambaye anao ushahidi wa kutosha wa kuelezea ufanisi au utendaji mbovu wa sheha yeyote wacha tushirikiane. Ninahakika kwamba sheha yeyote ambaye anakosesha hatua za kisheria na utulivu katika shehia anayoishi, anasema uongo katika sehemu mbali mbali, ni kitu cha kupeana taarifa ili tufanye uchunguzi haraka haraka na hatua zichukuliwe. Lakini bado tuna imani kwamba masheha wengi ni waadilifu labda asilimia moja au mbili inawezekana wapo ambao sio waadilifu.

Matatizo ya mshahara suala hili Wizara ya Fedha tayari Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji ameshalijibu. Pia kuhusiana na suala la kupata rais anayetoka nchi ambayo sio kutokana na ugawaji mbovu wa vitambulisho. Kama tutakuwa si waangalifu katika ugawaji mzima wa vitambulisho nakubaliana na kauli hii kwamba inawezekana mkampata kiongozi ambaye si Mzanzibari anakuwa rais. Lakini kwa imani yangu na kwa uhodari wa watendaji hawa wa vitambulisho wakianza kwa wazee wetu na vijana suala hili macho yetu yatakuwa wazi, masikio yetu yatakuwa wazi pia kuhakikisha suala hili halitokei hapa Zanzibar.

Suala la takrima tutaendelea kulifanyia utafiti. Hili ni suala zito kila mtu anaitafsiri takrima kwa njia zake. Lakini kwanza muhimu ni kuipata *proper definition* ya neno takrima. Hatuwezi kulitolea uamuzi bila kwanza kujua hii takrima ni kitu gani, inakuwaje hata unafikia pahala ukasema hii ni takrima au sio takrima. Kwa hiyo, kazi kubwa hapa ni kuweza kujua kuichambua zaidi mpaka tukafikia pahala tukasema hii ndio takrima. Ikiwa takrima ndio hii je, tutumie njia gani kuhakikisha takrima ile haitumiki kinyume na utaratibu uliokuwepo au adhabu inayotolewa inalingana na takrima.

Mhe. Assaa Othman Hamad tutakuwa pamoja tushirikiane kama nilivyosema pale mwanzo kuhusu uondoshaji wa taka kwa sababu maeneo mengi yameenea harufu mbaya za taka. Kama tulivyosema hapo nyuma kwamba taka zetu za mji wa manispaa ni nyingi mno ndio maana tunaomba magari tunakwenda sehemu mbali mbali. *World Bank* wamesema watashirikiana na sisi zaidi kuhakikisha watalii wetu wanapokuja katika mji wanajua kwamba kweli wamekuja kutembea Zanzibar na iko katika hali ya usafi na harufu nzuri inanukia katika mitaa yetu. Kwa hivyo, Mhe. Assaa tuko pamoja tushirikiane kuondosha uchafu huu katika eneo letu la Mji Mkongwe.

Kuhusu suala la Chuo cha Mafunzo nafikiri limeshatolewa ufafanuzi zaidi. Suala jengine kuhusu vitambulisho umeliweka pamoja na suala zima la mtu aliyekuwa hastahiki kurithi akarithishwa kutokana na vitambulisho hivi. Nataka nikubaliane na wewe ni kweli kama hatukuwa waangalifu kama nilivyosema tunaweza kupata rais kutoka nchi sio, tunaweza tukamrithisha mtu ambaye sie

na hiyo ni dhambi kubwa kwa Mwenyezi Mungu. Kuhusiana na mambo ya kodi ya msamaha suala hili Mhe. Waziri wa Fedha ameshalitolea ufafanuzi wa kutosha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi kuyajibu yale yote ambayo niliyaona na niliyasikia, lakini kama litabakia hili na hili basi nitakuwa niko tayari kutoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru kwa kunistahamilia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti yangu ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 17** | **-** | **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | |
| Kifungu 02 | - | Utawala | 12,167,000 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **12,167,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 18** | **-** | **CHUO CHA MAFUNZO** | |
| Kifungu 02 | - | Utawala | 27,144,000 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **27,144,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 09 - AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA SMZ**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 03 | - | Afisi Kuu Pemba | 185,349,000 |
| Kifungu 04 | - | Idara ya Mipango na Sera | |

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Waziri katika masuala yanayohusiana na Idara ya Mipango na Sera nilizungumzia mambo mawili. La kwanza ni suala la kanuni ambayo ameiingiza inayotatanisha shughuli za vitambulisho majibu yake nimeyasikia lakini sikuridhika nayo.

Lakini la pili ambalo ndio hasa nililosimamia ni suala la *sub-vote* za ofisi za wapiganaji wetu Pemba kwamba kukosekana kwake Kikosi cha Zimamoto, KMKM, JKU, Valantia na Mafunzo utaratibu wao wa kupata fedha kwa kweli kutoka Hazina unakuwa hauridhishi na unatatiza masuala ya utendaji wao wa kazi. Sasa bahati mbaya Mhe. Waziri alipokuwa anajibu hii hoja ameiruka kwa hiyo naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kweli itakuwa kidogo hakusikia lakini tumekubaliana nalo suala hili kwamba tutatekeleza vile ambavyo alivyoshauri.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kama amekubaliana na mimi katika bajeti hii *arrangement* itakuwaje ili ofisi za Pemba ziwe zinapata pesa kupitia Hazina moja kwa moja bila ya kupitia Makamanda waliopo Unguja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, hiyo tutashughulikia katika bajeti ijayo. Lakini ni kitu ambacho tunakipokea tutakifanyia utafiti nafikiri bajeti inayokuja tutakubaliana na vile ambavyo wewe ulishauri.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 04 - Idara ya Mipango na Sera

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ nilieleza wasi wasi wangu juu ya msamaha wa saruji uliotolewa na serikali. Lakini wakati wa majibu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) (MBLM) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi alieleza kwamba ushuru ni sehemu ya sera za serikali. Mimi naelewa hilo kwa sababu ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

Lakini pia alieleza kwamba nina *personal effect* juu ya misamaha. Mhe. Mwenyekiti, nataka kueleza kwamba sina *personal effect* yoyote katika Baraza hili. Mimi kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nawawakilisha wananchi

na ninayo haki ya kuhoji jambo lolote ambalo nina wasi wasi nalo. Kwa hivyo, sina *personal effect* bali ni jambo ambalo nalizungumza kila wakati, kila siku juu ya matumizi mabaya ya misamaha ya kodi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu msamaha wa kodi uliotolewa na Wizara ya Fedha na Uchumi ambao ilitoa msamaha wa ushuru wa forodha pamoja na *VAT* kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa barua yenye kumbukumbu WF/11/210/Vol. II ya tarehe 12 Mei, 2010 kwa madhumuni ya kusaidia miradi ya wananchi ya Wilaya ya Kati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, saruji iliyosamehewa ni kontena 50 zenye ujazo usiopungua pakti 250,000 zenye thamani ya milioni 114.8 msamaha wenyewe una thamani ya milioni 58. *bill of larding* ya karzai 001 ya tarehe 17/05/2010.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hilo tarehe 07/06/2010 mwezi uliofuata wa pili. Wizara ya Fedha na Uchumi ilitoa msamaha wa saruji kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kati kwa madhumuni hayo hayo. Katika barua yenye kumbukumbu nambari WF/A2010Volume 2 nambari 37 ya tarehe 07/062010, saruji iliyosamehewa ni kontena 100 zenye ujazo wa *packet* 500,000 zenye thamani ya milioni 229.9. Msamaha wenyewe uliotolewa ni wenye thamani ya milioni 116, kwenye *Bill of larding* ya Kazan 001 ya tarehe 24/04/2010. Jumla ya msamaha uliotolewa kwa miezi miwili yaani Mei na Juni 2010, ni milioni 174.

Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kati hadi Juni mwaka 2010 ilikwishakusanya jumla ya milioni 70,401,145 katika kipindi hicho. Miradi ya ujenzi 10 yenye thamani ya milioni 10 tu ilitekelezwa kwa asilimia 100. Ni dhahiri kuwa kuna nyongeza ya milioni 104 kutokana na msamaha uliotolewa.

Lakini Halmashauri ya Wilaya ya Kati katika kipindi kijacho cha mwaka 2010/11 inategemea kutumia jumla ya milioni 100 kwa miradi mbali mbali, ikiwemo miradi isiyo ya ujenzi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe fupisha, tunaomba uulize swali.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mtiririko huo ni dhahiri kuwa kuna dalili ya mchezo unaofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2009, kanuni ya 115(1) na kanuni ya 111(2) nilitaka niliombe Baraza lako tukufu, likubali kuundwa kwa kamati teule ya Baraza ili kuchunguza suala hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bado ninao muda wa kufanya kazi hii na bado naendelea kukusanya vielelezo juu ya jambo hili, bado tuna kamati ya fedha na uchumi ambayo nitaisoma katika kipindi nitakachokuja. Kwa hivyo, naomba suala hili niliache, lakini nataka kulihakikishia Baraza lako bado sijaridhishwa na majibu yaliyotolewa na Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi).*

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 04 | Idara ya Mipango na Sera | 1,177,421,000 |
| Kifungu 06 | Tawala za Mikoa na Serikali za Miji | 1,505,230,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **2,868,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 17 – JESHI LA KUJENGA UCHUMI**

Kifungu 02 Utawala Unguja

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri, niligusia juu ya suala la vikosi kutenganishwa na siasa. Nikamshauri Mhe. Waziri asiruhusu kambi za vikosi vyetu kutumiwa kwa shughuli za kisiasa. Pia nilimpa ushahidi kuwa kambi ya Chokocho mara moja ilitumiwa kuwa kambi ya umoja wa vijana wa CCM. Kuna sheria ya mwaka 2003, sheria nimeisahau ni nambari ngapi inayokataza askari kushirikishwa na mambo ya siasa. Kwa hivyo, suala hili hakuligusia chochote. Naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mjumbe atakubaliana na mimi kwamba kambi za umoja wa vijana hazipo siku hizi, hatuna kambi za umoja wa vijana. Vijana hawa ambao wameshiriki katika siasa nitalifuatilia na kwa wale ambao wanaleta siasa katika vikosi vyetu tutawachukulia hatua kama sheria zinavyosema.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hakunifahamu, sizungumzii askari mmoja mmoja kushiriki katika siasa. Ninachozungumzia ni kwamba kambi hii ilitumiwa na umoja wa vijana wa CCM kwa mafunzo ya vijana wake kiasi miezi mitatu. Hata ukitaka ushahidi hao vijana nawajua wengine, naishi nao mitaani, miezi mitatu waliwekwa kwenye kambi ya Chokocho umoja wa vijana na walikuja vijana kutoka sehemu mbali mbali Unguja na Pemba wakakaa pale.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri mimi na Mhe. Mbunge wangu tulikuwa bungeni Dar es Salaam kuna mtu hasa kiongozi wa umoja wa vijana Dar es Salaam akatuambia kwamba natoka katika Jimbo lenu kwenye semina ya umoja wa vijana iliyoko Chokocho. Kwa hivyo, ushahidi ninao wa kutosha Mhe. Mwenyekiti.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilichokuwa namuambia mimi ni kuwa, asikubali hata chama chake cha Mapinduzi kikatumia kambi za vikosi kwa siasa, kwa sababu sheria tuliyoipitisha katika Baraza ya mwaka 2003 inakataza.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 4,535,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **4,535,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO**

Kifungu 02 Utawala

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu suala la Chuo cha Mafunzo na kadhia ya jela ya watoto na yaliyotokea, tulitaka hatua zichukuliwe. Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba amekiri kuwa lile sio jambo la masihara. Lakini bado alisema kwamba hatua za awali alizochukua ni kuzuia robo tu ya mshahara wa huyo mfanyakazi. Hilo jibu mimi sijaridhika nalo kwa sababu nahisi bado ni masihara. Robo ya mshahara bado haijatosha kadhia ambayo wamekuwa wanatendewa watoto wetu. Tunataka hatua hasa zichukuliwe.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Waziri aniambie ni hatua zipi zinazokusudiwa kuchukuliwa na isijekuwa ni mchezo wa kuigiza?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, hatua hasa zitachukuliwa, baada ya kuthibitisha kulifuatilia hili suala na tukathibitisha kama ni kweli kitendo hiki kimefanyika. Kwa hivyo, sheria za serikali kuhusiana na kitendo kama hicho ndizo zitakazotumika kwa wakati huo.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakaribia kukubaliana na Mhe. Waziri, lakini bado nataka atamke bayana, kwa sababu sheria ni pamoja na

kumpeleka mahakamani. Sasa je, ikithibitika huyu mtu atapelekwa mahakamani?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Ndio Mhe. Mwenyekiti.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala | 3,766,000,000 |
| | Jumla ya Fungu | **3,766,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 29 – KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala | 6,109,000,000 |
| | Jumla ya Fungu | **6,109,000,000** |

**FUNGU 32 – KIKOSI CHA ZIMA MOTO NA UOKOZI**

Kifungu 02 Utawala Unguja

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba maelezo kidogo kuhusiana na jambo ambalo nilichangia kuhusiana na upotevu wa mishahara ambayo ilitokea kwenye kikosi hiki na wale ambao waliathirika hawakulipwa fedha zao hadi sasa. Jibu lake mimi sikulisikia na nilikuwa humu ndani wakati wote, nilikuwa naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, suala hili la upotevu wa fedha ni kweli umetokea, uchunguzi unaendelea kufanywa kwa wale ambao watachukuliwa hatua na utaratibu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ kukaa pamoja ili kuhakikisha wale ambao hawakupata mishahara yao wanalipwa kwa mujibu wa taratibu ulivyo.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili limekuwa ni la muda mrefu, mimi nakubali tuendelee. Lakini nimuombe Mhe. Waziri kwa heshima zote tafadhali walishughulikie suala hili, ili wanaohusika wapate haki zao. Tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 1,789,000,000 |
| | Jumla ya Fungu | **1,789,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila*

*ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 34 – KIKOSI CHA VALANTIA**

Kifungu 02 Utawala

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru tena Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni dogo tu. Katika michango yetu tulitaka kujua majukumu ya kazi za Kikosi cha Valantia, lakini sikumsikia Mhe. Waziri kutuambia hili, tulikuwa tunaomba kujua majukumu yake na sio kama yeye alivyosema kuwa jina unaweza kuwaita lolote. Lakini sisi hatukutaka jina, tulitaka majukumu ya kikosi hiki. Kwa sababu vikosi vyengine Zimamoto, KMKM vyote vinafahamika. Lakini hiki hatufahamu majukumu yake wengine.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, majukumu yake ni ulinzi wa usalama wa wananchi pamoja na mali zao.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nimecheka kidogo, kwa sababu kuna na askari polisi wana jukumu hili hili. Sasa KMKM wao tunajua moja kwa moja ni kwenye mambo ya magendo na kulinda bahari. Sioni kama hiyo itakuwa ndio kazi, inawezekana ni miongoni mwake, lakini ziada ya hapo tungependa zaidi kujua. Kwa sababu wanafanyakazi nyengine nyingi ambazo sisi tunakuwa tunashindwa kujua, ni jukumu lao au si jukumu lao. Ikiwemo na masuala ya kusimamia vituo vya kura na mambo mengine. Kwa hivyo, tungependa kujua zaidi Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri anayo maelezo. Kusimamia mitihani pia naambiwa wanakuwepo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza tufahamu kuwa Kikosi cha Valantia kimepitishwa hapa hapa kisheria. Kwa hivyo, nafikiria walikuwa na nafasi nzuri ya kutosha ya kupitia suala hili. Lakini kama vile nilivyosema ni kwamba askari yeyote kwanza anahakikisha panakuwa na usalama katika nchi yake, hiyo ndio kazi ya kwanza. Ndio maana panapotokezea kitu chochote, basi askari ndio wa mwanzo kupelekwa pale.

Kwa hivyo, nataka uchukuwe kwamba askari kazi yake ni kulinda usalama wa nchi pamoja na mali zao au na kazi yoyote ambayo watapewa na mkuu wa serikali.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Mhe. Mwenyekiti, naona inaelekea labda na Mhe. Waziri mwenyewe hazielewi, kwa sababu Mhe. Burhan Saadat Haji anamsaidia pale. Kwa hivyo nitamfuata baadae nijuwe zaidi. Kwa hivyo, tuendelee.

Kifungu 02 Utawala 2,182,000,000

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla ya Fungu | **2,182,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 37 – MKOA WA MJINI MAGHARIBI

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 04 | Mipango na Sera | 172,940,000 |
| Kifungu 05 | Wilaya ya Mjini | 285,652,000 |
| Kifungu 06 | Wilaya ya Magharibi | 202,408,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **661,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 38 – MKOA WA KUSINI UNGUJA

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 04 | Mipango na Sera | 170,014,000 |
| Kifungu 05 | Wilaya ya Kati Unguja | 269,176,000 |
| Kifungu 06 | Wilaya ya Kusini Unguja | 217,810,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **657,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 39 – MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Mipango na Sera | 137,640,000 |
| Kifungu 05 | Wilaya ya Kaskazini “A” | 254,029,000 |
| Kifungu 06 | Wilaya ya Kaskazini “B” | 193,595,000 |
| Kifungu 07 | Wilaya ndogo Tumbatu | 30,736,000 |
| | **Jumla ya Fungu** | **616,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila*

*ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 40 – MKOA WA KUSINI PEMBA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 04 | Mipango na Sera | 621,790,000 |
| Kifungu 05 | Wila ya Chake Chake | 233,958,000 |
| Kifungu 06 | Wilaya ya Mkoani | 194,252,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **1,050,000,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 41 – MKOA WA KASKAZINI PEMBA**

Kifungu 04 Mipango na Sera

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia shughuliza Mkoa wa Kaskazini Pemba hasa zile zinazosimamiwa na kitengo cha mipango na sera cha Mkoa, nililalamika kwamba katika Wilaya ya Wete na Micheweni mafungu yanayohusiana na msaada kwa jumla *general social welfare fund* hazikuingiziwa fedha mwaka huu. Bahati mbaya Mhe. Waziri hakuleta maelezo kuhusiana na suala hili. Naomba maelezo ya kadhia hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, suala hili sijafahamu alivyokusudia.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia shughuli za Mkoa wa Kaskazini Pemba, mambo ya mipango na sera nilizungumza kwamba katika vifungu vya *general social welfare fund* vya Wilaya ya Wete na Micheweni kwa mwaka huu havikuingiziwa hata shilingi moja. Nikamuuliza je, wale wezee wetu ambao wanapokea chochote, maana yake ni kwamba sasa watakuwa hawapati tena chochote au vipi? Kwa bahati mbaya Mhe. Waziri hakunijibu hilo swali, naomba maelezo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, suala hili itabidi tulifuatilie baadae.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, masuala haya yanahusu mustakabali wa wazee wetu. Sasa kupitisha fungu halafu ukaambiwa utafuata baadae ni mtihani kidogo Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Fedha na Uchumi bahati nzuri yupo, serikali nzima ipo. Kwa hivyo,

ningeomba jibu kwa serikali kuhusiana na suala hili ambalo ni muhimu sana kwa wazee wetu. Ni mtihani mkubwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na (MBLM) anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, labda atusaidie iko katika ukurasa wa ngapi, sijaipata kidogo.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ni katika ukurasa wa 468, kifungu 05 Wilaya ya Wete *sub vote* hiyo kifungu kidogo 12030.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Said Ali Mbarouk, huko bado hatujafika Wilaya ya Wete.

Kifungu 04 Mipango na Sera

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia niliuliza hili suala la *reform* ya *local government* ambayo imekuwa ikiahidiwa sana kwamba itatekelezwa hapa. Lakini nilikuwa nikimsikiliza Mhe. Waziri hapa, lakini sikusikia ambacho amekisema kuhusu hapa. Kwa hivyo, ninaomba maelezo kuhusu hili. Ni lini serikali itakamilisha mpango huu wa marekebisho makubwa ya serikali za mitaa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kijacho.

**Mhe. Mwenyekiti:** Anasema atarekebisha katika kipindi kijacho sio katika kipindi hiki cha fedha.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Mwenyekiti ni vyema tukaelezwa basi kwa sababu zilikuwa zikitolewa ahadi kwamba suala hili linashughulikiwa, basi Mhe. Waziri atuambie ni nini kilichoshughulikiwa katika *reform* yote hiyo, yaani hatua mbayo imefikiwa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, nadhani kwa kuwa itafuatiliwa katika kipindi kijacho cha fedha, kwamba suala hili litashughulikiwa baada ya bajeti hii. Sasa suala hili kwa hapa nadhani lingesubiri bajeti hiyo inayokuja. Ni wazo zuri umelitoa la kufanyia *reform*, lakini kwa mwaka huu wa fedha halikuwa *included*. Mimi nadhani tuendelee kwa hapa.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii kuhusu Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nilitangulia kusema kwamba kuna taarifa nyengine ambazo hazikuwa sahihi, na ni kuhusu moja katika kazi za utekelezaji wa mkoa kwa kushirikiana na wilaya husika.

Walisema kuwa wameshirikiana kupeleka maji katika vijiji vya Makongeni, Kivumoni, Machengwe, Mitambuni, Kinazini na Mkanjuni katika Wilaya ya Wete, ambapo vijiji hivi vyote vimo katika jimbo langu na ninavijua.

Kwa mfano, Kinazini na Mitambuni hakuna maji wala hakuna umeme. Kwa kufupisha ni kuwa kuna baadhi ya vijiji tu vina umeme lakini hakuna maji, yaani taarifa haikuwa sahihi kama ilivyo hapa. Katika kujibu Mhe. Waziri sikumsikia kusema chochote kuhusiana na suala hili, sasa sijui ataniambia nini.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na yeye kwa maelezo aliyosema kwamba taarifa sio sahihi. Kwa hivyo, itabidi yeye aifanyie kazi na mimi vile vile *(Kicheko/Makofi)*.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa jibu la Mhe. Waziri. Lakini nilivyosema mimi ni kwamba hii taarifa iliomo humu sio sahihi. Kwa mfano, kijiji cha Makonge kuna umeme tu maji hakuna, kijiji cha Kivumoni kuna maji tu umeme hakuna, kijiji cha Mkanjuni kuna maji tu umeme hakuna, vijiji vya Kinazini na Mitambuni hakuna maji wala umeme *(Makofi)*.

Kwa hivyo, nilisema hiki kitabu hakikuwa sahihi na suala hili nalizungumza kwa sababu nalifahamu. Suala hili limewekwa kwenye kitabu maana yake kama kusema hapo mahala pasishughulikiwe tena na mimi ndiye mtetezi. Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii sijaridhika nayo, Mhe. Waziri atanieleza nini *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala wa Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, sina mabadiliko ya maelezo yangu.
**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri anakubali kwamba atafanya mabadiliko.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, kwa vile taarifa ameikubali na amesema kwamba atafanya marekebisho. Kwa hivyo, namuomba anikubalie kufuata kama kilivyoeleza kifungu 6 kwenye ukurasa wa 37, kinachozungumzia masuala ya kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mbali mbali inayoendelea ikamilike.

Kwa hivyo, ajue kuwa haya mambo hayajakamilika na aniahidi kwamba atayakamilisha pamoja na kurekebisha hayo matatizo yaliomo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa kweli kama alivyosema kwamba amekubali basi na hilo pia atalifanyiakazi.

Mipango na Sera 412, 000,000/-

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa muongozo wako, ingawa pale ningeweza kupata maelezo ya wilaya zote mbili lakini hapa ni kwa Wilaya ya Wete tu.

Msaada kwa jumla mwaka huu kuna zero na Mhe. Waziri wetu amezoea kupata chochote. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi alitaka kunipa maelezo, kwa hiyo naomba maelezo ya serikali katika hili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, sasa lakini wewe mwenyewe ndiye uliyetaja Wilaya ya Wete na ndio maana tulikwambia Wilaya ya Wete bado haijafika.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hata mimi nimeshituka kuiona hii. Kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba tunaomba tulifuatilie, kwa kweli sina sababu ya msingi ya kueleza kuhusiana na suala hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Ustawi wa Jamii ukurasa wa 287 karibu na jumla, kuna msaada kwa jumla *General Social Welfare Fund* safari hii fedha zimewekwa hapa *(Makofi)*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, unakusudia fedha hizi zinataka kupelekwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kipindi hiki *(Kicheko/Makofi)*.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, masuala haya yanasimamiwa chini ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ. Sasa majukumu ya shughuli hizi za Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ni tofauti na yeye anazo shughuli zake ambazo amezifanyia *budget*, ambazo zinatofautiana kabisa na zile za Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa vya SMZ *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, nikiri kidogo kuna kosa, lakini wale wazee hawakusahauliwa na kifungu kile kimeondolewa katika Fungu 12000 na limepelekwa kwenye Fungu 4000 sehemu ya Maposho Mengineyo. Kwa hivyo, kifungu hicho kipo na wala hakikutolewa, isipokuwa ni bahati mbaya labda ni *printing mistake* tu.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nimeliona hilo jibu la Mhe. Waziri. Lakini jibu lake ni kwamba maposho ya Wazee yamepungua kutoka shilingi 103,000,000/- mwaka jana na sasa wazee wamepunguziwa hadi shilingi 69,000,000/-. Kwa kweli tulitegemea kutokana na hali ya ukali wa maisha vijisenti hivyo wanavyopewa vipande, lakini vimeteremka kwa asilimia kubwa sana. Hivi wizara au serikali kwa jumla iko makini na suala hili?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, wazee wengine huwa wanafariki.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, tuendelee *(Kicheko/Makofi)*.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 05 | - | Wilaya ya Wete | 214,000,000/- |
| Kifungu 06 | - | Wilaya ya Micheweni | 180,000,000/- |
| Kifungu 07 | - | Wilaya Ndogo Kojani | 28,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **834,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 43 - AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO**

Kifungu 02 - Utawala Unguja

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika Kambi yetu huku hakuna hata mjumbe mmoja ambaye hakuzungumzia suala hili, kwa sababu sisi ndio tunaojua idadi kubwa ya wananchi wetu wa Wazanzibari wenzetu ambao wamekosa Kadi za Utambulisho.

Kwa hivyo, nilishauri kama ifuatavyo, nilisema kwa kuwa hivi sasa suala hili la vitambulisho limechukua sura ya kisiasa kutokana na uchuaguzi. Kwa maana hiyo, baada ya uchaguzi kumalizika Wazanzibari wote wenye haki ya kupewa basi wapewe.

Mhe. Waziri hakunijibu hili, maana sisi tunaona uchungu kuona wenzetu hawana Kadi za Utambulisho, kwa sababu wanapata tabu watu kwenye huduma mbali mbali. Kwa hiyo, naomba maelezo, je anakubaliana na ushauri wangu baada ya uchaguzi Wazanzibari wote wapewe Kadi za Utambulisho.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe vile vile nakubaliana na maelezo aliyoyatoa Mkurugenzi wa Vitambulisho, kwamba wakati wowote mtu anapotimiza zile sifa au sheria, basi atengenezewe kitambulisho chake.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, sikumfahamu vizuri.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, amesema kwamba mtu anapotimiza masharti au sifa zilizowekwa, basi watatengenezewa vitambulisho vyao *(Makofi)*.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa wapo Wazanzibari ambao wametimiza masharti yote ya kisheri pamoja na katiba, lakini hawapewi. Kwa hivyo, hawapewi kwa sababu ya huu uchaguzi, je utakapomaliza uchaguzi watapewa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, hivyo itakuwa kama tunaipinda sheria nikisema baada ya uchaguzi ndio watengenezewe vitambulisho, wakati Sheria ya Vitambulisho haisemi hivyo *(Makofi)*.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyeikiti, tuendelee.

Kifungu 02 - Utawala Unguja

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nilidhani umeniona wakati ulipompa nafasi Mhe. Haji Faki Shaali na baadaye ndio unirudie mimi, lakini kumbe umetegemea nisimame tena.

Wakati nilipokuwa nikichangia hoja hii ya vitambulisho kuna mambo mawili ambayo yanahusiana na fedha niliyazungumza. Kwanza katika kitabu kikubwa ukurasa wa 501 kwenye kifungu kidogo 23.000 chenye *Heading* ya Takrima (*Hospitality*).

Hapa nilihoji kwa nini kuna ongezeko kubwa la fedha kutoka shilingi 32,000,000/- mwaka jana na kwenda shilingi 222,000,000/- mwaka huu, ambazo ziko chini ya maelezo Matumizi kwa Kazi zisizotazamiwa na hizi hazipatikani popote isipokuwa kwenye idara hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi alitoa maelezo ambayo sikuridhika nayo. Kwa hivyo, nahoji kama ni fedha ambazo zina kazi yake, kwa nini tuzifiche, nadhani ni vyema tukazipa jina lake, ili mkaguzi naye aweze kuziona na hapa si pahala pale na wala sikubaliani kabisa na hili *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nilihoji kwenye fungu hili ni juu ya ongezeko kubwa la bajeti kwa mwaka huu kutoka shilingi 371,000,000/- mpaka

shilingi 910,000,000/-. Nikiangalia kitabu ambacho tumeletewa hapa malengo ya utekelezaji wa kazi ambazo zimepangwa hazina tofauti kabisa na kazi ambazo zilifanywa kwa mwaka 2009/2010. Je, ni kitu gani kilichosababisha ongezeko hili?

Wakati maelezo ambayo Mhe. Waziri ametoa yanahusiana na juu ya uendelezaji wa Mradi wa Vitambulisho. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana katika Fungu la Maendeleo idara hii imepewa shilingi 800,000,000/- na zimetolewa zote kama tulivyoarifiwa kwa asilimia mia moja. Kwa hivyo, mwaka huu upo *allocation* nyengine ya shilingi 800,000,000/-. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo zaidi kuhusiana na hizi shilingi 222,000,000/- *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza upungufu wa fedha isiwe sababu, kwani wakati wowote inategemea na hali ya mtiririko mzima wa uchumi katika nchi pamoja na suala la matumizi ya fedha kuongezeka, yaani kushuka na kupanda. Hata hivyo, hali aliyoielezea nakubaliana naye kwamba tutakaa pamoja na kuweza kupitia, ili tuone matatizo na tuwe kuyatatua *(Makofi)*.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti, maelezo ambayo nataka bado sijayapata. Kwa hivyo, ninachokiona hapa ni kwamba tunayo mafungu katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambayo ni muhimu na wala hayana fedha. Kwa mfano, hivi sasa yalikuwa yakielezwa matatizo mengine, lakini tume-*allocate* fedha ambazo hatuzijui matumizi yake. Kwa kweli bado nahitaji maelezo kuhusiana na fedha hizi *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kusema kwamba kuna ya kukaa na kuangalia hali iko vipi kutokana na maelezo aliyosema Mhe. Mjumbe, yaani imenifanya na mimi nivutiwe kwa kukaa pamoja, kwa ajili ya kuweza kuifanyiakazi *(Kicheko/Makofi)*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, anataka mkae pamoja kwa ajili ya kuyaangalia.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kukaa pamoja hivi sasa na kuweza kulisawazisha hili kabla ya kuipitisha hii bajeti, bila ya hivyo tukipitisha hizi fedha maana yake tunaruhusu matumizi ya shilingi 222,000,000/- kwa maelezo ambayo hatuna sisi hapa kama watumishi wa wananchi. Kwa kweli hilo sitaliruhusu (*(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho nilimueleza kwamba

kuna suala la takrima, kwa kweli linahitaji lifanyiwe utafiti takrima ndio nini kabla hatujatumia kusema kwamba kitu hiki ni nini au gani. Sasa baada ya kupata uchambuzi wa kisheria suala la takrima na ulipaji wake, hapo ndipo tunaweza kusema litakwenda vipi. Lakini mpaka hivi sasa hatujui takrima ni kitu gani.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri kuna maelezo ya ziada kwa upande wa serikali, kwa sababu hapa tunazungumzia kifungu kinachosema Matumizi kwa Kazi Zisizotazamiwa (*General Expenditures*).

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, mambo hayo yanakuwa yanatokezea wakati wa kufanya mahesabu unaweka asilimia fulani *incase* kutokana matumizi haya pamoja na ukuaji wa uchumi, fedha kuanguka au kupanda. Kwa hivyo, unaweza kuziweka katika hali hiyo au kwenye *General Expenses*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, maelezo ya ziada tunaweza kuyapata kutoka upande wa serikali.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hata mimi nilipokuwa nikimjibu Mhe. Mjumbe kuhusu *point* hii, kwamba huu mradi bado unatanuka na tunatarajia kazi za *consultancy*, ambapo hiyo ni mikataba midogo midogo, yaani *is not fixed* mshahara wake hatuujui na yale ni maposho tu.

Vile vile tumesema kuna malighafi vile vitambulisho bado tunavi-*print* na tunayo mipango ya kuviboresha zaidi. Kwa hivyo, hizi ni kama aliyosema Mhe. Waziri kwamba matumizi usiyoyatarajia. Sasa aliuliza ukitimia tukakuya kufanya masuala ya *audit*. Kwa kweli hesabu zote zipo wazi na Mhe. Mjumbe pamoja na Kamati yako utakaribishwa kwenda kukagua. Lakini hizi zimewekwa kama alivyosema Mhe. Waziri kwamba hatutarajii.

**Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji:** Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya Mhe. Waziri, kwa sababu shughuli zote za Maendeleo ya Vitambulisho kuna fedha tayari zimeshatengewa katika Fungu la Maendeleo shilingi 800,000,000/- na mwaka jana tumetoa shilingi 800,000,000/- na imepatikana yote. Kwa hivyo, safari hii katika ukurasa wa 560 ipo *allocation* ya shilingi 800,000,000/- *(Makofi)*.

Kwa kweli suala hili lazima lishughulikiwe haraka tulishughulikie hapa na wala haiwezekani kwamba una shughuli tu unazikisia labda zinaweza kutokea na kuweka shilingi 222,000,000/- ambazo ni *too much*. Nadhani ningeelewa kidogo kama ningeambiwa mwaka jana zimewekwa shilingi 32,000,000/- na

mwaka huu tumeweka 64,000,000/-, yaani mara mbili yake. Lakini shilingi 222,000,000/- katika hali ya matatizo ya fedha tuliyonayo. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani *(Makofi)*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa tumefika pahala lazima tupitishe uamuzi. Kwa sababu tumejadili kwa hoja tatu, inabidi tuhoji watu wanaokubaliana na matumizi haya na wasiokubaliana na matumizi ya kifungu hiki.

Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na kifungu hiki kwamba fedha hizi ziingizwe kwenye kifungu kama ilivyooneshwa hapa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Kifungu 03 - Afisi Kuu Pemba

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, narudi tena kwenye vitambulisho na nilinyanyuka zamani, lakini kwa bahati mbaya sikupata nafasi. Wakati nilipokuwa nikichangia mada hii nilimuomba Mhe. Waziri baada ya kutoa vielelezo vyote kwamba wapo watu wenye haki ya kupata vitambulisho, lakini hawakupa kwa sababu ya shindikizo la sheha mpaka ninatumia neno "*there is no rule without exception*", ili hawa watu wapate haki yao.

Kwa taarifa hivi juzi tayari limeshapita Daftari la Jamhuri ya Muungano, katika jimbo langu wapo wapiga kura 1191 Wazanzibari waliokwenda *ZEC* na wakakoseshwa vitambulisho, wengine ijapokuwa wameshawahi kupiga kura zamani pamoja na watu wengine hawakupata kuandikishwa lakini kule wameandikishwa. Kwa hivyo, ikifika siku ya uchaguzi kwa kuwa ni siku moja *case* yao itakapokuja kwa wananchi kumbe *NEC* inajali zaidi watu wake kuliko *ZEC*.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako kuhusu kifungu kilichopigiwa kura kinaweza kujadiliwa naomba Katibu atusaidie.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, kifungu kile tumeshapita tuko kwenye kifungu chengine cha 03 Afisi Kuu Pemba. Tunaendelea *(Makofi)*.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi nimefahamika. Wananchi wa Zanzibar ambao walikuwa na haki ya kuandikishwa kupiga kura katika Uchaguzi huu wa *ZEC*, ambao walikoseshwa kwa sababu ya sheha tu

kutoa ruhusa kwamba wapatiwe Vitambulisho vyao vya Uzanzibari Ukaazi. Vile vile na wale ambao wameshawahi kupiga kura mara nyingi lakini safari hii hawakuingizwa kwenye daftari, kwa sababu hapo walipoandikishwa hawakuna na Vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema suala hili tusilichukue kwamba sheha ndiye mwenye uamuzi wa mwisho. Jambo la msingi tufanye vyovyote kwa sababu Mhe. Waziri yupo tuone kuwa hawa wakati ni haki yao, basi wapewe sasa kama kuna utaratibu mwengine wowote uendelee baadaye. Lakini Mhe. Waziri hakutoa jibu.

Kwa hivyo, nasema tutajihisi vipi baina ya *ZEC* na *NEC* siku ile ya kupiga kura, yaani ikawa *NEC* wametujali zaidi kuliko *ZEC* katika suala hili la haki ya raia.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, asiwe na wasi wasi Mhe. Mjumbe ushindi atapata jimboni kwake.

Lakini nasema kwamba Sheria za Vitambulisho ziwezi nikaziingilia kubadilisha kinyume na vile sheria inavyosema ndicho kitu ambacho kigumu. Hata hivyo, suala ambalo amelizungumza nakubaliana nalo, kwa hiyo ni vyema kukaa na kuliangalia na pia tukiliona linakwenda vizuri, basi tunaweza kulitengezea sheri na kulileta hapa na kuweza kufanya marekebisho kuhususiana na vitambulisho kwa yale makosa tuliyoyaona, ambayo yanaleta matatizo kwa wapiga kura au wananchi wetu kutokana na kukosa vitambulisho.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa taarifa tu kwamba ninaposimama hapa huwa ninasimama kwa wote si kwa CUF wala CCM, kwani ni mwakilishi wa wananchi wote. Vile vile nashukuru kwa busara zake Mwenyezi Mungu amjaalie tutekeleze na vitambulisho vitoke kabla ya uchaguzi. Ahsante tuendelee *(Makofi)*.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 03 | - | Afisi Kuu Pemba | 158,000,000 |
| | | **Jumla ya Fungu** | **910,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 09 - AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA SMZ**

Kifungu 06 - Tawala za Mikoa na Serikali za Miji

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasubiri hapa kwa hamu kubwa sana na hapa tumefika.

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bado Baraza halijamaliza shughuli za kamati, kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kutoa hoja kwamba Baraza liendelee na shughuli za kamati hadi hapo zitakapomalizika. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tuko ukurasa wa 526. Wakati nilipokuwa nikichangia kuna mradi hapa ambao sina uhakika nao sijui ndio katika *reform* zinazozungumzwa au vipi katika bustani hii ya Jamhuri. Nikataka maelezo nikauliza je, mradi huu kakabidhiwa nani maana yake tunaona mabadiliko makubwa. Lakini Mhe. Waziri kwa bahati mbaya hili hakulijibu kwa hivyo naomba maelezo. Kama ndio reform zenyewe hizi zimeshaanza kutangulia au ni jambo gani hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, uimarishaji wa Serikali za Mitaa. Nafikiri nilitoa maelezo kuhusu mabadiliko yatakayofanywa ni kutokana na uimarishaji wa Serikali za Mitaa. Maandalizi tunaanzia.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hajanifahamu. Wakati nilipokuwa nikichangia hotuba ya Mhe. Waziri nilitaka maelezo kuhusu *Jamhuri Garden*, kwa sababu tunaona hivi sasa imebadilika. Sasa tunajiuliza je amepewa mtu mwekezaji au kuna ubia na kampuni ama shirika lolote au ni kitu gani, yaani tunataka tupate maelezo na katika hiyo *reform* ambayo umeeleza, hii ndio katika hiyo *reform* au ni mradi mpya na nani mwenye kuushugulikia.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, huu ni mradi mpya ambao unaoshughulikiwa na Manispaa.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, hakuna ubia na watu kutoka nje kwa sababu mara moja tulipita na kuona wageni wengine. Sasa tunataka kuwa wawazi kabisa hivi kweli Manispaa haina ubia na mtu au kampuni yoyote.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuwepo kwa wageni sio maana kwamba ule mradi ni wageni. Kwa mfano, hivi sasa ukikaa *Forodhani Parck* unaweza kuambiwa na wewe ni mbia. Kwa hivyo, huu ni mradi mpya unaoshughulikiwa na Manispaa *(Kicheko/Makofi)*.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika na maelezo ya Mhe. Waziri, lakini tuendelee.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Mwenyekiti, kwenye kifungu cha mipango na sera niliuliza kuhusu marekebisho ya Serikali za Mitaa. Mhe. Waziri alisema hakuitaja hii kwa sababu itakuwa kwenye bajeti ijayo. Lakini kwenye kifungu hiki naona imetenga shilingi 250,000,000/- kwa ajili ya Serikali za Mitaa. Kwa hivyo, lile swali langu linarudi tena, kwa kuwa Serikali za Mitaa zimetengewa fedha kazi hii itakamilika lini?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunakwenda nayo na lini hasa itakamilika sijui *(Makofi)*.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Waziri hana jibu, basi tuendelee.

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Wakati Mhe. Waziri akijibu hoja za Mhe. Haji Faki Shaali amejibu kwamba *Jamhuri Garden* ni mradi mpya wa Manispaa. Lakini kuna taarifa nyengine ambazo sisi tumezipata, sasa sijui ukweli wake ni upi. Kwa kuwa kuna mama mmoja ambaye ametajwa ndiye mmiliki wa shughuli hiyo iliopo hapa.

Je, taarifa aliyotoa Mhe. Waziri na hii iliopo, ipi yenye ukweli na kama tushikilie hii anayosema yeye na baadaye utafiti ukionesha kwamba sio Manispaa moja kwa moja upo na mkono wa mtu, basi Mhe. Waziri atatueleza nini na hatokuwa amelidanganya Baraza hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni mradi mpya wa Manispaa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tuchukue kwamba ni mradi wa Manispaa ambayo ni kauli ya Mhe. Waziri ndani ya Baraza.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 06 | Tawala za Mikoa na Serikali za Mijini | 250,000,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **250,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | Utawala Unguja | 650,000,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **650,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 29 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala | 250,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **250,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 34 – KIKOSI CHA VALANTIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 100,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **100,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 38 – MKOA WA KUSINI UNGUJA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 04 | - | Mipango na Sera | 60,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **60,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 39 – MKOA WA KASKAZINI UNGUJA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 04 | - | Mipango na Sera | 150,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **150,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila*

*ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 40 – MKOA WA KUSINI PEMBA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 04 | - | Mipango na Sera | 60,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **60,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 41 – MKOA WA KASKAZINI PEMBA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 04 | - | Mipango na Sera | 40,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **40,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 43 – AFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 800,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **800,000,000/-** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Abass Juma Muhunzi:** Mhe. Mwenyekiti, utaratibu. Sikuisikia *total* sikuisikia. budget ya wizara hii ambayo tunataka tuikubali, sijui kama imetajwa

**Katibu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba utaratibu tunaoutumia ni kusoma fungu moja moja na mafungu yote ya wizara hii tayari tumeshayapitisha *(Makofi)*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimia Wajumbe, huo ndio utaratibu ambao umezoeleka ndani ya Baraza hili. Kwa hivyo, sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi).*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, nataka niwashukuru sana kama leo kungekuwa kuna shughuli basi ningesema nimetolewa kiukumbi kwenye Baraza hili. Lakini naamini nimehitimu *(Makofi).*

*(Saa 7:04 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa. 11.00 Jioni Baraza lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 - Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi (Afisi ya Rais) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehma kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena leo hii kuendelea na shughuli zetu muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima, busara na atuongoze vyema ili tuweze kufanikisha majukumu yetu vizuri.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea kutoamaelezo kunamasahihisho ambayo yamefanywa katika hotuba yanagu ambayo nadhani yamechapishwa, wajumbe wote waote watagaiwa ni kwamba katika pesa za *DPP* tulipewa milioni mia tano, lakini kumbe za miaka miwili kwa hivyo itabidi tutumie mia mbili na hamsini mwaka huu na miambili na hamsini milioni tutumie kwa mwaka ujao, kwa hivyo hayo masahihisho mtayaona na kila palipofanyiwa masahihisho mtapaona.

**Mhe. Spika:** Kuna karatasi kama hii ndio hiyo ambayo Mhe. Waziri anaizungumza, kwa hivyo tuhakikishe kwamba kila mjumbe ameipata hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora :**Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume kwa juhudi zake za kuimarisha ustawi wa maisha kwa wananchi. Aidha, nampongeza kwa juhudi zake za makusudi anazochukuwa za kulinda amani, kudumisha utulivu na maelewano miongoni mwa wananchi kama anavyoongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Waziri Kiongozi, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kusimamia vyema utekelezaji wa siku hadi siku wa shughuli za serikali. Aidha, busara zake katika kusimamia shughuli za Baraza hasa pale hoja na maamuzi mazito kwa mustakabali wa nchi yetu zinapojitikeza, hatuna budi kuzipongeza. Juhudi zake hizo zimelijengea heshima kubwa Baraza letu hili pamoja na serikali yetu kwa ujumla ndani na nje ya nchi. Vile vile napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliendesha vyema Baraza letu hili tukufu kwa misingi ya uwazi na demokrasia ya hali ya juu.

Mhe. Spika, naomba kutumia nafasi hii vile vile kuwapongeza wajumbe wako wote na kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa namna walivyoichangia hotuba ya wizara yangu katika mwaka wa fedha 2009/2010. Pongezi za pekee nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haji Omar Kheri kwa ushauri, maelekezo na busara zao wanazozitoa. Naomba nikiri kwamba michango yao imeisaidia sana wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake.

## HALI YA UTAWALA BORA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2000-2010

Mhe. Spika, wakati tunaelekea ukingoni mwa kipindi cha pili na cha mwisho cha awamu ya sita ya serikali yetu, ni vyema tukatafakari kwa muhtasari hatua zilizofikiwa na changamoto zilizojitokeza katika uimarishaji utawala bora. Ingawa hakuna utafiti rasmi uliofanywa kutathmini hali halisi kwa kipindi hiki, lakini bado hili halitunyimi nafasi ya kujielewa wapi tunakotoka, wapi tulipo na wapi tunakoelekea kwa kadiri dhana ya utawala bora inavyohusika hapa Zanzibar. Ripoti, makala na taarifa mbali mbali zimekuwa zikitambua hatua kadhaa zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa katika kuimarisha utawala bora.

Mhe. Spika, kila enzi ina mambo yake. Nasema hivi nikimaanisha kuwepo kwa mambo makubwa ambayo kila awamu ya serikali yetu ilitilia mkazo katika kuendesha nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kazi kubwa ya kutafuta, kulinda uhuru wetu na kuwaunganisha wananchi ilifanywa na awamu ya kwanza, na ile ya pili ikaanza kutandika misingi ya demokrasia kwa kuanzisha Baraza la Wawakilishi. Awamu ya tatu, kwa upande wake, ilijikita katika kuinua uchumi kwa kuanzisha biashara ya soko huria. Awamu ya nne

ikaendeleza mageuzi ya kiuchumi na awamu ya tano ilikuja na changamoto ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Mhe. Spika, awamu ya sita licha ya kuweka mkazo maalum katika kuimarisha miundombinu, pia ndio iliyokuja na dhana nzima ya uimarishaji wa utawala bora. Utekelezaji wa dhana hii ni chachu muhimu katika kuyatekeleza yale yote yaliyoanzishwa katika kila awamu iliyopita kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa kutambua umuhimu huo, katika awamu hii ya sita chini ya uongozi wa Mhe. Dr. Amani Abeid Karume kumeanzishwa rasmi wizara iliyopewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa misingi ya utawala bora. Kuundwa kwa wizara hii kumekuja sambamba na mageuzi kadhaa yaliyolenga kuharakisha ustawi wa maendeleo yetu yakiwemo mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kama inavyoelezwa katika mikakati yetu ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, kwa kutekeleza na kusimamia misingi ya utawala bora nchini, wizara imekuwa ikitekeleza Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000/2010 kama ilivyoelezwa katika Sura ya tano na Ilani za Uchaguzi za mwaka 2000 Sura ya tano na ile ya mwaka 2005 Sura ya saba ibara ya 99. Hivyo basi tukiwa tunakamilisha awamu ya sita ya uongozi wa serikali yetu naona fahari, japo kwa muhtasari, kuyataja mafanikio yaliyopatikana katika ujenzi wa utawala bora kwa kipindi hiki cha miaka kumi.

**Utawala bora katika siasa na demokrasia *(political and democratic governance)***

i. Kuimarika kwa demokrasia na umoja wa kitaifa: Marekebisho ya 8 na ya 9 ya Katiba ya mwaka 2002 yamepanua demokrasia kwa kuweka utaratibu ulio bora wa kuwashirikisha wananchi katika kufanya maamuzi. Juhudi za kujenga umoja na mshikamano zimeonesha kuwepo kwa dhamira ya kweli ya viongozi wetu wakuu wa kisiasa katika kujenga mustakabali wa wananchi wa Zanzibar na hivyo kuleta matumaini ya kuwa na jamii yenye utulivu na amani;

ii. Kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi na ile ya Mahakama kumeimarisha uhuru na utendaji kazi wa mihimili hii ya dola;

iii. Kuimarika kwa uhusiano wa kidiplomasia na jumuiya za kimataifa ni chachu katika harakati za kuimarisha ustawi wa Zanzibar na watu wake;

iv. Mafanikio katika sekta ya sheria yanahusisha kuanzishwa na kufanyakazi kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambako kumesaidia kuimarisha imani ya wananchi juu ya upatikanaji wa haki katika vyombo vya sheria. Kubwa la kujivunia ni kupungua kwa kesi za jinai zisizo za lazima kutokana na utaratibu wa kukamilisha upelelezi kabla ya kupeleka kesi mahakamani. Elimu ya sheria imeimarika Zanzibar na lile

tatizo sugu la uhaba wa wanasheria na mahakimu halipo tena sasa kutokana na kuwepo kwa vyuo vikuu vinavyotoa wanataaluma wa sheria; na

v. Mapitio na hatimaye kurekebishwa kwa sheria za kazi mwaka 2005. Marekebisho haya yameweka misingi ya uajiri, mahusiano kazini na usalama sehemu za kazi kwa taasisi za serikali na zile binafsi. Mambo haya yamefanyika kwa kuzingatia Azimio la Shirika la Kazi Ulimwenguni *(ILO)* kuhusu haki za msingi kazini.

**Utawala bora katika biashara *(corporate governance)***

i. Jitihada za ujenzi wa utawala bora katika biashara zimepata msukumo mkubwa katika kipindi hiki. Kuanzishwa kwa Baraza la Biashara (Zanzibar Business Council) ni hatua ya kujivunia ambapo wadau kutoka serikalini na taasisi binafsi hulitumia jukwaa hili chini ya uenyekiti wa Rais wa Zanzibar kujadili mambo muhimu ya kustawisha biashara. Udhibiti wa Bidhaa za vyakula kupitia Bodi ya Chakula na Madawa nao sasa unampa matumaini mlaji juu ya usalama wa afya yake; na

ii. Kuimarishwa na kurahisishwa kwa mazingira ya biashara ikiwemo uwekezaji kupitia sheria mbali mbali kunatoa nafasi ya kukua kwa sekta hii.

**Utawala bora katika usimamizi wa fedha na uchumi *(financial and economic governance)***

Mhe. Spika, hatua kadhaa zimechukuliwa katika kipindi hiki kwa lengo la kudhibiti matumizi ya mali na fedha za umma ikiwa ni mojawapo ya mihimili ya utawala bora. Kuundwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama taasisi inayojitegemea chini ya sheria Nam. 11 ya mwaka 2003 kumeongeza uwezo wa kudhibiti matumizi ya fedha na mali za umma. Kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2005 na ile ya Manunuzi Serikalini Nam. 9 ya mwaka 2005 ni hatua muhimu katika kudhibiti fedha na mali za serikali. Aidha, mifumo ya kisasa ya kusimamia shughuli za fedha ikiwemo ya *IFMS, ZBAS, MTEF* n.k. imesaidia sana katika usimamizi huo.

**Utawala bora katika kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kijamii *(socio-economic governance)***

Mhe. Spika, hatua kadhaa za kuimarisha uchumi wa nchi na kupunguza umasikini kwa wananchi wetu zimechukuliwa ambapo mafanikio makubwa yamepatikana yakiwemo:

i. Maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara Unguja na Pemba na ukarabati wa uwanja wa ndege, ujenzi wa bandari mpya ya Malindi, mradi mkubwa wa umeme kutoka gridi ya taifa hadi Pemba, kuimarika kwa huduma za afya, maji, na elimu ambapo kwa vipimo vya utekelezaji wa Malengo ya Milenia *(MDGs)* Zanzibar imepiga hatua. Kuanzishwa kwa mifuko ya wananchi wa kipato cha chini ukiwemo Mfuko wa Rais Jakaya Kikwete na Rais Karume, kumewasaidia sana wananchi wetu kujikwamua kiuchumi;

ii. Kutayarishwa kwa Programu ya Mageuzi katika Sekta ya Umma *(ZPSRP)* ni eneo muhimu linaloweka mustakabali mwema zaidi kwa watendaji na utendaji katika sekta hii muhimu; na

iii. Kupitishwa kwa sheria na sera mbali mbali zenye kuweka mazingira bora ya uwekezaji pamoja na kuwashajiisha wajasiriamali wadogo wadogo kujiajiri.

Mhe. Spika, baada ya kuyaeleza kwa muhtasari mafanikio katika maeneo hayo makuu manne ya utawala bora, naomba sasa nielezee kwa muhtasari mafanikio ya taasisi za wizara yangu kwa kipindi hiki cha miaka kumi kama ifuatavyo:

i. Ripoti za Ukaguzi zimetolewa kwa wakati, ambapo kwa kipindi cha 2007-2009 zinaonesha kuwepo kwa mafanikio makubwa ya kiutendaji na kupungua kwa matumizi mabaya ya fedha za umma;

ii. Sheria za msingi za jinai *(Penal Decree, Chapter 13)* na sheria ya nyendo za Jinai *(Criminal Procedure Decree, Chapter 14)* zimefanyiwa mapitio makubwa na kutayarisha Sheria mpya ya Jinai (Sheria Nam. 6) na Sheria ya nyendo za Jinai (Sheria Nam. 7), zote za mwaka 2004 ambazo zinatumika. Mbali na sheria hizo, kanuni mpya kadhaa za jinai nazo zilitungwa. Muongozo wa Uendeshaji Mashtaka umeandaliwa na nakala zake kugaiwa kwa Mahakimu, Wanasheria, na Jeshi la Polisi. Utaratibu wa kukamilisha kesi kabla ya kuzipeleka mahakamani umesaidia kupunguza muda wa kesi kuwepo mahakamani, kupunguza mahabusu na rushwa katika usimamizi wa jinai kutokana na kugawana kazi na hivyo kutoa fursa kwa taasisi moja kuiangalia nyengine;

iii. Kazi ya kuishauri serikali imefanywa vyema kupitia taasisi za wizara, ikiwemo Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambayo pia imechapisha seti 890 za Sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1980 hadi 2009 na kuzisambaza kwenye taasisi mbali mbali. Kwa kawaida seti moja inachukua ‘Volume’ 14;

iv. Kuundwa kwa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (Sheria Nam. 14 ya mwaka 2004) kumepelekea haki za wenye-hakimiliki na wabunifu kuanza kupatikana kwa watumiaji wa kazi hizo kibiashara kulipia matumizi kwa utaratibu wa leseni. Afisi imeandaa kanuni za utoaji leseni na ugawaji mirabaha kwa wenye-hakimiliki waliojisajili. Jumla ya kazi 527 za sanaa na ubunifu zimesajiliwa Unguja na Pemba;

v. Mahakama imeimarika kwa kuundwa Tume yake ya Utumishi. Aidha katika kipindi hiki cha miaka kumi kumekuwa na mafanikio makubwa ambapo uhaba wa Majaji na Mahakimu umepungua. Hali hii imepelekea kupungua kwa mrundikano mkubwa wa kesi katika Mahakama mbali mbali;

vi. Afisi ya Mufti wa Zanzibar imeundwa kisheria (Sheria Nam. 9 ya mwaka 2001). Afisi imekuwa na mafanikio makubwa katika kuwaongoza waumini wa kiislamu, yakiwemo mafanikio yanayohusu utoaji wa taarifa sahihi za kuandama kwa mwezi, jambo ambalo lilikuwa likileta utata mkubwa. Afisi imeendelea kujiimarisha kwa kujenga jengo la ofisi, imetoa mchango mkubwa katika vita dhidi ya UKIMWI kwa mbinu za kiislamu na kujenga umoja baina ya waumini wa kiislamu na wa dini nyengine;

vii. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imeimarishwa kiutendaji na kujijengea uwezo mkubwa wa kusimamia shughuli za Hijja na kusimamia mali za Wakfu na Amana na kufanya marekebisho ya Sheria Nam. 5 ya mwaka 1980 na kutunga sheria mpya (Sheria Nam. 2 ya 2007) ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwenye sheria ya zamani; na

viii. Kuimarisha utendaji wa Jumuiya za Kiraia kwa kuzihamasisha kujisajili ambapo baadhi yao zina mchango mkubwa kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera ya jumuiya zisizo za Kiserikali imeandaliwa kwa kutoa mwelekeo wa utendaji.

**CHANGAMOTO/MATATIZO**

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio ya jumla niliyokwisha kuyaeleza, bado utekelezaji wa misingi ya utawala bora umekuwa ukikabiliana na changamoto mbali mbali zikiwemo;

i. Upya wa dhana ya utawala bora ambao umesababisha kuwepo kwa ufahamu na matarajio tafauti ya dhana hii. Wananchi wengi na hata wanasiasa na viongozi wengine wa kijamiii walitarajia mabadiliko ya ghafla katika uendeshaji wa mambo yetu iwe ya kiserikali au ya kijamii. Hata hivyo ukweli unabaki kuwa kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora ni mchakato ambao mabadiliko yake yanakuja taratibu kutegemea na utayari wa kweli wa kila mdau;

ii. Uhaba wa nyenzo kwa taasisi katika kuendeleza utawala bora ni tatizo linaloathiri zaidi taasisi zetu zinazosimamia sheria na hivyo kuathiri upatikanaji wa haki. Aidha, kazi za kuratibu na kutathmini hali ya utawala bora nayo haijafikiwa katika kiwango kinachoridhisha;

iii. Tatizo la rushwa; na

iv. Utendaji na nidhamu katika sekta ya umma hauridhishi na hivyo kukosekana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma.

Mhe. Spika, baada ya kuyaeleza kwa muhtasari mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizopo katika ujenzi wa utawala bora, sasa naomba nianze kueleza hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya wizara kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, utekelezaji wa jumla wa kazi za wizara kwa mwaka 2009/2010 ulikwenda vizuri pamoja na kuzorota kwa shughuli nyingi za kiuchumi na za kijamiii kulikosababishwa na kukosekana kwa nishati ya umeme kwa kipindi cha miezi mitatu. Katika kukabiliana na hali hiyo, wizara ilichukuwa hatua ya kupitia upya mipango yake na kuanza kutekeleza kwa kuangalia kipaumbele kwa kila jukumu. Hivyo basi kwa kupitia taasisi zake wizara iliweza kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

i. Ukarabati wa jengo la Mahakama Vuga kwa kuweka paa jipya na ukarabati wa jengo lililokuwa Maktaba Kuu ili kwa kuanzia liweze kutumika kwa shughuli za Mahakama ya Biashara;

Kukamilika kwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2008/2009;

ii. Kupitishwa kwa sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka;

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali huko Pemba;

iv. Kuchapisha nakala za sheria za Zanzibar za mwaka 1980 hadi 2008 na kuzisambaza kwa watumiaji wakuu serikalini, taasisi za sheria, maktaba kuu, vyuo vya elimu na kwa wanasheria. Aidha, matangazo 25 ya sheria yalitayarishwa na miswada minane ya sheria iliandikwa na kuwasilishwa kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali;

v. Kazi ya kuimarisha mazingira ya biashara inayohusisha marekebisho ya sheria ya usajili wa biashara, usajili wa rehani na sheria ya ufilisi zimefikia hatua ya mwisho baada ya kukabidhiwa rasimu ya ripoti ya mwisho kwa mapitio; na

vi. Wizara imewasomesha wafanyakazi 69 ambapo kati yao 46 wamesomea elimu ya juu na 23 wamesomea Stashahada na Cheti.

## UPATIKANAJI WA FEDHA

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 wizara yangu iliidhinishiwa Sh. 5,123,000,000.00 ambapo hadi mwezi Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 3,619,616,893.00 sawa na asilimia 71. Kati ya hizo Sh. 1,886,188,119.00 sawa na asilimia 74 kwa mishahara na maposho na Sh. 1,733,428,774.00 sawa na asilimia 67 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, fedha zilizoidhinishwa ni Sh. 1,460,000,000.00. Hadi kufikia Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 1,040,000,000.00 sawa na asilimia 71 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa upande wa washirika wa maendeleo fedha zilizokadiriwa ni Sh. 2,482,381,000.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 1,963,546,033.00 sawa na asilimia 79 ya makadirio. Wizara pia inakusanya mapato kupitia Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Mahakama na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Makadirio yalikuwa ni Sh. 331,400,000.00 na hadi kufikia Machi, 2010 fedha zilizokusanywa Sh. 197,581,612.00 sawa na asilimia 59.62 ya makadirio. Matarajio ni kukusanya Sh. 260,661,600.00 ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni sawa na asilimia 78 (angalia viambatanisho Nam. 1, 2 & 3). Maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi za kawaida na malengo kupitia idara na taasisi za wizara kwa mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

## IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Spika, idara hii ni kiungo kinachounganisha taasisi za wizara na zile zilizo nje ya wizara. Jukumu kubwa la idara hii ni kuratibu utekelezaji shughuli za kila siku za idara na taasisi za wizara. Idara pia inahusika katika masuala yote ya kisera yanayohusu taasisi za wizara zinazojitegemea. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, Idara ya Mipango na Sera imetekeleza majukumu yafuatayo:

### Kuimarisha uwezo wa idara katika kuratibu kazi za wizara

Mhe. Spika, Idara ya Mipango na Sera imeendelea kuimarisha uwezo wa kuratibu shughuli zake ambapo katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010 imewapeleka wafanyakazi wawili masomoni katika Shahada ya Uzamili *(angalia kiambatisho namba 10b)*. Aidha, wafanyakazi wanne wamerejea kutoka mafunzoni baada ya kuhitimu mafunzo yao ambapo wawili wamehitimu katika kiwango cha Shahada ya Uzamili na wawili katika kiwango cha Stashahada. Idara pia imeendelea na utaratibu wake wa kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo na vitendea kazi. Mazingira ya kufanyia kazi yaliimarishwa hasa katika kipindi cha kukosekana kwa nishati ya umeme, kwa

kuhakikisha kuwa umeme wa dharura na maji yanapatikana kwa muda wote katika jengo la wizara.

Mhe. Spika, idara imeratibu utayarishaji wa taarifa mbali mbali zikiwemo za utekelezaji wa Miradi na Mipango ya Matumizi ya Muda wa Kati *(MTEF)* na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, idara imeratibu uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2005-2010 na Tathmini na Mwelekeo wa Sera 2010-2020. Vile vile idara imeratibu na kuandaa taarifa mbali mbali kwa ajili ya Kamati za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, idara imeshiriki katika mchakato wa kuufanyia mapitio Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini *(MKUZA)* na kushiriki katika vikao vya kamati ya ufundi ya *MKUZA* inayohusisha watendaji wa serikali na washirika wa maendeleo. Kamati hiyo inaratibiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Idara imeshiriki pia katika utayarishaji wa Ripoti ya Umasikini na Maendeleo ya Watu *(Zanzibar Poverty and Human Development Report*). Na kushiriki katika hatua mbali mbali za kuyarisha mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma

pamoja na utayarishaji wa Sera ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma. Ushiriki huu wa idara katika kazi hizi ni kutokana na nafasi iliyonayo wizara ya kuwa mwenyekiti wa klasta ya tatu ya *MKUZA* inayoshughulikia utawala bora.

Mhe. Spika, katika kukiimarisha kitengo chake cha habari, idara imeendelea kupokea nyaraka na machapisho mbali mbali na kuzihifadhi kwa ajili ya rejea. Aidha, nakala za nyaraka hizo pia zimesambazwa kwa taasisi nyengine za wizara.

Mhe. Spika, idara kupitia kitengo chake cha manunuzi imeratibu vikao vya Bodi ya Zabuni ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Machi vikao sita vimeratibiwa. Pamoja na mambo mengine, bodi imepitisha zabuni zenye thamani ya Sh. 1,168,781,000.00 kwa ajili ya mradi wa kuzihuwisha sheria zinazohusiana na usajili wa biashara.

**Kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI**

Mhe. Spika, katika kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI, idara kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI Zanzibar imetayarisha vipeperushi vinavyohusiana na Haki za Binaadamu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Lengo kuu ni kuutanabahisha umma juu ya kuzilinda na kuzijali haki za kibinaadamu. Aidha, idara imefanya utafiti mdogo kwa wafanyakazi wake wa kupima uelewa wa masuala ya UKIMWI na athari zake ambapo matokeo yameonyesha kuwa wafanyakazi wengi wanao uelewa wa kutosha juu ya masuala ya UKIMWI.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo, idara iliratibu kazi za kukamilisha ujenzi wa jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali lililopo Wete Pemba. Jengo hilo sasa limekamilika na limekwisha zinduliwa.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Idara ya Mipango na Sera iliidhinishiwa jumla ya Sh. 470,967,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 204,449,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 266,518,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 317,102,553.00. Kati ya hizo Sh. 154,827,295.00 sawa na asilimia 76 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 162,275,258.00 sawa na asilimia 61 kwa matumizi mengineyo (*angalia kiambatisho Nam. 1*).

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Idara ya Mipango na Sera itatekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa ripoti ya utekelezaji ya miaka kumi; na
ii. Kupitia upya mpango wa kimkakati wa wizara

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango na Sera iweze kutekeleza kazi zake kwa mwaka ujao wa fedha, 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 475,880,000.00 kwa kazi za kawaida.

**MAHAKAMA**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, jumla ya kesi 5,472 zilifunguliwa katika mahakama mbali mbali Unguja na Pemba, ambapo kesi 1,229 ni za madai na 4,055 ni za jinai. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 22.6 ukilinganisha na mwaka uliopita. Kati ya kesi 5,472 zilizofunguliwa, kesi 2,195, sawa na asilimia 40 zimetolewa uamuzi (*angalia viambatisho 6a & b*). Hadi kufikia Machi, 2010 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Kufanya matengenezo ya jengo la Mahakama Vuga**

Mhe. Spika, shughuli za matengenezo ya jengo la Mahakama Kuu Vuga zilianza rasmi katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Matengenezo hayo yalianza kwa kazi ya ujenzi wa paa na dari ambapo kwa sasa ujenzi wa paa tayari umemalizika na kazi ya kukarabati dari unaendelea. Kwa upande mwingine, jengo lililokuwa Maktaba Kuu limekabidhiwa kwa mahakama na kufanyiwa matengenezo kwa ajili ya kuanzisha Mahakama ya Biashara. Matengenezo hayo yako katika hatua za mwisho. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Mwera nao umemalizika na tayari jengo limeanza kutumika baada ya kupatiwa vitendea kazi. Vile vile, ujenzi wa Mahakama ya Mkoa Kusini Tunguu umeanza kwa hatua ya kujenga uzio na Mahakama ya Mkoani Pemba imefanyiwa matengenezo katika sehemu ya paa. Aidha, Mahakama imepata kiwanja Mkoani Pemba kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama mpya.

**Kuimarisha uwezo wa Mahakama**

Mhe. Spika, wafanyakazi 11 wa Mahakama wameanza masomo katika mwaka wa fedha 2009/2010. Kati ya wafanyakazi hao watatu wanasomea Shahada ya Uzamili ya Sheria *(Norway, Zanzibar na Morogoro)*. Wafanyakazi wawili wanasomea Shahada ya Sheria na Shahada ya Uongozi *(India na Malaysia)*. Wafanyakazi wawili wanasomea Stashahada katika fani za Sheria na Utumishi *(Dar es Salaam na Zanzibar)*, na wafanyakazi wanne wapo katika ngazi ya Cheti, ambapo watatu wanasomea kompyuta na mmoja uhasibu *(angalia kiambatisho namba 10b)*.

Mhe. Spika, Mahakimu wa ngazi mbali mbali walishiriki katika semina ya kuwajengea uwezo juu ya Sheria za Uvuvi. Semina hiyo ilitayarishwa na Idara ya Uvuvi Zanzibar kwa kushirikiana na Mahakama. Makarani wa Unguja na Pemba nao wameshiriki katika semina iliyotayarishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar ili kuwajengea uwezo juu ya shughuli zao za kila siku.

Mhe. Spika, Mahakama imepata vitendea kazi mbali mbali ambapo kwa sasa mahakama zote za mikoa zimepatiwa kompyuta ili kurahisisha utendaji wa kazi. Vile vile Mahakama ilipokea kompyuta moja kutoka Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* ili kusaidia kitengo cha Mahakama ya Kazi. Aidha, katika kukabiliana na suala la usafiri Mahakama Pemba imepatiwa basi moja kwa shughuli za kazi.

**Kuimarisha kamati ya kusukuma kesi**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 jumla ya vikao vitatu vimefanyika. Mafanikio yameanza kuonekana kwani hivi sasa karibu kesi zote za jinai zinazopelekwa mahakamani zinafunguliwa baada ya kukamilika upelelezi. Hatua hiyo imesaidia katika kupunguza gharama za utendaji wa shughuli za mahakama.

**Mpango wa wahalifu kutumikia jamii**

Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa Mpango wa Wahalifu Kutumikia Jamii tayari umefahamika na hukumu za kutumikia jamii zimeanza kutolewa katika mahakama mbali mbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010 jumla ya kesi 15 za Jinai washtakiwa wake walipewa adhabu za kutumikia jamii. Kati ya kesi hizo, 10 zilitolewa Unguja na tano Pemba. Aidha, Mahakama imefanya mikutano na Makamanda wa Jeshi la Polisi pamoja na Wakuu wa Vituo vya Polisi vya Mkoa Mjini Magharibi na Kusini Pemba, maeneo ambayo ndiyo yanayohusika na mpango huo kwa kuanzia. Katika mikutano hiyo kanuni na mwenendo mzima wa mpango huo ulifafanuliwa kwa wadau ili waufahamu vyema.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Mahakama iliidhinishiwa jumla ya Sh. 1,298,000,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 914,500,000.00 ni kwa

mishahara na maposho, na Sh. 383,500,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 955,527,053.00 ambapo Sh. 670,845,017.00 sawa na asilimia 73 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 284,682,036.00 sawa na asilimia 74 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Sh. 550,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo zote zinatoka serikalini. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni Sh. 275,000,000.00 sawa na asilimia 50. Fedha zilizokusanywa ni Sh. 34,061,942.00 sawa na asilimia 81 ya makadirio (*angalia viambatisho 1, 2 & 3)*.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Mahakama itaendelea kuimarisha uwezo wake, ikiwa ni pamoja na :-

i. Kuendelea na matengenezo ya Mahakama Kuu Vuga;
ii. Kufanya ukarabati wa majengo ya mahakama nne; na
iii. Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar.

Mhe. Spika, ili Mahakama iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka 2010/2011 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya shillingi 1,391,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 1,561,125,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 550,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 1,011,125,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo). Aidha, Mahakama katika mwaka 2010/2011 inakusudia kuchangia katika Hazina ya Serikali mapato ya Sh. 38,000,000.

## AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliweza kufanikisha kuwajengea uwezo wafanyakazi kitaaluma hasa wakiwemo wanawake, kutoa ushauri muafaka kwa serikali na hatimae kupungua kwa kiwango kikubwa cha kesi dhidi yake na kuchapisha sheria mbali mbali za Zanzibar. Aidha, ajira kwa wafanyakazi wanawake zimeongezwa na kufanikisha kupatikana kwa viwanja vya ujenzi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ilitekeleza malengo yafuatayo:

### Kuendelea kuchapisha sheria za Zanzibar pamoja na sheria ndogondogo

Mhe. Spika, kazi ya kuchapisha sheria za Zanzibar kutoka mwaka 1964 – 2009 pamoja na sheria ndogo ndogo *(Subsidiary Legislations)* za 1980 – 2008 iliendelea katika kipindi hiki. Afisi imekamilisha uchapishaji wa sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1980 hadi 2009 ambapo jumla ya *"Volume"* kumi na nne zimechapishwa. Sheria hizo tayari zimeshasambazwa kwa wadau. Sheria za mwaka 2010 bado zipo kwa mchapaji kwa hatua za mwisho. Aidha, sheria ndogondogo *(Subsidiary Legislations)* za 2009 – 2010 tayari zimekamilika na

zipo katika hatua ya kuzisambaza kwa wasimamizi husika. Kazi hii ya kuchapisha sheria ilikuwa imesita kwa takriban miaka 26 iliyopita lakini sasa tunaahidi kuiendeleza.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, jumla ya miswada minane iliandikwa na kuwasilishwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (*angalia kiambatisho Nam. 7a).*Kwa upande mwingine, jumla ya kesi 21 zinaendelea kusimamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa niaba ya serikali (*angalia kiambatisho namba 7b).*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, matangazo ya kisheria 25 yalitayarishwa na tayari yameshawasilishwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kati ya matangazo hayo, zipo sheria ndogondogo nne zifuatazo:-

i. Kanuni za Fedha za Mfuko wa Barabara Zanzibar, 2009

ii. Kanuni za Watumishi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar, 2009

iii. Kanuni za Mfuko wa Fedha za Mafunzo ya Amali, 2009

iv. Kanuni za Jeshi la Kujenga Uchumi

Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imewasomesha wafanyakazi wake wanne ambapo watatu wanasomea fani ya Uzamili wa Sheria *(LLM)* na mmoja anachukua Stashahada ya Utumishi *(angalia kiambatisho namba 10b)*. Afisi pia imetoa mafunzo mafupi kwa mfanyakazi mmoja yaliyohusu sheria za kimataifa, afya, jinsia, amani na usalama katika Afrika Mashariki. Aidha, vifaa vya afisi kama vile vespa moja, kompyuta tatu, vifaa vya kutendea kazi na vitabu mbali mbali vya sheria vimenunuliwa kwa ajili ya matumizi ya maktaba. Vile vile, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inatoa taarifa zake mbali mbali ili kuwasiliana na wadau kwa njia ya mtandao kupitia anuani yake ‘www.agc.go.tz’. Kwa upande mwingine, ujenzi wa uzio katika kiwanja cha Afisi ya Mwanasheria Mkuu kilichopo eneo la Mazizini Unguja unaendelea. Aidha, michoro ya majengo yatakayojengwa Unguja na Pemba tayari imekamilika.

**Kuimarisha Tume ya Kuchunguza Sheria**

Mhe. Spika, Tume ya Kuchunguza Sheria imewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili ngazi ya Shahada ya Uzamili ya Sheria. Aidha, wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Kwa upande wa vitendea kazi, Tume imenunua vespa moja, kompyuta moja na vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya Tume. Hata hivyo, miongoni mwa matatizo

yanayoikabili Tume hiyo, ni ukosefu wa Mwenyekiti na Makamishna ambao wangeweza kufanikisha shughuli za tume.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa jumla ya Sh. 546,000,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 146,731,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 399,269,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 328,266,000.00. Kati ya hizo Sh. 118,958,000.00 sawa na asilimia 81 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 209,308,000.00 sawa na asilimia 52 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Sh. 140,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo zote zilitoka serikalini. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni Sh. 90,000,000.00 sawa na asilimia 64 *(angalia viambatisho 1&2)*.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kutoa ushauri wa kisheria ulio makini kwa serikali, kutayarisha miswada mbali mbali kwa mujibu wa mahitaji na kuendelea kuiwakilisha serikali mahakamani. Aidha, itaendelea na jitihada za kuwawezesha wafanyakazi kitaaluma kwa ajili ya kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu na Kusimamia na kutetea haki za watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, watoto, wanawake, na watu wenye ulemavu. Afisi pia itaendelea kuimarisha Tume ya Kuchunguza Sheria na Kufanyia mapitio sheria za Zanzibar na kupendekeza marekebisho yanayostahiki kwa mujibu wa mahitaji.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kujenga majengo ya Afisi Unguja na Pemba; na

ii. Kuchapisha Sheria za Zanzibar.

Mhe. Spika, Ili kuiwezesha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 546,000,000.00 kwa kazi za kawaida na 1,718,899,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 250,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 1,468,899,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo).

**AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeanzishwa chini ya kifungu cha 56 A cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kufuatia marekebisho ya nane ya Katiba. Afisi ilianza kazi rasmi tarehe 10/7/2002 baada ya kuteuliwa Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwa ni dira ya kujenga utawala bora chini ya Awamu ya Sita ya Serikali. Afisi hii ina mamlaka ya kusimamia na kuendesha

kesi zote za Jinai katika mahakama yoyote Zanzibar isipokuwa Mahakama za Kijeshi.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefanikiwa kurekebisha mfumo wa uendeshaji wa mashtaka uliokuwa ukiendeshwa na Jeshi la Polisi na badala yake kuendeshwa kiraia kwa kuwatumia Wanasheria wa Serikali. Mfumo huo umepunguza idadi ya kesi zisizo za lazima, kupunguza muda wa kesi kuwepo mahakamani, mahabusu na kujenga misingi ya kitaalamu *(professionalism)* katika usimamizi wa kesi badala ya mazoea.

Mhe. Spika, chini ya utendaji wa afisi hii, zimetungwa Sheria mpya zifuatazo: (i) Sheria ya Kanuni za Adhabu Nam. 6/2004, (ii) Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7/2004, (iii) Sheria ya Fedha Haramu Nam 10/2009, pamoja na (iv) Sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nam. 2/2010. Aidha, Afisi imetayarisha kitabu cha Muongozo wa Uendeshaji Mashtaka na kuanzisha mkutano wa kila mwaka kwa wadau wote wa uendeshaji mashtaka.

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imejenga jengo jipya lenye maktaba ya kisasa ya sheria iliyopo Unguja na kuanzisha afisi ndogo Pemba. Aidha, imeweza kuajiri wanasheria 32 na makarani wa sheria wanne na kuwapatia mafunzo mbali mbali ya uendeshaji wa mashtaka ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Machi, 2010 wanasheria saba wamepata Shahada ya Uzamili nchini Uingereza, Norway, Sweden na New Zealand. Wanasheria wanaoendelea na masomo ya Shahada ya Uzamili ni watano na wafanyakazi katika kada nyengine wamepatiwa mafunzo katika ngazi mbali mbali *(angalia kiambatisho namba 10b).*

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi zake za kawaida kwa kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, Afisi ilifungua na kusimamia jumla ya kesi 812. Mahakama Kuu pekee iliyopo Vuga ilifungua kesi 68 na katika mahakama nyengine ni kama zinavyoonekana kwenye *kiambatisho namba 6c*. Aidha, Afisi imepokea majalada 260 kutoka Polisi kuhusiana na makosa mbali mbali yakiwemo ya taarifa za kifo 41, shambulio 7, wizi 33, ubakaji 10, kutorosha 3, kuua bila kukusudia 10, kuua kwa makusudi 10, madawa ya kulevya 61, kesi za usalama barabarani 74 na tuhuma ya kutenda kosa la jinai 1. Majalada hayo yamepatiwa ushauri kulingana na mahitaji husika. Aidha, Afisi imekuwa ikitoa ushauri wa aina mbali mbali kwa wananchi wanaofika ofisini.

Mhe. Spika, katika utoaji elimu kwa umma, Afisi iliandaa na kurusha hewani vipindi viwili (2) vya redio. Aidha, Afisi ilichapisha nakala elfu tano za jarida la *SHAHIDI*. Toleo la kwanza nakala 1,000; na toleo la pili na la tatu kila moja nakala 2,000. Jarida hili lilisambazwa kwenye wizara zote na idara zake, skuli, kwa wananchi, taasisi binafsi na jumuiya zisizo za kiserikali. Jarida hili hutolewa mara nne kwa mwaka. Vile vile skuli 10 zikiwemo za Unguja na

Pemba zimetembelewa kwa ajili ya kupatiwa elimu ya uraia. Masheha wa Mkoa wa Kaskazini Pemba walipatiwa mafunzo kuhusu kazi za Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na makosa ya jinai.

Mhe. Spika, Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo:

**Kuimarisha uwezo wa utendaji**

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa lengo hili, Afisi ilikamilisha na kuzindua jengo lake jipya la ghorofa moja ambalo lina maktaba ya kisasa na ofisi za wanasheria. Kwa upande mwengine tayari hatua za awali za ujenzi wa jengo la ofisi Pemba zimekamilika.

Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi saba na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wawili. Vile vile watendaji walipatiwa mafunzo ya Kompyuta, Utawala, Fedha Haramu, Sheria ya Mafuta na Gesi n.k, yaliyoendeshwa na wakufunzi wa ndani na nje. Mafunzo haya yanatekelezwa kupitia mkakati maalum wa kuendesha mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi kulingana na taaluma zao. Afisi pia imeajiri wafanyakazi wanane wakiwemo wanasheria saba na mkutubi mmoja. Wanasheria watano kati ya saba walioajiriwa tayari wamepatiwa mafunzo ya miezi mitatu Tanzania Bara.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imepata vifaa vya kisasa vitavyoiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Vifaa hivyo vimejumuisha, “sound system”, kompyuta, mashine ya fotokopi na vitabu vya sheria ambavyo vimetolewa msaada na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**Mpango wa pamoja wa usimamizi wa kesi za jinai**

Mhe. Spika, utekelezaji wa lengo hili ulijumuisha uandaaji wa Mfumo wa Pamoja wa Usimamizi wa Kesi za Jinai. Kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, mfumo huo umeandaliwa na kuwasilishwa kwa wafadhili kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, Afisi iliendelea na vikao vya mara kwa mara na wadau katika kuhakikisha usimamiaji bora wa kesi za jinai. Kwa kujua umuhimu wa usimamizi wa pamoja wa kesi za jinai, watendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wamefanya ziara mbali mbali katika ofisi za mikoa za Jeshi la Polisi katika kuimarisha mashirikiano na usimamizi bora wa kesi za jinai.

**Kuimarisha maktaba na kuanzisha kituo cha mafunzo na utafiti wa sheria**

Mhe. Spika, kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Afisi imepatiwa vifaa vya Maktaba vya kisasa pamoja na vitabu mbali mbali vya sheria. Maktaba hii inatoa huduma kwa wafanyakazi na wanasheria wa serikali

kutoka taasisi mbali mbali wakiwemo wanafunzi wa Sheria kwa utaratibu maalum. Taratibu za kuanzisha kituo cha mafunzo zinaendelea.

**Kukamilisha sheria ya kuanzishwa kwa Afisi na kurekebisha muundo wake kulingana na sheria mpya**

Mhe. Spika, napenda kulishukuru Baraza lako tukufu ambalo kwa kauli moja limeupitisha Mswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na hatimae Machi 10, 2010 Mswada huo umetiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa sasa Afisi inaendelea na kujenga Muundo wa Afisi kulingana na matakwa ya Sheria ya Uanzishwaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, pamoja na kutekeleza majukumu mengine yaliyoelezwa ndani ya Sheria hiyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa Sh. 653,000,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 272,000,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 381,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2010, fedha zilizopatikana ni Sh. 385,169,835.00. Kati ya hizo, Sh. 161,287,060.00 sawa na asilimia 59 zilipatikana kwa ajili ya mishahara na maposho na Sh. 223,882,775.00 sawa na asilimia 59 kwa matumizi mengineyo.

Aidha, Sh. 746,600,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo mchango wa serikali ni Sh. 300,000,000.00 na Sh. 446,600,000.00 zilitegemewa kutoka kwa wadau wa maendeleo. Shilingi 913,450,000.00 zilipatikana *(angalia viambatisho 1&2)*. Ongezeko hili lilikuja kutokana na kupata fedha za ziada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambazo zilibaki kutoka kwenye miradi ya taasisi nyingine zilizofadhiliwa na benki hii.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, mbali na jukumu kubwa la kuendelea kujiimarisha kiutendaji, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na mpango wa uendeshaji mashtaka kiraia katika mahakama nne za wilaya;

ii. Kuanza ujenzi wa Afisi Pemba; na

iii. Kukamilisha uanzishwaji wa kituo cha mafunzo na utafiti wa sheria.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 719,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 1,000,000,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 500,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 500,000,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo).

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni taasisi muhimu katika kuimarisha misingi ya utawala bora kama ilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Katika kipindi cha 2009/2010 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu No.112 (3) na kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Sheria namba 11 ya mwaka 2003. Jukumu kubwa la afisi hii ni kuzifanyia ukaguzi fedha zote zinazotolewa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, mapato ya serikali pamoja na matumizi ya fedha zinazotolewa na washirika mbali mbali wa maendeleo na kutoa taarifa zake za ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, ripoti ya ukaguzi wa hesabu ya mwaka 2008/2009 imekamilika. Aidha, ukaguzi wa hesabu za mwaka 2009/2010 unaendelea vizuri na ni matumaini yetu kwamba utakamilika kwa wakati uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo pamoja na fidia hadi kufikia Machi, 2010, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu imepokea majalada 789 ya wastaafu na wafanyakazi walioumia kazini. Majalada 764 yamekaguliwa kwa ajili ya malipo ya Wizara ya Fedha na Uchumi sawa na asilimia 97 na majalada 23 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, majalada 670 ya wastaafu yamepokelewa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Kati ya majalada hayo 664, sawa na asilimia 99 yamekaguliwa na sita yanaendelea kufanyiwa kazi kwa ajili ya malipo ya michango ya hifadhi ya jamii.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pia imewapatia mafunzo ya ukaguzi wa kisasa wafanyakazi wake 60 Unguja na Pemba, kwa kupitia wafadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Aidha, imejiimarisha kwa kuwapatia wafanyakazi watano mafunzo ya uongozi, kununua jengo na gari mbili, jenereta moja na kompyuta 30 na kazi za ujenzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huko Tibirinzi Pemba zimeanza. Kufanya ukaguzi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa kushirikiana ilitekeleza malengo iliyojiwekea kama ifuatavyo:-

### Kufanya ukaguzi katika taasisi za Serikali pamoja na miradi ya maendeleo

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeendelea kufanya ukaguzi katika taasisi zote za serikali, miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo pamoja na Halmashauri za Wilaya. Afisi imeweza kutimiza lengo lake kwa kukamilisha kazi za ukaguzi wa hesabu na matarajio

ni kuwa taarifa za ukaguzi huo zitatoka kwa wakati uliopangwa. Aidha, ushauri wa kitaalam umeendelea kutolewa kwa watendaji wa taasisi za serikali juu ya uwekaji wa kumbukumbu mbali mbali kwa kufuata sheria na taratibu za hesabu.

**Kuongeza uwezo wa watendaji, vitendea kazi na kuimarisha mazingira ya afisi**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, wafanyakazi tisa wamehitimu masomo katika fani zifuatazo: Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Biashara (1), Shahada ya Uhasibu (6) na Stashahada ya Ununuzi na Ugavi (2). Jumla ya wafanyakazi 17 wanaendelea na masomo, ambapo wafanyakazi watatu wanasomea Shahada ya Uzamili ya Uongozi wa Fedha, Stashahada ya Uzamili ya Uongozi wa Fedha (1), Shahada ya Kwanza ya Uongozi wa Biashara (5), Stashahada ya Juu ya Uhasibu (2), Stashahada (2), na wafanyakazi wanne (4) wanasomea ngazi ya Cheti *(angalia kiambatisho namba 10b)*.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imeendelea kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wake kwa kupitia miradi inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mpango wa Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma na Mradi wa Maendeleo ya Ukaguzi Zanzibar unaofadhiliwa na Afisi ya Ukaguzi ya Sweden kupitia Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia miradi hiyo zaidi ya wafanyakazi 60 Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo mbali mbali ya ukaguzi wa kisasa pamoja na mafunzo ya msingi ya matumizi ya kompyuta. Aidha, wafanyakazi watano wamepatiwa mafunzo ya uongozi.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu imenunua gari mbili kupitia Mpango wa Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha za Umma. Afisi imenunua jengo eneo la Maisara na tayari limeshaanza kufanyiwa ukarabati. Vile vile kazi za ujenzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huko Tibirinzi Pemba zimeanza. Afisi pia imenunua jenereta moja na laptop 30 zinazotumiwa na watendaji katika kazi za ukaguzi na utayarishaji wa ripoti. Vyote hivyo vimenunuliwa kupitia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Zanzibar imeendelea kuimarisha mashirikiano na afisi nyengine za ukaguzi duniani kama vile Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Tanzania na ya Sweden, pamoja na jumuia za ukaguzi za kimataifa na kikanda. Aidha, Afisi imeendelea kujenga uwezo na uhusiano mzuri na wadau wake mbali mbali ikiwemo Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali pamoja na taasisi nyengine za serikali.

**Kufanya ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa**

Mhe. Spika, katika mwaka 2009/2010, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu Zanzibar kwa kushirikiana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

Tanzania na Sweden, zimeweza kuweka mazingira mazuri ya kiutendaji ambayo yatapelekea shughuli za ukaguzi zifanyike kwa kuzingatia viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Kwa kulifanikisha hilo mambo yafuatayo yametekelezwa:

i. Kutayarishwa muongozo wa kazi za ukaguzi unaozingatia viwango vya kimataifa *(Regularity Audit Manual).* Muongozo huo utakuwa ndio dira ya kazi za ukaguzi kwa taasisi zote za serikali na miradi ya maendeleo; na

ii. Kuwaelimisha wafanyakazi Unguja na Pemba, juu ya taaluma mbali mbali zinazohitajika katika kufanikisha utumiaji wa muongozo huo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya Sh. 1,007,000,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 443,001,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 563,999,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, fedha zilizopatikana ni Sh. 852,121,042.00 sawa na asilimia 85. Kati ya hizo Sh. 368,091,042.00 sawa na asilimia 83 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 484,030,000.00 sawa na asilimia 86 kwa matumizi mengineyo. Sh. 1,067,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo mchango wa serikali ni Sh. 300,000,000.00 na Sh. 767,000,000.00 zilitegemewa kutoka kwa wadau wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2010, Sh. 300,000,000.00 zote zilipatikana kutoka serikalini. Kwa upande mwingine, Afisi ilikadiriwa kukusanya Sh. 4,000,000.00 ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2010, makusanyo halisi ni Sh. 2,500,000.00 sawa na asilimia 62.5 ya makadirio *(angalia viambatisho 1, 2 &3)*.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu itaendelea kuongeza uwezo wa watendaji, vitendea kazi na kuimarisha mazingira ya afisi. Aidha, Afisi itatekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha muongozo wa kazi za ukaguzi unaozingatia viwango vya kimataifa; na

ii. Kujenga ofisi za kisasa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Sh. 3, 620,000.00

Mhe. Spika, ili Afisi iweze kutekeleza malengo ya kazi zake kwa ufanisi katika mwaka ujao wa fedha, 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 1,147,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 1,129,771,000.00

kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 38,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 749,771,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo).

**AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR**

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar ni moja ya taasisi za wizara ambayo inajukumu kubwa la kutoa miongozo na kutatua migogoro mbali mbali ya kidini kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Afisi imeendelea kutekeleza shughuli zake za kawaida kwa kupokea migogoro mbali mbali na kuipatia ufumbuzi. Kwa kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, migogoro 18 imepokelewa ambapo 16 imepatiwa ufumbuzi na miwili inaendelea kushughulikiwa. Migogoro hii ilihusika zaidi na mizozo ya kifamilia, mizozo ya misikiti, mizozo ya madrasa n.k. Aidha, imepokea maswali 97 kutoka kwa waumini na wananchi ambapo maswali yote yalijibiwa.

Vile vile, Afisi imefanya mkutano mmoja wa kawaida na Baraza la Ulamaa. Kwa upande mwingine, jamii imeendelea kuelimishwa kwa kutumia hotuba za Ijumaa na ziara za Mufti Mkuu misikitini. Mada zilizotolewa ni pamoja na kuepuka migogoro isiyo ya lazima katika jamii yetu hasa katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu.

Mhe. Spika, katika kuendeleza mashirikiano na jumuiya za kidini za ndani na nje, Afisi imepokea Masheikh saba kutoka Misri, Iran na kituo cha Kiislamu cha Chang'ombe ambao walifanya mkutano na Masheikh mbali mbali wa Unguja. Aidha, imepokea Ujumbe kutoka *"World People Islamic Leadership"* wa Libya ambao ulifanya mkutano na wanawake wa Unguja sambamba na mkutano wa Mamufti Wakuu kutoka Nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Spika, Afisi ilishirikiana na Tarika ya Kadiriyya kufanikisha IJ-TIMAI iliyofanyika Pujini Pemba ambapo jumuiya ya "*World Islamic Call Society"* ya Libya ilitoa mchango mkubwa. Aidha, katika kujitangaza zaidi kimataifa, Afisi ya Mufti wa Zanzibar imealikwa na kuhudhuria mikutano ya kimataifa kama vile "*World Conference on Religion and Peace" (WCRP), "African Council Religion for Peace" (ACRP), n.k.*

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, Afisi ya Mufti imeendelea kuelimisha wafanyakazi wake wanne walioko masomoni ili kuwajengea uwezo ki-taaluma. Aidha, katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI kwa taratibu za Kiislamu, Afisi ya Mufti wa Zanzibar imefanya mafunzo kuhusu elimu ya UKIMWI kwa kufuata Muongozo wa Kiislamu kwa walimu sitini (60) wa madrasa za Wilaya za Kaskazini "B" na Magharibi Unguja. Vile vile Afisi imesaidia watoto yatima 581 wanaoishi katika mazingira magumu ambapo Wilaya ya Wete watoto 292 na Magharibi watoto 289. Misaada hii inajumuisha vyandarua, sare, na vifaa vyengine vya skuli.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya Sh. 136,466,000.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo Sh. 80,790,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 55,676,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi Machi, 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 100,838,809.00. Kati ya hizo Sh. 65,638,809.00 sawa na asilimia 81 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 35,200,000.00 sawa na asilimia 63 kwa matumizi mengineyo *(angalia kiambatisho Nam. 1)*.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Afisi ya Mufti itatekeleza lengo la Kutayarisha mpango mkakati wa Afisi ya Mufti

Mhe. Spika, ili Afisi ya Mufti iweze kutekeleza kazi zake kwa mwaka ujao wa fedha, 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 159,239,000.00 kwa kazi za kawaida.

## IDARA YA URATIBU UTAWALA BORA

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Utawala Bora inajukumu kubwa la kuratibu misingi ya utawala bora hapa Zanzibar. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010 idara imetekeleza kazi za kawaida na malengo iliyojipangia kama ifuatavyo:-

### Kuendeleza uelewa na utekelezaji wa utawala bora

Mhe. Spika, idara imeendelea na kazi ya kukuza uelewa wa wananchi juu ya utawala bora kwa kupitia elimu ya uraia. Jumla ya vipindi 32 vilitayarishwa na kurushwa hewani vikitoa mada mbali mbali za utawala bora. Aidha, idara katika kipindi hiki imeendelea kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora kwa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali.

Mhe. Spika, idara ilifanya semina zilizowashirikisha watendaji wa baadhi ya jumuiya zisizo za serikali na kwa maafisa wa vikosi mbali mbali vya ulinzi na usalama wa raia hapa Zanzibar. Katika semina hizo vitabu vya Muongozo wa Haki za Binadamu na Sera ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali, vilivyotayarishwa na idara kwa mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, vilisambazwa kwa wadau.

Mhe. Spika, idara imeendelea na kazi ya kusimamia utayarishaji wa Mkakati wa Elimu ya Uraia Zanzibar ambapo hatua iliopo hivi sasa ni kwamba rasimu ya mkakati huo imetayarishwa na wataalamu na kupitiwa na wanakamati. Taratibu zinafanyika kuiwasilisha katika ngazi za juu serikalini kwa kuridhiwa na kuanza utekelezaji wake.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata uelewa juu ya demokrasia na utawala bora, idara kwa kushirikiana na Taasisi ya Demokrasia Tanzania na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, imeweza kuratibu maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani. Katika utekelezaji wake,

programu mbali mbali zilizozungumzia masuala ya demokrasia ziliandaliwa zikiwemo semina, makongamano, tenzi na vipindi vya radio na televisheni kupitia vyombo vya habari vya serikali na kibinafsi.

Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, idara iliratibu sherehe za siku ya kimataifa ya Haki za Binadamu iliyofanyika tarehe 10 Disemba 2009. Mgeni rasmi alikua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na sherehe hizo zilifikia kilele kwa maandamano ya wananchi. Aidha, rasimu ya Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2008/2009 imeshawasilishwa wizarani.

Mhe. Spika, uimarikaji wa idara kiutendaji ni pamoja na kuwa na viashiria vya utawala bora hapa Zanzibar. Idara kwa kutumia wataalamu wake wa ndani imeanza kazi za kutayarisha viashiria hivyo ambapo vitasaidia kutathmini uimarishaji wa misingi ya utawala bora Zanzibar. Tayari idara imeweza kuandaa mkutano wa kazi wa siku tatu uliowajumuisha washirika na wadau mbali mbali wa utawala bora kujadili viashiria hivyo.

**Kuimarisha uwezo wa idara kiutendaji**

Mhe. Spika, idara imeendelea kuwahudumia wafanyakazi wake sita waliopo masomoni katika fani mbali mbali ikiwa ni utekelezaji wa lengo la kuimarisha idara kitaaluma. Wafanyakazi watatu wanaendelea na masomo ya Shahada ya Uzamili na wengine wawili wanaendelea na mafunzo ya vitendo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Aidha, mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania *(angalia kiambatisho namba 10b)*.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililieleza Baraza lako tukufu juu ya kukamilika kwa kazi ya mapitio ya mswada wa rushwa iliyofanywa na kikosi kazi kupitia msaada wa UNDP. Katika hili wizara yangu bado inaendelea na jitihada za kuona kwamba sheria ya rushwa inakamilika na kuwa moja ya nguzo kuu za kuimarisha Utawala Bora hapa nchini na ililipangia suala hilo kufikishwa katika ngazi mbali mbali za maamuzi ikiwemo Baraza lako tukufu. Hata hivyo, suala hili ilibidi kusitishwa kutokana na uamuzi wa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wa kupitisha maamuzi ya kufanya suala la utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi lisiwe suala la Muungano; uwezekano wa kulifanya suala hilo kuwa si la Muungano ni mkubwa sana.

Mhe. Spika, Wataalam wa mambo ya mafuta wametutahadharisha kwamba suala la uchimbaji mafuta na gesi hutawaliwa sana na rushwa tangu utafiti wake hadi uchimbaji. Rushwa hutawala katika utafiti, utoaji vibali, ukusanyaji wa mapato na pia uwazi wa shughuli yenyewe. Rushwa hiyo huwa baina mamlaka husika, utawala wa mapato, utoaji wa maamuzi na hugusa kampuni

za kuchimba mafuta, nchi zenye uwezo katika jambo hilo na hata watu binafsi. Kwa hivyo sheria ya rushwa lazima ilizingatie kabisa suala hili.

Mhe. Spika, wakati hilo likiendelea nawaomba Waheshimiwa wajumbe na wananchi tuwe wastahamilivu na bado masuala ya rushwa yatasimamiwa na sheria ya mwenendo wa jinai hapa Zanzibar. Aidha mkakati wa kupambana na rushwa ambao uliotayarishwa na kikosi kazi ni lazima uboreshwe, ili kukidhi haja hii na hatimae kuuwasilisha katika ngazi mbali mbali za maamuzi. Ni matumaini ya Wizara kuwa katika kipindi kifupi kijacho suala hili litakamilika.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Idara ya Uratibu Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Sh. 116,203,000.00. Kati ya fedha hizo Sh. 45,416,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 70,787,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, fedha zilizopatikana ni Sh. 68,755,912.00. Kati ya hizo, Sh. 32,955,912.00 sawa na asilimia 73 ni kwa mishahara na maposho, na Sh. 35,800,000.00 sawa na asilimia 51 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Sh. 210,000,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo mchango wa serikali ni Sh. 110,000,000.00 na Sh. 100,000,000.00 zilitegemewa kutoka kwa wadau wa maendeleo. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni Sh. 86,000,000.00 ambapo Sh. 75,000,000.00 sawa na asilimia 68 zilitoka serikalini *(angalia viambatisho 1&2)*.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, idara itaendelea kutekeleza kazi zake za kawaida ikiwa ni pamoja na:-

i. Kuweka utaratibu wa upatikanaji wa taarifa za utawala bora; na

ii. Kuunda kamati za maadili za wizara.

Mhe. Spika, ili idara hii iweze kutekeleza vyema shughuli zake ilizojipangia katika kipindi cha mwaka wa fedha ujao 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 130,516,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 35,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

## AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

Mhe. Spika, shughuli za Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali zinamuhusu kila mwananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na wageni ambao wanafanya shughuli zao visiwani humu. Kimsingi kazi za Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali zinalenga kwenye utekelezaji na usimamizi wa sheria na haki mbali mbali za wananchi kwa kutoa huduma za usajili wa aina mbali mbali kwa mujibu wa sheria husika.

Mhe. Spika, kwa ujumla Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inasimamia shughuli za uandikishaji wa Vizazi na Vifo; kuendesha na kusimamia Tirka za

Mali Maiti kwa Wasiokuwa Waislamu; uandikishaji wa Makampuni na Majina ya Biashara; na Uandikishaji wa Nyaraka mbali mbali. Afisi inahusika pia na uandikishaji wa Alama za Biashara na Vielelezo vya Uvumbuzi, pamoja na kusimamia shughuli zote zinazohusu Haki za Mali za Ubunifu; uandikishaji wa Ndoa na Talaka; uandikishaji wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali; na kutoa ushauri na maelekezo ya sheria kwa wananchi juu ya shughuli za afisi. Kazi hii ya msingi inazaa kazi nyengine mbili muhimu ambazo ni kutunza kumbukumbu zilizotokana na kazi za usajili ambazo hutumika kama marejeo na kutoa taarifa kwa taasisi za kitaifa, kimataifa pamoja na watu binafsi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka kumi ya awamu ya sita, Afisi imefanikiwa kuzifanyia marekebisho sheria tano na kutengeneza sheria mpya tatu zilizofuta sheria hizo tano. Sheria zenyewe ni (i) Sheria Nam. 14 ya mwaka 2004 ya Hakimiliki, ambapo Afisi ilisimamia kikamilifu mchakato mzima wa kuanzishwa kwa sheria hiyo na afisi yake (ii) Sheria Nam. 10 ya mwaka 2006 ya usajili wa vizazi na vifo, na (iii) Sheria Nam. nne (4) ya mwaka 2008 ya 'Industrial Property' ambayo imefuta sheria tatu za zamani (Patents Decree Cap. 157, Trade Marks Decree Cap. 159 na Industrial Designs Decree Cap. 158).

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza kazi zake za kawaida, ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2010, jumla ya vizazi 32,620 vimesajiliwa. Kati ya hivyo wanaume ni 14,798 na wanawake ni 17,822. Idadi hii kubwa kwa asilimia kulinganisha na ile ilyosajiliwa katika kipindi kama hiki cha mwaka wa fedha uliopita ambapo jumla ya vizazi 30,799 vilisajiliwa *(angalia kiambatisho Nam. 8a)*. Usajili wa vizazi vilivyochelewa kuandikishwa *(late registration*) ni 1337.

Mhe. Spika, jumla ya vifo 1,440 vimesajiliwa ambapo wanaume ni 879 na wanawake ni 561. Usajili wa vifo vilivyochelewa kuandikishwa (*late registration of death*) ni 20. Kwa upande wa urithi wa wasiokuwa waislam, '*estate duty'* moja na tirka tano zimefunguliwa na kushughulikiwa. Mabuku ya kusajili ndoa yaliyosambazwa ni 90 na ya kusajili talaka ni 18. Mabuku ya kusajili ndoa yaliyosambazwa mahakamani ni mawili na yale ya kusajili talaka ni 13.

Mhe. Spika, makampuni yaliyosajiliwa ni 171, majina ya biashara 277, alama za biashara (*Trademarks*) 502 na jumuiya zisizo za kiserikali (NGOs) 65. Nyaraka zilizosajiliwa ni 485 zinazohusisha nyaraka za Dhamana za Benki (A1), nyaraka za Mauziano na Urithi (A2), nyaraka za Wakfu, Hiba, Kiapo, Kodi n.k (A3) na waraka wa kufuta dhamana za Benki (*angalia kiambatisho Nam. 8b*). Usajili wa baadhi ya nyaraka za mauziano umehamishiwa Idara ya Ardhi. Wakati huo huo Afisi kwa mara ya kwanza imeanza kusajili mikataba ya uhaulishaji wa vyombo vya usafiri (magari na mapikipiki), ambapo jumla ya mikataba 170 imesajiliwa.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, hadi kufika mwezi wa Machi 2010, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali illitekeleza malengo yake iliyojiwekea kama ifuatavyo:

**Kuimarisha uwezo wa kiutendaji**

Mhe. Spika, katika kujiimarisha kiutendaji katika awamu hii ya sita, Afisi imeajiri wafanyakazi 20 katika kada mbali mbali wakiwemo wanasheria na wataalamu wa kompyuta. Afisi pia ina wasaidizi wawili wa usajili wa vizazi na vifo katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Afisi iliwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 19, wakati wafanyakazi 23 wamehudhuria katika mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi imewapeleka masomoni wafanyakazi wanne ngazi za Shahada ya Kwanza na Stashahada ya Uzamili. Idadi hii inafanya jumla ya wafanyakazi wanaoendelea na masomo ya muda mrefu katika fani mbali mbali kuwa tisa *(angalia kiambatisho namba 10b)*.

Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, Afisi imewapatia mafunzo ya "*Corporate Governanc*e" maafisa wake watano katika chuo cha ESAMI kilichopo Arusha. Aidha, Afisi imewapeleka maafisa wake wawili katika Afisi za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni Tanzania Bara kwa lengo la kuwapatia mafunzo ya utekelezaji wa mradi wa "Digitalization".

Mhe. Spika, Afisi iliandaa safari ya kimafunzo nchini Norway kuhusiana na mifumo ya kisasa inayotumika katika usajili wa biashara. Mifumo kama hiyo itatumiwa na Afisi baada ya kukamilika kwa Mradi wa Kuimarisha Mazingira ya Biashara. Safari hiyo iliwahusisha maafisa kutoka taasisi nyengine ambao ni wadau wa mradi huo zikiwemo Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Kuendeleza Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwa upande wa vitendea kazi, Afisi imepata kompyuta 14 ambapo 10 kati ya hizo zilitolewa kwa ufadhili wa Shirika la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA). Msaada huu ni hatua ya kuimarisha upatikanaji wa taarifa za vizazi na vifo kupitia mradi unaotekelezwa kwa mashirikiano na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar. Kompyuta hizo zimepelekwa katika ofisi za usajili wa vizazi na vifo za wilaya zote za Unguja na Pemba. Wakati kompyuta nne, "*server"* (1) printa (1) na skana (1) zimetolewa na Shirika la *"World Intellectual Property Organization"* (WIPO) kwa ajili ya kuimarisha usajili wa mali bunifu (Industrial Property).

Mhe. Spika, Afisi imekamilisha ujenzi wa jengo lake lilioko Pemba na tayari limeanza kutumika. Afisi pia imefanya ukarabati wa jengo lake sehemu ya kitengo cha usajili wa Mali Ubunifu (IP) na kuweka vifaa vipya. Vifaa hivyo vimepatikana kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa linaloshughulikia masuala

ya mali za ubunifu (WIPO). Shirika hilo pia lilileta wataalamu wake wawili kwa ajili ya kuweka mfumo mpya wa usajili unaolingana na mifumo mingine duniani, pamoja na kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya utunzaji na utumiaji wa mfumo huo. Aidha, Afisi imenunua jenereta kwa ajili ya umeme wa dharura.

**Kuendeleza mradi wa usajili wa vizazi na vifo**

Mhe. Spika, katika kulitekeleza lengo hili, kumeanzishwa kamati mbili za pamoja za mashirikiano, baina ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali *(Steering Committee na Technical Committee)* ambazo tayari zimeshakutana mara kadhaa na kujadili mwelekeo wa kusajili na kutoa taarifa za kitakwimu za vizazi na vifo. Aidha, maafisa sita wanaoshughulikia usajili wa vizazi na vifo walifanya safari ya kimafunzo katika Afisi za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ya Tanzania Bara kwa ajili ya kubadilishana uzoefu.

**Kuendelea kuzipitia sheria zinazoongoza kazi za usajili**

Mhe. Spika, Afisi imetayarisha rasimu tatu za sheria ambazo ni

(i) Sheria ya usajili wa biashara *(Business Registration Act)*;

(ii) Sheria ya usajili wa rehani au mali zinazohamishika *(Security on Movable Property Act Registration);* na

(iii) Sheria ya Ufilisi (*Insolvency Act*).

Katika kutayarisha rasimu hizo, Afisi ilizingatia umuhimu wa kuwashirikisha wadau mbali mbali. Pamoja na rasimu hizo Afisi imeandaa michanganuo ya mifumo ya usajili kwa kutumia kompyuta itakayotokana na sheria hizo. Kazi hii imewezeshwa kupitia Mradi wa kuimarisha mazingira ya biashara unaotekelezwa chini ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA),

**Kuikamilisha sheria ya uanzishwaji Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali**

Mhe. Spika, Afisi tayari imepokea mapendekezo ya kitaalamu yaliyolenga kuioanisha sheria ya uanzishwaji ya Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali na mageuzi ya shughuli za usajili yanayoendelea. Afisi inaendelea kuyafanyia kazi mapendekezo hayo. Hata hivyo, changamoto kubwa inayoikabili Afisi ni uchakavu wa jengo kiasi kwamba halitafaa kutumika kwa mifumo ya kisasa ya usajili inayotarajiwa kutengenezwa.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Mrajis Mkuu ilikadiriwa kutumia Sh. 286,339,000.00. Kati ya fedha hizo, Sh. 130,923,000.00 kwa ajili ya mishahara na maposho na Sh. 155,416,000.00 zimetengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kuanzia Julai 2009 hadi Machi 2010 kiasi cha Sh. 181,872,966.00 zimepatikana ambapo mishahara na maposho ni Sh 87,357,966.00 (67%) na Sh. 94,515,000.00 (61%) ni kwa matumizi mengineyo.

Aidha, Sh. 1,228,781,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo mchango wa serikali ni Sh. 60,000,000.00 na Sh. 1,168,781,000.00 zilitegemewa kutoka kwa wadau wa maendeleo. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni Sh. 572,096,033.00 ambapo Sh. 50,000,000.00 sawa na asilimia 83 zilitoka serikalini. Makadirio ya mapato kwa mwaka 2009/2010 ni Sh. 285,400,000.00. Kwa kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, fedha zilizokusanywa ni Sh. 161,019,670.00 sawa na asilimia 56.4 (angalia viambatanisho Nam. 1,2,&3).

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuipitia na kuiimarisha mifumo, kufanyia marekebisho sheria na kanuni zinazoongoza kazi za usajili
ii. Kuhakikisha rasimu za Sheria mbali mbali zilizotayarishwa zimepitishwa na kuwa sheria; na
iii. Kutayarisha mpango mkakati.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Sh. 258,250,000.00.

Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 307,766,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 4,437,720,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 25,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 4,412,720,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo).

**AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar ina majukumu kisheria ya kusimamia haki na maslahi ya wenye-hakimiliki wa ndani na nje ya Zanzibar ambao kazi zao zinahusika hapa Zanzibar. Aidha, ina jukumu la kutoa leseni kwa kuruhusu matumizi halali ya kazi za sanaa kwa kukusanya na kugawa

mirabaha kutoka kwa watumiaji mbali mbali wa kazi hizo. Afisi inaelimisha wasanii, wabunifu, watumiaji wa kazi na jamii kwa jumla ili dhana ya usimamizi wa pamoja ifikiwe. Hadi kufikia Machi 2010 utekelezaji wa malengo ulikuwa kama ifuatavyo.

**Kuimarisha utendaji**

Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki imeendesha jumla ya vikao sita vya Bodi ya Hakimiliki Zanzibar, ambapo vikao vinne ni vya kawaida na viwili ni vya dharura. Vikao hivyo ndivyo vinavyotoa mwongozo katika utekelezaji wa shughuli za afisi. Kutokana na kuanza shughuli za ukusanyaji wa mirabaha, Afisi imempeleka mhasibu wake kwenye Chama cha Hakimiliki Tanzania Bara (*COSOTA*) kwa mafunzo ya muda mfupi. Afisi pia imempeleka mfanyakazi wake mmoja katika mafunzo ya udereva. Kwa upande wa vitendea kazi, Afisi imenunua vifaa kwa ajili ya usajili wa kazi za kielektroniki ili kuimarisha afisi ya Pemba. Aidha, Afisi iliunga jenereta katika kukabiliana na dharura ya ukosefu wa umeme.

**Kuimarisha mfumo wa usajili wa kazi za ubunifu**

Mhe. Spika, Afisi kupitia wataalamu wa Shirika la Ulimwengu la Milki Ubunifu (*WIPO*) imefunga mfumo mpya wa Usajili na Usimamizi wa Pamoja wa Kazi za Hakimiliki (*The WIPO Software for Collective Management of Copyright and Related Rights – WIPOCOS)* na kuwapatia mafunzo wafanyakazi kuhusiana na matumizi na utunzaji wa mfumo huo. Manufaa yanayotokana na mfumo huu mpya ni pamoja na kuweka masharti bayana ya kuomba uanachama yenye lengo la kuondoa mizozo likiwemo kusaini waraka wa ridhaa (*deed of assignment*).

Mhe. Spika, suala la usajili ni ridhaa ya msanii kuikabidhi haki yake kwa Afisi. Katika kufikia makubaliano haya ni lazima kuwe na waraka unaoonesha ridhaa hiyo (*Deed of Assignment*). Kukosekana kwa waraka huu kulipelekea Afisi kukabili changamoto nyingi hasa kwa kazi za vikundi ambazo wabunifu waliochangia kazi hizo hukanusha usajili uliofanyika.

Mhe. Spika, kwa kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, Afisi imesajili jumla ya kazi 121 kwa Unguja na Pemba. Kazi hizo ni pamoja na muziki 79, Filamu 11, Maigizo 3, Miswada ya filamu 15, Miswada ya Mashairi 6, Vitabu 2, na Kasida rekodi 5. Idadi hii ni tofauti na mwaka uliopita ambapo jumla ya kazi 178 zilisajiliwa. Upungufu wa usajili umetokana na ukosefu wa umeme, kwani utayarishaji wa kazi hizi kwa kiasi kikubwa hutegemea umeme. Afisi imeshasajili jumla ya kazi 527 za sanaa na ubunifu kuanzia mwaka 2007 kazi hiyo ilipoanza.

**Kutoa na kusimamia utoaji wa leseni**

Mhe. Spika, Afisi imeshaanza kutoa leseni kwa kuruhusu matumizi halali ya kazi za sanaa na ubunifu kibiashara. Katika kusimamia utoaji wa leseni, Afisi imetoa mafunzo kwa watayarishaji na waendeshaji wa vipindi vya muziki na filamu katika vituo vyote vya utangazaji vilivyopo Zanzibar juu ya ujazaji wa Fomu za Marejesho (*Log Sheets*) kwa kazi zilizotumika kwa vituo vyote vya utangazaji Zanzibar. Fomu hizo ndizo zinazotumika katika kugawa mirabaha.

Mhe. Spika, ijapokuwa programu mbali mbali za elimu zimetolewa, bado kumekuwa na mwamko mdogo sana wa kukubali ukweli wa thamani ya hakimiliki kibiashara. Afisi imeendelea kufanya mazungumzo ya ana kwa ana kuwahamasisha watumiaji wa kazi kibiashara kufahamu umuhimu wa kulipia matumizi ya kazi za sanaa. Mazungumzo hayo yalianza na Umoja wa Wawekezaji wa Utalii Zanzibar (ZATI) kwa lengo la kuwafikia kirahisi watumiaji wa mahoteli na mikahawa ambamo kazi za sanaa na ubunifu zinatumika.

Mhe. Spika, katika kipindi hiki wamiliki wanane wenye maduka ya kukodishia na kuuza kanda za Video na CD's wameanza kulipa kwa mpangilio maalumu waliopangiwa na afisi**.** Idadi hii ndogo inatokana na ukosefu wa umeme ambao ulizorotesha zoezi la ukusanyaji katika vyanzo hivyo. Kwa upande mwengine, Afisi ilifanikiwa kufikia muafaka wa malalamiko kati ya Nadi Ikhwan Safaa na Chuo cha Muziki Zanzibar ambapo chuo cha Muziki kitailipa Nadi Ikhwan Safaa dola za kimarekani 5,000 kwa kutumia kazi za Nadi Ikhwan Safaa bila ya ridhaa yao.

Mhe. Spika, Afisi imeendelea kukusanya malipo ya kazi za sanaa kutoka katika vyombo vya habari vya umma. Naipongeza Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuonesha mfano katika ulipiaji wa matumizi ya kazi za sanaa. Kwa upande wa vyombo vya habari binafsi zoezi hili bado halijafanikiwa kwa sababu Afisi ipo katika kuangalia uwezekano wa kuzingatia maombi yao ya kupatiwa unafuu wa viwango vya malipo. Aidha, katika kusimamia haki na maslahi ya wenye-hakimiliki wa Zanzibar kimataifa, Afisi imeomba kujiunga na Shirikisho la Kimataifa la Taasisi za Watunzi na Washairi Ulimwenguni (*The International Confederation of Authors and Composers Societies – CISAC).*

**Kukuza uelewa wa jamii juu ya dhana na sheria ya hakimiliki**

Mhe. Spika, Afisi imeendelea kuelimisha jamii juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki (Nam.14) ya mwaka 2003 kupitia programu za redio na televisheni. Jumla ya vipindi thelathini na nane (38) vya televisheni na vinane vya redio kwa Unguja na Pemba vilirushwa. Afisi imefanya tathmini katika wilaya zote kumi za Zanzibar kupima uelewa wa jamii kwa vipindi vyake vyote vilivyoanza kurushwa kuanzia mwaka 2007. Tathmini hiyo imeonesha kuwa elimu juu ya dhana na Sheria ya Hakimiliki kwa njia ya televisheni haikufika Pemba ukilinganisha na Unguja. Hali hii imesababishwa na tatizo la ukosefu

wa matangazo ya vyombo hivyo huko Pemba. Kwa upande wa Unguja, mwamko wa elimu haukuwa mzuri vijijini ikilinganishwa na mjini. Afisi imejipanga kutumia taratibu nyengine zaidi za kuwafikia walengwa *(outreach programs).*

**Utafiti wa kiwango cha ubunifu na mchango wake kiuchumi**

Mhe. Spika, matokeo ya awali ya utafiti uliofanyika mwaka 2008 – 2009, ambayo yamepatikana katika kipindi hiki, yameonesha kuwa kuna jumla ya wabunifu 2,034 waliorodheshwa, ambapo 1,376 ni kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na wabunifu 658 kwa mkoa wa Kaskazini Unguja. *Kiambatisho 8c* kinafafanua idadi hiyo katika makundi ya kazi za ubunifu na sanaa kama ambavyo matokeo hayo ya awali yanavyoonesha. Sura halisi ya matokeo ya utafiti itapatikana baada ya kumalizika kwa mikoa mitatu iliyobakia.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki iliidhinishiwa ruzuku ya Sh. 120,000,000.00. Kati ya hizo, Sh. 16,140,900.00 ni kwa mishahara na maposho na Sh. 103,859,100.00 ni kwa matumizi mengineyo *(angalia kiambatisho Nam. 1)*.

Mhe. Spika, pamoja na kujiimarisha kiutendaji, katika mwaka ujao wa fedha Afisi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo;

i. Kuongeza kasi ya ulipiaji kazi za sanaa na ubunifu kwa watumiaji kibiashara; na
ii. Kukamilisha utafiti wa kiwango cha ubunifu katika mikoa mitatu iliyobaki.

Mhe. Spika, ili Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha, 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Ruzuku ya Sh. 120,000,000.00.

## KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina jukumu kubwa kisheria la kusimamia Mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya kheri. Katika utekelezaji wa kazi za kawaida, Kamisheni imeweza kuendesha tirka za Urithi kwa muda mfupi pale masharti yote yalipokamilika na pakawa hapana vizuizi. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 jumla ya Tirka mpya 298 zimefunguliwa na Tirka 234 zenye thamani ya Sh. 1,531,911,340.35 zimefungwa.

Mhe. Spika, kwa vile masuala ya mirathi mara nyengine hupelekea mizozo ya kifamilia miongoni mwa warathi, Kamisheni hujitahidi kuisuluhisha na pale inaposhindikana tu ndio hupelekwa mahakamani. Katika kipindi hiki mizozo minane imeshughulikiwa, mitatu kati ya hiyo imesuluhishwa na warathi

wamekubaliana, minne inaendelea na usuluhishi na mmoja umepelekwa mahakamani.

Mhe. Spika, Mali za Wakfu na Amana zimeendelea kusimamiwa vyema na Kamisheni na kupelekea kukusanywa jumla ya Sh. 124,910,157.00 kwa wapangaji wa nyumba 462 za Wakfu na Amana. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2010 jumla ya Shillingi 10,131,500.00 zimetumika kwa kuzifanyia matengenezo madogo madogo nyumba 10 na Sh. 5,400,000.00 katika kuendeleza ujenzi wa nyumba ya ghorofa tatu ya Wakfu iliyoko Mbweni ambayo hadi sasa gharama za ujenzi wake zimefikia Sh. 168,667,000.00

Mhe. Spika, Kamisheni imeendelea na kazi ya usimamizi wa mashamba manne na vikataa tisa vya wakfu na imekusanya jumla ya Sh. 4,160,000.00 kutokana na kodi ya mashamba na vikataa hivyo. Kamisheni pia imewalipa mafao yao wanufaika wa wakfu kiasi cha Sh. 5,395,000.00 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu imeendelea na kazi za ufuatiliaji wa kodi zake na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 imekuwa inazidai taasisi za serikali jumla ya sh. 13,900,000.00 ikiwa ni malimbikizo ya madeni ya kodi za afisi mbali mbali. Kwa upande mwingine, kazi za usimamizi wa kesi katika mahakama mbali mbali umekuwa ukiendelea vizuri. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010, Kamisheni imezisimamia jumla ya kesi 42. Kesi 12 zimeshatolewa maamuzi na kesi 30 bado zinaendelea (*angalia kiambatisho 9a*).

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu imeiwakilisha Zanzibar katika vikao vya kutathmini Hijja ya mwaka 1429H na kupanga utaratibu wa kufanikisha Hijja ya mwaka 1430H huko nchini Saudi Arabia. Kamisheni pia ilisimamia uratibu wa safari ya Hijja kwa taasisi zote 14 za Tanzania ambapo taasisi nane kati ya hizo zimesajiliwa Zanzibar. Jumla ya Mahujaji 1951 kutoka Tanzania walishiriki ibada ya Hijja huko nchini Saudi Arabia. Uchambuzi wa Mahujaji upo katika *kiambatisho Nam. 9b*. Mahujaji 1,053 kati ya hao walisafirishwa na taasisi za Zanzibar. Mahujaji wawili walifariki dunia Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, kwa upande wa misaada ya kheri, Kamisheni imepokea tani 26.65 za sadaka ya nyama kutoka Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB) na kuigawa katika taasisi na baadhi ya misikiti ya Unguja na Pemba. Aidha, Kamisheni ya Wakfu imepokea katuni 200 za tende kutoka Ubalozi wa Falme za Kiarabu (UAE) na kuzigawa Unguja na Pemba. Pia imegawa futari iliyotolewa na Ubalozi wa Saudi Arabia kwa watoto yatima 200 katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Aidha, Kamisheni imeziombea msamaha wa ushuru jumuiya na misikiti kama inavyoonyesha kwenye *kiambatisho Nam. 9c*.

**Kuongeza uwezo na uelewa wa Sheria ya Kamisheni kwa wadau**

Mhe. Spika, katika kukuza uelewa wa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2007, Kamisheni imetoa taaluma kupitia vyombo vya habari kama vile televisheni, redio na magazeti. Kamisheni pia imekutana na kuzielimisha taasisi zinazosafirisha mahujaji kwa kutoa miongozo na maelekezo. Vile vile Kamisheni imeanza kutoa taaluma juu ya matakwa ya Sheria Nam. 2 ya mwaka 2007 kuhusu kukusanya na kugawa zakka na misaada ya kheri. Wakati huo huo**,** wafanyakazi wanne wa Kamisheni wamejiunga na masomo ya Shahada *(angalia kiambatisho namba 10b)*.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iliidhinishiwa ruzuku ya Sh. 274,000,000.00. Kati ya hizo, Sh. 160,579,829.00 ni kwa mishahara na maposho na Sh. 113,420,171.00 ni kwa matumizi mengineyo. Fedha zilizopatikana ni Sh. 197,971,890.00 ambapo mishahara na maposho ni Sh. 122,054,226.00, sawa na asilimia 76 na Sh. 75,917,664.00, sawa na asilimia 67 kwa matumizi mengine *(angalia kiambatisho Nam. 1)*.

Mhe. Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itatekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutayarisha utaratibu wa kuongeza makusanyo ya zaka na kuratibu vyema ugawaji wake;
ii. Kutayarisha mpango mkakati wa Kamisheni; na
iii. Kufanya mapitio ya mfumo mzima wa uwekaji na utunzaji wa nyaraka za Kamisheni.

Mhe. Spika, ili Kamisheni iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha 2010/2011, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Ruzuku ya Sh. 300,000,000.00.

**AFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Afisi Kuu Pemba imeendelea kuratibu shughuli zake kwa ufanisi na kuwa karibu na jamii na jumuia za kiraia katika kutoa huduma zilizo bora. Katika kipindi hiki Afisi imetekeleza yafuatayo:-

Mhe. Spika, kupitia Afisi ya Mufti, imeendelea kuratibu shughuli mbali mbali ikiwemo kutatua migogoro ya wanandoa, wanajamii na kutoa fat-wa ya masuala mbali mbali ya sheria ya kiislam ambayo walihitaji kupata ufafanuzi wa kisheria. Jumla ya masuala 111 yamepokelewa na kutolewa fat-wa. Majibu hayo hutolewa ufafanuzi kwa muhusika alieuliza na si kwa njia ya redio. Mizozo 18 ya misikiti imepokelewa na yote imepatiwa suluhu. Mizozo ya ndoa

55 imepokelewa na kati ya hiyo 49 imepatiwa suluhu na mizozo 6 walielekezwa wahusika kwenda katika Mahakama ya Kadhi baada ya wenyewe kukataa suluhu. Aidha, Afisi imeweza kujenga uhusiano mzuri na taasisi za kiislamu pamoja na wanajamii kwa ujumla, na kwa sasa taasisi na jamii wanaitumia ipasavyo afisi hii.

Mhe. Spika, katika kuratibu Jumuia Zisizokua za Kiserikali wizara imeandaa mazingira mazuri katika kuziwezesha jumuia hizo kufanya kazi zake kwa ufanisi. Jumla ya jumuiya 10 zimesaidiwa katika kuomba miradi kutoka kwa wafadhili. Aidha, Afisi kwa kushirikiana na Idara ya Fedha za Nje ya Wizara ya Fedha na Uchumi, imetoa mafunzo ya siku mbili kwa jumuiya 40 za Pemba. Mafunzo hayo yalihusu uhamasishaji wa jumuiya hizo kutoa taarifa za fedha wanazozipata kutoka kwa wafadhili ili serikali iweze kujua kiasi cha fedha zinazoingia nchini pamoja na shughuli zinazofanywa na jumuiya hizo. Baada ya mafunzo hayo, jumuiya nying**i** zimehamasika na zimeanza kuwasilisha ripori hizo.

Mhe. Spika, ili kuimarisha utendaji wake Afisi imeufanyia matengenezo ukumbi wa mikutano na kununua samani. Aidha, Afisi katika kuongeza nguvu za kiutendaji na ufanisi, imeajiri wafanyakazi watano ambao ni wahitimu wa Shahada ya Kwanza kwa mujibu wa kada zao.

Mhe. Spika, Afisi Kuu Pemba imefanya juhudi kubwa ya kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake wanne, akiwemo mwanamke mmoja, kwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika fani ya utawala, uhasibu na useketeri *(angalia kiambatisho namba 10b)*. Afisi pia imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wanne kwa kozi mbali mbali. Aidha, mfanyakazi mmoja ameshiriki katika mafunzo ya wiki moja nchini Qatar juu ya umuhimu wa utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa.

Mhe. Spika, katika kupiga vita ugonjwa wa UKIMWI sehemu za kazi, Afisi imezijengea uwezo jumuiya za kiraia 50 ambazo zinajihusisha na masuala ya UKIMWI juu ya uwajibikaji, ushirikishaji na uwazi katika utekelezaji wa kazi zao. Afisi pia imewapatia mafunzo ya siku moja wafanyakazi 100 na familia zao. Aidha, kamati ya UKIMWI ya wizara imeweza kufanya mikutano na wafanyakazi wote wa taasisi na idara za wizara Pemba ili kuhamasisha wafanyakazi umuhimu wa kupima na kujua afya zao.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Afisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla Sh. 203,353,000.00 kati ya hizo Sh. 105,750,000.00 ni mishahara na maposho na Sh. 97,603,000.00 ni matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi 2010 fedha zilizopatikana ni Sh. 132,806,183.00. Kati ya hizo Sh. 82,034,994.00 sawa na asilimia 78 ni mishahara na maposho na Sh. 50,771,189.00 sawa na asilimia 52 matumizi mengineyo *(angalia kiambatisho Nam. 1)*.

Mhe. Spika, katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011, Afisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu shughuli za wizara, kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma na kuwaelimisha juu ya ugonjwa wa UKIMWI. Afisi Kuu Pemba inaazimia:

-Kutayarisha mpango mkakati wa afisi

Mhe. Spika, ili Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza shughuli zake hizo naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 223,558,000 kwa kazi za kawaida.

**SHUKURANI**

Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiwasilisha Hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Aidha, haitokuwa jambo la busara kama sitatoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbali mbali za wizara pamoja na taasisi zake zote. Shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu. Sambamba na hilo natoa shukurani kwa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa taasisi za wizara yangu kwa hatua nzuri za kiutendaji. Vile vile kwa niaba ya watendaji wa wizara yangu napenda kutoa shukurani kwa Wajumbe wa Baraza hili kwa michango yao mizuri na yenye manufaa kwa wizara na taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika, wizara yangu imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano na wafadhili na wahisani mbali mbali na kwa heshima na taadhima naomba ruhusa yako kuwashukuru wale wote wanaotusaidia wakiwemo UNDP, ADB, WIPO, GLOBAL FUND, WORLD BANK, *Africa Muslims Agency, Al - Youseif Charitable Society,* Serikali ya Saud Arabia, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania, Swedish *National Audit Office (SNAO), Islamic Development Bank,* Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC) na vikundi mbali mbali vilivyosafirisha Mahujaji.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe matumizi ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 ya jumla ya Sh. 5,533,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Sh. 9,632,515,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 1,740,000,000.00 kutoka serikalini na Sh. 7,892,515,000.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo) ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. Aidha, naliomba baraza lako likubali mchango wa Sh. 299,870,000.00 ikiwa ni mapato yatakayokusanywa na wizara hii ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Haji Mkema Haji: (Kny. Mhe. Haji Omar Kheri Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Mhe. Spika, awali ya yote, napenda

kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili, nikiwa na afya njema, ili niwasilishe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Spika, halkadhalika, napenda kukushukuru na wewe Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya awali ya kutoa maoni ya Kamati yetu katika Wizara hii muhimu katika utawala wa nchi yetu.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa ustadi wake katika kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yake, lakini pia, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Uatawala Bora waliohusika, kwa namna moja au nyengine, katika kumtayarishia Mhe. Waziri hotuba hii aliyoisoma hivi punde.

Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ndio Wizara ya mwisho ambayo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiwasilishia maoni na mapendekezo yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Na kwa kuwa tumo ukingoni mwa Baraza letu hili la Saba, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mashirikiano na mshikamano mzuri waliouonesha kwa muda wote ambao Kamati yetu imekuwa ikitekeleza shughuli zake mbali mbali. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atukutanishe tena katika Baraza lijalo la Nane ili tuweze kuendeleza pale tulipofikia.

Mhe. Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Haji Omar Kheri | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Haji Mkema Haji | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Zahra Ali Hamad | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Fatma Abdalla Tamim | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Suleiman Hemed Khamis | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Najma Khalfan Juma | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | - | Mjumbe |
| 11. | Ndg. Nasra Awadh Salmin | - | Katibu |
| 12. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | - | Katibu |

Mhe. Spika**,** kabla ya kutoa maoni ya Kamati yetu ninaomba uniruhusu kutoa masikitiko ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa baadhi ya Taasisi za Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha nilioutaja hapo kabla Kamati yetu haikupata mashirikiano mazuri na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hapa ninamaanisha kuwa wakati Kamati yetu inatekeleza majukumu yake katika mzunguko wa tatu Afisi hii ilishindwa kuwasilisha taarifa za kiutendaji kutokana na kukosekana mwakilishi wa Afisi hii.

Aidha, katika mzunguko wa nne Afisi hii iliwakilishwa na Mtendaji ambaye alishindwa kutoa majibu kama alivyoulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii. Mhe. Spika, katika mzunguko huo huo wa nne Kamati haikupata taarifa za kiutendaji kutoka Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na sababu iliyotolewa ni kuwa Mrajis Mkuu wa Serikali yupo nje ya nchi. Mhe. Spika, tunaelewa kuwa endapo kiongozi wa Taasisi atakuwa nje ya Zanzibar au anakabiliwa na dharura yoyote ile basi majukumu yake hutekelezwa na mtu mwengine kwa niaba yake.

Mhe. Spika, Kamati yetu imeona isilifumbie macho hili ili wizara hii ijipange vyema kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwani baadhi ya Taasisi zilizochini ya wizara hii kwa makusudi huichafulia jina wizara hii muhimu inayosimamia utawala bora.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa uniruhusu nitoe maoni yangu kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Wananchi wangu wa Jimbo la Koani.

**IDARA YA MIPANGO NA SERA**

Mhe. Spika**,** Kamati ya Katiba Sheria na Utawala inaipongeza kwa dhati Idara ya Mipango na Sera kwa jinsi ilivyosimamia vyema Mipango na Sera za Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Aidha, tunaipongeza Serikali kwa kuipatia gari Idara hii. Hatua hii itaiwezesha Idara hii kuzidi kutekeleza vyema majukumu yake iliyojipangia.

Mhe. Spika, ukurasa wa 552 wa Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2010/2011 unatuonesha kuwa Idara ya Mipango na Sera imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 35,000,000/- kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Utawala Bora. Kasma 72200 ya Kifungu 04 inathibitisha kauli yangu hiyo. Mhe. Spika, Kamati yetu inaunga mkono hili hasa kwa kuzingatia kuwa kuna haja ya kuimarisha utawala bora katika nchi yetu, kwani ripoti zinazotolewa na Taasisi

mbalimbali zinaonesha kuwa bado Zanzibar utawala bora hautekelezwi ipasavyo. Hivyo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba Idara hii iwe na mashirikiano ya karibu na Idara ya Uratibu wa Utawala Bora katika kutekeleza hili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katueleza kuwa katika mwaka wa fedha ujao, Idara hii inatarajia kuandaa ripoti ya utekelezaji ya miaka 10. Mhe. Spika, hatuna pingamizi na lengo hili kwani litaiwezesha wizara hii kujua ni mafanikio yaliyopatika, changamoto zilizopo pamoja na kuweka mikakati bora itakayozikabili changamoto hizo.

**AFISI YA MRAJISI MKUU WA SERIKALI**

Mhe. Spika, Afisi hii inajukumu la kusimamia na kushughulikia masuala yote ya usajili chini ya Sheria mbali mbali zilizopo pamoja na kutoa ushauri wa maelekezo ya Sheria hizo kwa wananchi, ili waweze kuzitambua shughuli za Afisi hii. Mhe. Spika, ingawa Afisi hii inatekeleza shughuli zake kwa ufanisi mkubwa, hata hivyo, inakabiliwa na baadhi ya changamoto ambazo ni busara Serikali ikazichukulia hatua haraka iwezekanavyo kwa maslahi ya maendeleo ya nchi yetu. Kwani kuna uwezekano mkubwa changamoto hizi zikaviza ufanisi uliokusudiwa. Miongoni mwa changamoto hizo ni;- Jengo la Afisi hii ni la zamani na halitoshi. Jambo hili lilipelekea Mfumo wa Vizazi na Vifo na Mfumo wa Alama za Biashara, na Makampuni kuharibika kutokana na kuangukiwa na udongo. Kutokana na kadhia hiyo, kamati inashauri kukodiwa sehemu afisi hii, ili tuzithamini juhudi za Wahisani wa Maendeleo kwani mifumo hii iligharimu fedha nyingi na kwa muda mfupi tu imeanza kuharibika.

Mhe. Spika, kwa kuwa Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali inaratajia kujenga afisi mpya huko Mazizini na kwa kuwa shughuli za taasisi mbili hizi zinafanana kamati inazidi kuiomba Serikali kuziweka afisi hizi pamoja ili zizidi kushirikiana vyema katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, tunaelewa kuwa kwa kipindi hiki Serikali yetu inakabiliwa na mambo muhimu ambayo hayawezi kuepukwa. Hata hivyo, kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti ya matumizi ya kazi za maendeleo afisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hii ni kutokana na kuwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 afisi hii ilikadiriwa kutumia Tsh. 60,000,000/- ikiwa ni mchango wa Serikali kwa kazi za maendeleo, wakati kwa mwaka ujao wa fedha imekadiriwa kutumia Tsh. 25,000,000/- tu ikiwa ni upungufu wa zaidi ya asilimia 50.

Aidha, tunaiomba Serikali kwa nguvu zetu zote kuipatia usafiri Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Kwani kwa hivi sasa afisi hii haina usafiri kwa Unguja na Pemba. Mhe. Spika, kamati yetu inaomba hili, kutokana na kuwa Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inajukumu zito la kufuatilia shughuli zake kwa Wilaya zote 10 za Zanzibar.

**AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala inaipongeza afisi hii kwa jitihada zao wanazozifanya katika kusimamia na kuendesha kesi za jinai katika Mahakama mbali mbali kama kifungu cha 56A cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinavyoelekeza. Mhe. Spika, tunaipongeza afisi hii kwa jitihada zao wanazozifanya katika kuimarisha afisi hii kiutendaji kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la afisi ya kisasa Unguja. Kamati yetu inathamini juhudi hizi kwani watendaji wa afisi watazidi kutekeleza majukumu yao katika mazingira bora kama mikataba na maazimio mbali mbali ya kazi yanavyoelekeza.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2010/2011 inatarajia kuanza ujenzi wa Afisi Pemba. Hivyo, kwa kuwa eneo la Tibirinzi – Pemba ardhi yake ni laini. Mhe. Spika, kamati inamshauri Mkandarasi wa Jengo la Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuchukua juhudi za makusudi na kuhakikisha kuwa tahadhari zote zinachukuliwa wakati wa ujenzi wa jengo hilo ili tusije tukaitia hasara Serikali.

**AFISI YA MWANASHERIA MKUU**

Mhe. Spika, tunaipongeza afisi hii kwa kuendelea kuchapisha sheria za Zanzibar pamoja na Sheria ndogo ndogo. Kwani jambo hili itawawezesha wananchi kufanya rejea "*reference*" bila usumbufu wowote endapo watahitaji kufanya hivyo. Aidha, litasaidia kuzihifadhi Sheria zetu ili zisipotee.

Mhe. Spika, kwa kuwa afisi hii imepatiwa kiwanja cha kujenga afisi yake huko Pemba katika eneo la Tibirinzi. Tunaiomba afisi hii kuuzingatia ushauri tulioutoa kwa upande wa kiwanja cha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwani viwanja hivi vipo katika eneo moja.

Sambamba na hayo, tunaipongeza kwa moyo wa dhati afisi hii kwa utaratibu wao waliouanzisha wa kutoa taarifa zao mbali mbali kwa njia ya mtandao. Kwa hakika utaratibu huu utasaidia upatikanaji wa taarifa za utekelezaji wa afisi hii kwa haraka, pia, kutawawezesha wananchi kutoa maoni yao mbali mbali kwa wepesi. Hatua hii itasaidia kuleta maendeleo zaidi ya kuitendaji kwa afisi hii. Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo, tunapenda kuchukua nafasi hii kuziomba na

taasisi nyengine ambazo hazijafungua tovuti kuiga mfano huu kwa maslahi ya maendeleo ya taasisi zao na wananchi kwa ujumla.

**AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI**

Mhe. Spika, kwa kiasi fulani Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imeridhishwa na utendaji wa Afisi ya Hakimiliki kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua. Ikiwa ni pamoja na kuielimisha jamii juu ya dhana nzima na Sheria ya Hakimiliki. Mhe. Spika, afisi hii kwa upande mwengine tunaweza kusema kuwa inatoa ajira kwa wananchi wanaojihusisha na mambo ya sanaa na ubunifu endapo watasajili kazi zao hizo. Hata hivyo, kamati yetu inaomba kufanyiwa mapitio Kanuni za Hakimiliki, kwani imebainika kuwa kiwango cha fedha wanachotozwa watumiaji wa kazi hizi ni kikubwa mno ukilinganisha na nchi nyengine duniani. Ingawa wasanii na wabunifu wetu bado hawaridhiki na kile wanachokipata kutokana na gharama kubwa wanazozipata.

**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

Mhe. Spika, afisi hii ni muhimu sana katika kulinda fedha na raslimali za taifa, kwani miongoni mwa majukumu yake ni kuzifanyia ukaguzi Taasisi za Serikali pamoja na Miradi ya Maendeleo. Mhe. Spika, kamati yetu inaiomba afisi hii kuzidi kuwa makini wakati inapotekeleza jukumu lake hili, ili kulinda fedha za wananchi wa nchi hii pamoja na kuzithamini nguvu za Washirika wa Maendeleo. Mhe. Spika, hapa tunamaanisha kuwa ni muhimu sana kuona hatua zinanzostahiki zinachukuliwa iwapo itagundulikana katika taasisi yoyote ile kuna upotevu wa fedha au matumizi yasiyokubalika ili kuleta mantiki na dhana halisi ya kuwepo kwa afisi hii.

Mhe. Spika, kamati yetu haikuridhika na kiwango cha mapato kilichokusanya na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tunasema haya baada ya Mhe. Waziri kutueleza kuwa katika mwaka wa fedha 2009/2010 Afisi hii ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 4,000,000/-. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikusanya jumla ya Tsh. 2,500,000/-, ingawa katika Kiambatanisho 3 ukurasa wa 58 wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri kinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi wa Juni, 2010 afisi hii inatarajia kukusanya kwa asilimia 100.

Mhe. Spika, kutokana na makusanyo hayo kuwa madogo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaiomba afisi hii kuyachukulia hatua haraka iwezekanavyo mashirika yote ambayo hayakutoa ada ya uchunguzi wa hesabu. Kamati inatoa ushauri huo baada ya kubaini kuwa mashirika haya hayalipi ada hizo sio kama hayana uwezo wa kufanya hivyo, bali yanafanya hivyo, kwa kuonesha dharau

mbele ya Serikali. Mhe. Spika,,kama yapo mashirika ambayo hayana uwezo wa kilipa ada hiyo, kamati yetu inashauri Mashirika hayo yafutiwe usajili wao. Kwani ni vyema kuwa na mashirika kidogo ambayo yanaleta tija kuliko kuwa na utitiri wa mashirika ambayo hayana faida yoyote.

**MAHAKAMA**

Mhe. Spika, tumefarajika sana na hatua ya Serikali ya kuitengea Mahakama Kuu Zanzibar jumla Tsh. 150,000,000/- kwa ajili ya Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja. Kamati yetu inalipongeza hili na inaiomba Serikali kuziingiza fedha hizi mapema ili lengo lililokusudiwa litekelezwe. Kamati yetu inasisitiza hili, kwani jengo la Mahakama ya Mkoa huu liliopo hapo Mwera lipo kwenye makaazi ya watu.

Mhe. Spika, tunaunga mkono lengo la 3 la Mahakama ambalo ni uanzishaji wa Mahkama ya Biashara. Mpango huu ni mzuri kwani utaruhusu kesi zinazohusiana na masuala ya biashara moja kwa moja kusikilizwa katika mahakama hiyo. Aidha, utaziwezesha kesi za makosa mengine kutolewa maamuzi haraka, kwani kutakuwa hakuna mrundikano mkubwa wa majalada ya kesi katika Mahakama zetu. Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo, kamati yetu inaiomba Mahakama kumteua Hakimu ambaye atakuwa ana sifa za kusikiliza kesi zinazohusiana na mambo hayo ili lengo lililokusudiwa lifikiwe.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri katueleza kuwa Mahakama inatarajia kufanya ukarabati wa majengo yake manne na hakuyabainisha majengo hayo. Tunamuomba aweke kipaumbele zaidi kwa majengo ya Pemba. Kwani asilimia kubwa ya majengo haya ni machakavu ingawa yanafanyiwa matengenezo mara kwa mara. Sambamba na hilo, kamati yetu inaishauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi za kuliondosha tatizo la mchwa katika Mahakama ya Konde. Kwa kuanzia tunaishauri Mahakama kupata ushauri katika Afisi ya Rais Ikulu juu ya kukabiliana na tatizo hilo. Tunashauri hivyo, kwa kuwa afisi hii pia ilikuwa na tatizo kama hilo na hivi sasa limekwisha.

Mhe. Spika, Mahakama Pemba ina upungufu wa Makadhi wa Wilaya hususan Mahakama ya Kadhi ya Wilaya ya Konde kufuatia kifo cha Kadhi huyo. Aidha, hivi sasa Kadhi wa Wilaya ya Chake Chake anasikiliza kesi za Konde na Wete kwa kuwa Kadhi wa Wete ni mgonjwa. Mhe. Spika, kamati yetu inaishauri kuchaguliwa haraka iwezekanavyo Makadhi wa kushika nafasi hizi, ili kuondosha usumbufu kwa watendaji hawa pamoja na wananchi kwa ujumla. Mhe. Spika, kwa kuwa watu wa kushika nafasi hizi wamefanyiwa usaili "*interview*" siku nyingi zilizopita tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze ni sababu gani zinazoikwamisha Tume ya Utumishi ya Mahakama kushindwa kulitekeleza hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa vyuo mbali mbali vinatoa taaluma kuhusiana na Sheria ya Kiislamu na kwa kuwa Sheria Nam. 3/1985 haijawazuia vijana kushika nafasi ya Ukadhi. Kamati yetu inashauri wachaguliwe vijana ambao wanahitimu katika vyuo vyetu hivi. Hii ni kutokana na kuwa Makadhi wetu wengi aliopo hivi sasa wana umri mkubwa, jambo ambalo linapelekea kukosekana ufanisi mzuri unaotakiwa wa shughuli zao hizi.

**IDARA YA URATIBU UTAWALA BORA**

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu Utawala Bora inakusudia kuunda Kamati za Maadili za wizara katika mwaka wa fedha ujao. Kamati yetu haina pingamizi na uundwaji huo. Hata hivyo, inaishauri idara hii kuhakikisha kuwa kamati hizi zinatekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, tunashauri kuwa kila Kamati ya Wizara ihakikishe kuwa inawasilisha ripoti ya utekelezaji wa shughuli zake mbele ya idara hii kila baada ya miezi mitatu. Ili Idara ya Uratibu Utawala Bora iweze kufanya tathmini juu ya mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa kamati hizi. Mhe. Spika, tunazidi kulisisitiza hili kutokana na sababu nilizozieleza wakati natoa maelezo kwa upande wa Idara ya Mipango na Sera.

**AFISI YA MUFTI**

Mhe. Spika, tunaipongeza Afisi ya Mufti kwa jitihada zao wanazozichukuwa kwa kushughulikia migogoro mbali mbali na kuipatia ufumbuzi, sambamba na kuyapatia ufafanuzi masuali mbali mbali ya kidini yanayofikishwa afisini hapo kupitia vyombo vya habari. Mhe. Spika, tunaunga mkono hili, hata hivyo tunaiomba afisi hii kutoa muongozo bora kama sheria ya dini inavyoelekeza. Hii ni kutokana na kuwa jamii ya Kiislamu inategemea kwenye majibu yaliyotolewa na afisi hii, kwa kuwa ni miongoni mwa chombo kinachoshughulikia masuala ya Kiislamu kwa Zanzibar. Mhe. Spika, pamoja na maelezo hayo, kamati yetu inawashauri waumini wa dini ya Kiislamu kuendelea kutafuta elimu ya dini yao zaidi, pamoja na kuendeleza mashirikiano na mshikamano kwenye masuala mbali mbali ya kijamii kama misingi ya dini hiyo inavyoelekeza.

**KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA**

Mhe. Spika, kamati hii imerafajika sana na tamko la Mhe. Waziri wa wizara hii kuwa Afisi ya Wakfu na Mali ya Amana kwa mwaka wa fedha ujao inatarajia kufanya mapitio ya mfumo mzima wa uwekaji na utunzaji wa nyaraka za Kamisheni. Mhe. Spika, mpango huu utauwezesha Kamisheni hii kujua idadi halisi za Wakfu na Mali za Amana. Kwani kwa hivi sasa Kamisheni ya Wakfu na Mali za Amana haijui idadi za Wakfu na Mali za Amana. Mhe. Spika, kwa

kuthibitisha kauli yangu hii, mnamo mwezi wa Mei, 2010 tulielezwa kuwa Kamisheni hii imezibaini nyumba 2 za Wakfu na shamba 1 huko Pemba. Hivyo, kutokana na kasoro hizo tunaiomba afisi hii kuwa makini katika kutekeleza malengo yake.

**AFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, tunaipongeza Afisi Kuu Pemba kwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli za Wizara ya Katiba Sheria na Utawala Bora kwa upande wa Pemba. Ni matarajio yetu kwamba jitihada hizi zitaongezeka na kuleta ufanisi mkubwa kwa wizara hii na kuleta mafanikio yanayotarajiwa katika mwaka wa fedha 2010/2011.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, ili wakatekeleze majukumu yao kwa mwaka wa fedha 2010/2011, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waidhinishe matumizi ya Tsh. 5,533,000,000/- kwa kazi za kawaida na Tsh. 9,632,515,000/- kwa kazi za maendeleo kwa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora na taasisi zake. Aidha, naliomba Baraza hili pia likubali mchango wa Tsh. 299,870,000/- ikiwa ni mapato yatakayokusanywa na wizara hii ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kimsingi huu ndio mukhtasari unaohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Tunawaomba wajumbe wote wa Baraza hili nao waichangie vizuri hotuba hii kwa madhumuni ya kuiimarisha zaidi, lakini hatimae wayakubali na kuyaidhinisha makisio hayo bila ya pingamizi. Baada ya kutamka hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, naomba nichukue muda mchache kutoa maoni ya wananchi wa Jimbo la Koani. Mhe. Spika, tunampongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake hasa na kazi zake, watu wa Jimbo la Koani tunamjua Mhe. Waziri amefanya kazi nzuri sana na tunamuombea dua anamaliza kazi zake vizuri Mwenyezi Mungu amjalie arejee tena katika wizara hii katika kipindi kijacho.
Mhe. Spika, katika kazi tulizozitaja Mhe. Spika, upande wa Mahakama tunaomba wazee wa Mabaraza zile posho wanazopewa ni ndogo, hivyo hizo pesa tulikuwa tunaomba ziongezwe na pia zipatikane kwa wakati. Kuna baadhi ya wengine tangu mwaka 2009 hadi hii leo bado mtu hajapata fedha zake. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naiomba Idara ya Mahakama zile pesa kwanza waziongoze na pia ziweze kupatikana kwa wakati.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba kuna tatizo la kesi ndogo ndogo hasa za madai kwenye Mahakama za mwanzo hucheleweshwa sana kwa kupigwa tarehe. Mhe. Spika, hili bado ni tatizo. Kwa hivyo, hili nalo ni tatizo jengine sugu.

Mhe. Spika, Ijumaa iliyopita tumesali msikiti huu hapa hatibu wa siku hiyo hakunipa raha katika sala yangu kwa sababu Mwenyezi Mungu ameumba siku saba katika wiki lakini Ijumaa ni siku tukufu na ni bora. Mhe. Spika, utukufu wake umewekwa kwa siku hiyo ni kutokana na ile sala ya Ijumaa, na sala ya Ijumaa imepewa utukufu kwa sababu ya hotuba ambayo wanapewa waumini kama ni muongozo wa siku zote saba. Kwa hivyo, hotuba ile inatakiwa iwe ni ya makini, muongozo ili iwe ndio kielelezo katika siku zao saba.

Mhe. Spika, hatibu wa siku hiyo alitamka kuwa Afisi yetu ya Baraza la Wawakilishi tumeletewa msaada ambao utakiuka maadili ya dini unaohusiana na haki za watoto. Jambo hilo ni baya kabisa lisifanywe na watakaofanya kazi hiyo watahukumiwa yeye anajitoa kabisa. Mhe. Spika, hatibu wa siku hiyo alisema mengi lakini muhtasari wa hotuba hiyo ilikuwa haina mantiki ya kutosha wala ukweli na ilikuwa na mambo mengi ya dhana.

Mhe. Spika, ni kwamba sisi hatujaletewa msaada unaohusu haki hiyo, hata katika vikao vya *briefing* hujatueleza kwamba serikali ina nia ya kutuletea msaada huo au umeshatayarishwa tujitayarishe. Hilo ni jambo la dhana. Kwa hivyo, nimeogopa waumini au wenzetu waislamu ambao tumewapa nguzo ya dini kutuongoza sio vizuri kutoa kauli za dhana hili jambo baya. Kwa hivyo, Afisi ya Mufti ifuatilie jambo hili.

Kwa hivyo, mimi nawashauri maimamu wetu kuna mambo mengi katika nchi yetu hivi sasa ambayo yanatakiwa kuyafanya, watu wavivu sasa hivi hawataki kufanya kazi, watoto wezi huko, haya ndio mambo ya kuweza kuyaendeleza. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nimemsamehe na Mwenyezi Mungu namuomba amsamehe lakini tuhakikishe katika hotuba zetu ziwe zinatolewa bila ya jazba na zenye muongozo na kuweza kuleta mstakbal mzuri wa dini yetu.

Mhe. Spika, namuombea kheri Rais wetu anayemaliza muda wake kwani ametuongoza miaka 10 vizuri na anamaliza kwa salama Mwenyezi Mungu amjaalie kheri na maisha mazuri tunayokwenda. Pia niwapongeze na niwaombee dua wale wote waliojitokeza kumrithi nafasi yake na ni vyema niwataje:-

1. Maalim Seif Sharif Hamad wa Chama cha CUF
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha
3. Ndg. Ali Abeid Karume
4. Mhe. Ali Juma Shamuhuna

5. Ndg. Bakar Hamad Mshindo
6. Ndg. Mohd Gharib Bilali
7. Mhe. Ali Moh'd Shein
8. Mhe. Moh'd Aboud Moh'd
9. Mhe. Haroun Ali Suleiman
10. Ndg. Moh'd Raza
11. Ndg. Moh'd Yussuf Mshamba

Mhe. Spika, hawa wote namuomba Mwenyezi Mungu awakubalie dua zao na awape mahitaji yao. Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hotuba hii, ahsante sana.

**Mhe. Zahra Ali Hamad (Kny: Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora):** Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa Kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha maoni ya kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Katiba na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Pia nakushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii adhimu na nakuahidi nitafuata mwongozo wako uliotupa wa kutumia muda mfupi.
Mhe. Spika, pia naomba kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Mkanyageni kwa mashirikiano wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu.

**MAFANIKIO:**

Mheshimiwa Spika, wizara hii ambayo inashughulikia suala mtambuka la utawala bora katika kipindi cha miaka mitano iliopita imepata mafanikio mengi yakiwemo yafuatayo:-

a) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wengi katika idara na taasisi zake zote;
b) Imetoa kitabu kizuri cha muongozo wa haki za binadamu;
c) Imefanikiwa kuchapisha na kusambaza vitabu vingi vya sheria za Zanzibar;
d) Imetayarisha Sera ya Jumuiya zisizo za Kiserikali;
e) Imeiruhusu Tume ya Haki za Binadamu ya Jamhuri ya Muungano kufanya kazi Zanzibar;
f) Imefanikiwa angalau kwa kiwango kidogo kukuza uelewa wa dhana hii ya utawala bora katika taasisi za Serikali na umma kwa ujumla;
g) Imefanikiwa kupunguza utawala wa mabavu kwa vyombo Serikali;
h) Imefanikiwa kupunguza tatizo sugu la wananchi kubuniwa kesi na kuwekwa ndani ovyo bila kupelekwa Mahkamani;

i) Imeleta mwamko kwa wasanii nchini kujua haki zao na sasa wamefanikiwa kugawana mirahaba na watumiaji wa sanaa zao; na

j) Imefanikiwa kuwasilisha ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati muafaka na kadhalika.

**MATATIZO/CHANGAMOTO:**

Mhe. Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *APRM* Tanzania iliyowasiliswa katika semina ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi iliyofanyika tarehe (16 November 2009) katika Hoteli ya Fisherman Resort. Utawala bora nchini umekabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo zifuatazo:-

(a) Sheria zinazo wanyima wananchi haki zao za msingi (*basic rights*);
(b) Wanachi wa kawaida sio rahisi kupata haki;
(c) Tume za Uchaguzi yani (*NEC* na *ZEC*) sio vyombo huru;
(d) Tabia ya chombo cha kutunga sheria na serikali kuweka sheria zinazo punguza madaraka ya mahakama;
(e) Matumizi mabaya ya dola kwa baadhi ya watendaji wa serikali;
(f) Mwingiliano (*Fusion*) kati ya Serikali na chombo cha kutunga sheria;
(g) Kiwango cha chini cha uwajibikaji, ufisadi na wizi wa mali ya umma. Watendaji katika utumishi wa umma ni wagumu kubadilika wana mawazo mgando;
(h) Uwajibikaji na uwazi katika serikali za mtaa uko katika kiwango cha chini sana;
(i) Serikali kuu ina tabia ya kuingilia shughuli za Serikali za mitaa.
(j) Hakuna uwazi katika mikataba yenye maslahi na taifa;
(k) Hapana Mahkama ya kikatiba licha ya ibara ya (125) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kuruhusu jambo hilo; na
(l) Hapana mamlaka ya kupambana na ufisadi na kusimamia maadili ya viongozi.

**MAHAKAMA**

Mhe. Spika, naupongeza muhimili wa Mahakama kwa kulikarabati jengo la Mahakama Kuu Vuga ingawa bado halijafikia hatua ya kuvutia machoni mwa watu. Vile vile napongeza hatua ya ujenzi wa Mahakama ya Mkoa iliyopo Mwera. Naiomba Serikali iuwezeshe muhimili wa Mahakama ili iweze kuyakarabati majengo yake yote Unguja na Pemba. Aidha, kambi yetu imefarijika kwa maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la Mahkama Wilaya ya Mkoani.

Mhe. Spika, katika hotuba yetu ya mwaka jana tulieleza tatizo la kucheleweshwa kutolewa uamuzi wa kesi katika Mahkama zetu. Pamoja na

ahadi nzuri tuliyopewa na Mhe. Waziri bado hali haijabadilika. Katika kipindi cha Julai (2009) hadi Machi (2010) jumla ya kesi (5,472) zilizofunguliwa katika Mahakama za Unguja na Pemba ni kesi (2,195) tu sawa na asilimia (40) ndizo zilizotolewa maamuzi. Je, huku si kucheza na haki za wananchi?

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana niligusia juu ya mishahara midogo ya mahakimu. Hali hii bado ipo na inawakatisha tamaa Mahakimu. Vile vile niligusia juu ya suala la mfanyakazi mmoja anayefanya kazi katika Afisi ya Mrajis Mkuu mwenye diploma tu ya sheria lakini anapata mshahara mkubwa kuliko Mahakimu ambao wana shahada za sheria za Chuo Kikuu. Tokea nilipotoa kauli hiyo mwaka jana hakuna marekebisho yoyote yaliyofanyika.

Mhe. Spika, matatizo katika Mahkama ya Kadhi bado yako vilevile kama nilivyoeleza mwaka jana. Bado mishahara yao haijaongezwa na wala hawajapatiwa utaalamu wa kuendesha shughuli zao.

Mhe. Spika, katika usikilizaji wa kesi Mahakimu hawana utaalamu wa uandikaji wa mwenendo wa kesi wala hukumu. Sheria wanazotakiwa wazifuate ni ngumu kwa wao. kifungu cha 9 (2) cha sheria ya Mahakama ya Kadhi kinawaelekeza Makadhi watumie *(civil procedure decree*) wakati elimu zao haziwawezeshi kuifahamu sheria hii ambayo chimbuko lake ni (*common law*).

Mhe. Spika, wakati umefika sasa wa kuachana na ajira za Makadhi ambao elimu zao ni ndogo. Ni vyema Idara ya Mahakama ya Kadhi ikaajiri wahitimu waliosoma katika Vyuo Vikuu vya Kiislamu ambao wataweza kuzimudu kazi hizi.

Mhe. Spika, Serikali kwa nia njema imeanzisha Mahakama ya Ardhi. Kwa upande wa Unguja Mahakama hiyo ipo Mji Mkongwe na kwa upande wa Pemba iko katika mji wa Chake Chake. Hali hii inaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaotoka vijijini. Naishauri serikali ianzishe Mahakama ya Ardhi katika kila Mkoa ili kuwapunguzia shida wananchi.

**Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana**

Mhe. Spika, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inalalamikiwa sana na wapangaji wake ambao hukubaliana wazifanyie matengenezo nyumba wanazo ishi kwa gharama zao na baadae watakatizana gharama wakati wa ulipaji wa kodi.

Mhe. Spika, baada ya wapangaji kuzifanyia matengenezo nyumba hizo, Kamisheni huwageuka na kuwataka walipe kodi kamili. Je, mashekhe hii si dhulma?

Mhe. Spika, kuna kilio cha Jumuiya ya Mabohora kunyanganywa nyumba yao iliopo Chachani Chake Chake ambayo inatumiwa kama ghala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wenyewe wamechoka kudai lakini hawapewi. Je, mashekhe hamuuogopi Moto Mkali wa Jahannam?

Mhe. Spika, naomba maelezo juu ya nyumba zilizojengwa na Kamisheni ya Wakfu huko Mbweni. Mtaji wa ujenzi huo umetoka wapi? Mmiliki wa nyumba hizo atakuwa nani? Zimekusudiwa kutumika kwa shughuli gani?

**Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali kuna kilio cha muda mrefu cha Wanasheria wa Serikali cha mishahara duni. Hali hii imepelekea wanasheria wengi wenye uzoefu kuhama na kutafuta maslahi upande mwengine.

Tatizo jengine lililopo katika afisi hii ni kutozingatiwa *seniority* katika upandishaji wa vyeo. Tatizo hili nalo kwa kiasi kikubwa limechangia wanasheria wazoefu kuihama afisi na kutafuta maslahi sehemu nyengine.

Mhe. Spika, Tume ya Kuchunguza Sheria imeshafariki dunia. Haina mwenyekiti, Makamishna, hapana lolote linalofanyika. Kutokana na umbwe hii zimejitokeza baadhi ya *NGOs* kujaribu kuzifanyia mapitio baadhi ya sheria za zamani, lakini wanapopeleka rasimu za Miswaada hiyo katika wizara zinazohusika hukwama.

**Afisi ya Mrajisi Mkuu**

Mhe. Spika, jengo la Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ni la zamani sana na halifai tena kutumika kwa ajili ya afisi nyeti kama hii. Kambi ya Upinzani inaishauri serikali impatie Mrajis jengo jipya la afisi lenye hadhi.

Kambi ya Upinzani pamoja na kumuombea Mrajisi Mkuu wa Serikali jengo jipya lenye hadhi, lakini haturidhishwi na mwenendo mchafu wa kupewa watu wasiohusika vyeti vya kuzaliwa vikionesha kwamba ni Wazanzibari wakati sio Wazanzibari.

Kilio chetu cha pili ni utolewaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa vijana walio chini ya umri wa miaka (18) ili wapate fursa ya kupata vitambulisho vya Uzanzibari Ukaazi na hatimaye waweze kuandikiswa katika Daftari la Wapiga Kura.

Mhe. Spika, Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali Pemba haina uwezo wowote zaidi ya kutoa nyaraka za nyumba tu. Shughuli zote zimehodhiwa Afisi ya Mrajisi Unguja. Kambi ya Upinzani inashauri afisi ijengewe uwezo ili shughuli zote zinazofanywa Unguja ziweze pia kufanywa Pemba ili kuwapunguzia shida wananchi.

**Afisi Ya Mkurugenzi Wa Mashtaka**

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inaipongeza Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua iliochukua ya kujenga jengo la kisasa na pia kuanzisha Maktaba ya kisasa. Vile vile tunaipongeza afisi hii kwa kuanzisha jarida la SHAHIDI ambalo linaelimisha umma juu ya makosa na mambo mbali mbali ya jinai.

Kambi ya upinzani hairidhishwi na kasi ndogo ya kupeleka waendesha mashtaka katika Mahakama za Wilaya. Kuendelea kutumia polisi katika kuendesha kesi kunadumaza shabaha njema ya kuwatendea haki raia mahakamani. Tunaishauri Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika mwaka huu wa fedha wilaya zote zipatiwe waendesha mashtaka wa kiraia na polisi waendelee na shughuli zao za upelelezi tu.

**Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inatoa pongezi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kukamilisha ripoti ya mwaka (2008/2009). Vile vile tunapongeza kwa kuyapitia kwa haraka majalada ya wastaafu ili wapate mafao yao kwa wakati mwafaka. Hii ni hatua nzuri na lazima ipongezwe.

Kwa kuwa jukumu la afisi hii linafanana sana na jukumu la Baraza la Wawakilishi, tunarudia kupendekeza afisi hii ni vyema ingekua chini ya muhimili wa Baraza kuliko kubaki serikalini kama ilivyo sasa.

Katika nchi nyengine Mdhibiti hutoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari juu ya ukaguzi uliofanywa. Tunaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu iige mfano huo nzuri ili wananchi waelewe uwajibikaji katika utunzaji wa fedha na mali ya umma ulivyo katika serikali yao.

Mhe. Spika, shughuli za ukaguzi bado hazijazingatia kiwango cha kimataifa cha ukaguzi. Tunashauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu iharakishe kulishughulikia tatizo hili.

Kambi ya upinzani inashauri wafanyakazi waliopo afisi ya Pemba wasisahauliwe wakati zinapotokea fursa za ziara za nje ya nchi. Uzoefu unaonesha kwamba ziara zote za nje wanakwenda ni wafanyakazi wa afisi ya Unguja tu.

**Mamlaka ya Kupambana na Rushwa**

Mhe. Spika, kama kambi yetu ya upinzani ilivyokuwa inafikiria, matumaini ya kuundwa kwa mamlaka ya rushwa na maadili ya viongozi yametoweka kabisa. Katika hotuba za bajeti za miaka iliyopita suala hili lilikuwa angalau linatajwa na kuekewa malengo ya utekelezaji.

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka huu tunapewa hadithi mpya kwamba masuala ya rushwa yatasimamiwa na sheria ya mwenendo wa jinai. Pamoja na *APRM* Tanzania katika ripoti yake ya 2009 kubainisha kwamba ufisadi upo katika kiwango cha juu na kupendekeza Zanzibari ianzishe mamlaka ya kupambana na ruswa serikali imeamua kuachana na mpango huu.

Mhe. Spika, napenda kulishawishi Baraza lako tukufu lisiidhinishe shilingi 13,000,41,000 ambazo zimeombwa kwa ajili ya mamlaka ya kupambana na rushwa na kusimamia maadili ya viongozi kwa vile hapana tena azma ya kuundwa mamlaka hiyo.

**Ofisi ya Mufti**

Mhe. Spika, kambi ya upinzani inaipongeza Afisi ya Mufti kwa kujenga jengo jipya la afisi yake kwa msaada kutoka serikali ya Oman.
Zanzibar inakabiliwa na migogoro miwili ya kidini ambayo inahitaji kudhibitiwa mapema. Mgogoro wa kwanza unahusu ongezeko kubwa la mabaa yaliyozagaa ovyo katika Manispaa ya Zanzibar. Baa zilizofikishwa mahakamani kwa ajili ya pingamizi ili zipatiwe leseni ni 173 ambapo 10 kati yao zilinyimwa leseni lakini hata hivyo, zinaendelea na biashara bila ya leseni na serikali imeufumbia macho mgogoro huo.

Mhe. Spika, mgogoro wa pili unahusu rasimu ya Mswaada wa Sheria ya Mtoto 2010. Rasimu hii inapingwa na Waisilamu kwani kwa kiasi kikubwa inapingana na imani ya dini hii. Kambi ya upinzani inashauri Afisi ya Mufti ichukue hatua mapema kushughulikia migogoro hii kabla haijaleta maafa katika nchi.

Mwisho Mhe. Spika, nawashukuru waheshimiwa wote kwa kunisikiliza kwa makini na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazrui:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuzungumza katika kuchangia hotuba nzuri ya Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri, fupi na inayoeleweka. Ahsante sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni mdogo sana katika hotuba hii na nitaanzia na ukurasa wa 5 ambao unaelezea habari ya utawala bora katika biashara.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika ukurasa huu kwamba, Baraza la Biashara limeanzishwa na kwa kweli hili ni suala muhimu katika nchi ambazo zinataka kuendesha biashara huru na biashara ambayo kuwa kama ni kitovu cha uchumi cha nchi hiyo. Kwa hivyo, Baraza la Biashara limeanzishwa na hii ni hatua nzuri ya kujivunia.

Kwa sababu wafanyabiashara wengi watapata fursa ya kutoa michango yao moja kwa moja kusikilizwa na viongozi wakuu wa serikali kama Rais wa Zanzibar akiwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza hili. Kwa hivyo, mimi kwa moyo mkunjufu kabisa naomba kupongeza hatua hii na nasema kwamba, tuendelee mbele tusirudi nyuma.

Lakini jengine ambao nataka kulisisitiza liko ukurasa wa 10 suala la Mahakama ya Biashara. Mhe. Spika, Mahakama ya Biashara imekuwa ni hadithi ya muda mrefu sana. Kwa vile tumeweka tangu mwaka 1984 tumeamua Zanzibar kuwa na biashara huru, vile vile katika kipindi cha muda mrefu sana tumetoa nafasi wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi kuja kuwekeza katika nchi yetu. Bado Mahakama ya Biashara haipo nchini kwa hivyo, wawekezaji wanapotatizana katika mambo ya biashara wote wanakuwa katika kapu moja kwenye sehemu ya Mahakama ya kawaida.

Tatizo hili kwa kweli linaleta usumbufu mkubwa sana hasa kwa wale wafanyabiashara wa nje ambao hawajazowea habari hizi, wao wamezowea kwamba matatizo ya kibiashara yanatatuliwa katika Mahkama za Kibiashara. Ingawaje Mhe. Waziri katika hotuba yake hapa kaeleza kwamba kuna jengo katika Mahkama ya Vuga na vile vile kuna jengo la Maktaba Kongwe iliyohamwa, ile itafanywa kuwa ni Mahakama ya Biashara. Lakini bado hajatuelezea hii Mahakama ya Biashara hasa itaanzishwa lini? Kwa sababu hiki ndio kilio kikubwa cha wafanyabiashara na wawekezaji katika nchi hii.

Ningemuomba Mhe. Waziri atupe taarifa rasmi ili wafanyabiashara pamoja na wawekezaji wapate kuona kwamba hili jambo mwaka huu linafanikiwa.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 9 imeelezwa kwamba katika changamoto ambazo zinakabili wizara yake ni tatizo la rushwa na nidhamu katika sekta ya umma hairidhishi na kwa hivyo, hukosekana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma. Tatizo la rushwa Mhe. Spika, ukiliangalia kwa kweli katika nchi yetu limejificha sana, kama ni jambo la aibu kwa hivyo, halitangazwi tangazwi. Lakini lipo na linaathiri ndani kwa ndani na linateketeza uchumi wa nchi hii. Lakini jambo hili kulifumbia macho na kulidharau huenda likatumaliza kama vile linavyoendelea Tanzania Bara.

Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha hapa atueleze kiunaga ubaga ni hatua gani kwa sababu hii ndio wizara yake itakayochukua kuona kwamba angalau taasisi madhubuti ambayo itaweza kukabiliana na haya masuala ya rushwa na ufisadi. Ufisadi hasa umeingia katika masuala ya kutoa huduma katika masuala ya siasa na sehemu mbali mbali. Vipi tutaweza kuyakabili, tukiyaachia haya yakiendelea yatazidi kutuathiri na huenda yakatuletea matatizo makubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 9 utekelezaji wa jumla kazi za wizara kwa mwaka 2009/2010 ulikwenda kama ifuatavyo, majukumu yake. Ukija ukurasa wa 10 Mhe. Waziri kaonesha kwamba katika kipengele cha nne kukamilika kwa ujenzi wa Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali huko Pemba.

Mimi sijaiona, hii afisi iko wapi ya Mrajis Mkuu iliyojengwa mpya? Mhe. Waziri ananambia Wete. Mimi najua pana kiwanja kitupu hakina jengo. Ahsante kwa hivyo, suala hili nitalifuta madhali kalijibu haraka haraka.

Katika ukurasa wa 10 kazi ya kuimarisha mazingira ya biashara inahusisha marekebisho ya sheria usajili wa biashara, usajili wa rehani na sheria ya ufilisi imefikia hatua ya mwisho baada ya kukabidhiwa rasimu ya ripoti ya mwisho kwa mapitio. Kwa kweli hili vile vile ni suala nyeti sana ambalo wafanyabiashara wanalingojea kwa muda mrefu. Mhe. Waziri umeeleza vizuri sana lakini je, ni lini suala hili litamalizika ili ianze kazi zake na wafanyabiashara nao wapate kuridhika na masuala haya.
Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kutueleza hapa ningeomba suala hili utubainishie ili wafanyabiashara nao wapate kufahamu hali halisi ilivyo.
Mhe. Spika, tukienda katika suala la Mahalama, *Alhamdulillah* Mahakama zinajengwa na Mahakama ya Vuga imetengenezwa, lakini hizini sehemu muhimu sana za kushughulikiwa. Ni sehemu ambayo kila siku wageni

wanaingia na kutoka, Mahakama zetu zinang'ara pale tu zinapopigwa rangi kwa muda wa miezi mitatu mpaka sita, lakini ikitoka hapo Mhe. Waziri nasikitika kwamba Mahakama zetu ni chafu na wafanyakazi wapo wanalipwa mishahara kusafisha hizi sehemu, lakini hazisafishwi. Mahakama zetu hazipendezi ukiangalia majaji wamependeza, wanasheria makoti yao mazuri na suti kubwa kubwa, lakini Mahakama hazipendezi kabisa kutokana na hali ya uchafu.

Kweli ni masikini hatuna kitu, lakini umaridadi unaondosha umasikini. Yaani ukiwa maridadi unaficha uchafu. Kwa hivyo, ningeomba tujitahidi kama inawezekana Mahakama zetu ziwe safi kabisa kama Mahakama nyengine. Mahakama zetu kwa kweli haziridhishi kutokana na masuala ya usafi.

Jengine Mhe. Spika, Mahakama zetu kwa mfano Mahakama ya Vuga ni Mahakama ambayo ilijengwa tangu wakati huo *population* ya Wazanzibari ilikuwa chini ya watu laki tatu, leo tuko watu milioni moja, laki mbili na ushei Mahakama hii inataka *extension*. Kwa keli haikidhi tena haja. *Furniture* zake zimekuwa kongwe, zimechoka, jengo lenyewe limechoka na halitoshi ni finyu sana. Ningemuomba Mhe. Waziri angalau atuoneshe katika *vision*, hiyo *Vision 2020* au *Vision 2030*, lini Serikali ya Zanzibar imewekeza kujenga Mahakama mpya ambayo itakuwa na vigezo vyote vya Mahakama zinazotakiwa.

Mhe. Spika, naomba kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na idara yake hii ya Mrajis. Kwa kweli wanasema watu sina hakika, lakini nawasikia wengi wanasema kwa Afrika nzima ukiacha Misri basi ya pili ni Zanzibar katika uwekaji wa kumbukumbu za wananchi za vifo, nyaraka za mashamba, za kuzaliwa. Wanasema kwamba ukitoka Misri kwa Afrika ni Zanzibar kwa muda mrefu sana kihistoria wana kumbukumbu za muda mrefu zaidi kuliko nchi nyengine zote.

Humu Mhe. Waziri kaandika kwamba wamekwenda Dar es Salaam kubadilishana mawazo na *RITA* hiyo *RITA* imeanza hivi miaka ya karibuni. Lakini urajisi wa Zanzibar umeanza miaka mingi sana na katika historia ya Afrika Zanzibar ni nambari mbili. Kwa hivyo, ili kuweka heshima hii izidi kung'ara na kuendelea ningeomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri aone kwamba upo umuhimu wa kuipa hadhi yake ile ofisi. Ofisi imekuwa finyu, jengo lina unyevuunyevu mwingi sana ambao unapelekea karatasi nyingi kuharibika na vyombo vyengine kuharibika. Kwa kweli jengo kama lile kukaa karibu na pwani ni hasara kubwa sana, ma-*document* mengi sana yanaathirika na unyevuunyevu na hawana ghala la kuhifadhia ma-*document* ili yasiharibike.
Mhe. Spika, siku moja nilikwenda kuonana na bwana mmoja yeye anahifadhi *document* za zamani kule Dubai. Nikaona ameweka mafriza na *document* zake zote anatoa katika friza anaota nje anafungua ndio tunasoma. Nikashangaa,

nikasema mpaka hizi *document* pia yanatiwa humu? Akasema *document* kuna njia mbali mbali za kuhifadhi. Kwa hivyo, kwa bahati mbaya pale kwetu sisi mabuku mengine yanatolewa yamechanikachanika karatasi zinakatika vipande vipande kweli hali kama hii hairidhi.

Mhe. Spika, naasema tena kwamba, sifa za nyaraka Zanzibar ni kuwa zimehifadhiwa kwa muda mrefu na katika historia ya Afrika Zanzibar ni nambari mbili. Kwa hviyo, tusidharau tuipe kipaumbele afisi ile, tuipe zana, tuipatie ikiwezekana ofisi mpya ambayo itakuwa na kila aina ya vifaa ambavyo vitaweza kuhifadhi *document* zile. Siku hizi kunatumika mambo ya kompyuta na mambo mengine yangetumika zaidi ili tukaweza kufanya ofisi ya mrajis ikawa nzuri zaidi.

Mhe. Spika, natafuta nione kwa sababu tulipotembelea pale tulikuta Mkurugenzi wa idara ile gari hana anatembea kwa miguu. Zamani tulipokuwa tukienda pale Wazungu wanakuja wanataka kwenda kusajili kampuni zao wakifika wanaona kwamba pengine katika *documentation* na nini wanaambiwa lipeni shilingi 11 milioni, likija lile faili ambalo linahifadhi zile *document* la shilingi mia tatu. Kwa hivyo, mtu anashituka ah, hili faili la shilingi mia tatu mimi nalipa shilingi 11 milioni *documentation*. Lakini leo utakuta yule Mkurugenzi wa idara ile anakwenda kwa miguu gari hakuna na sisi tunakwenda pale na *dump millions of money*. Kwa hivyo, ningeomba katika bajeti hii niangalie je, Mkurugenzi huyu kapatiwa gari?

Jengine Mhe. Spika, ningeomba idara hii iangaliwe zaidi kwa sababu wageni wengi wanaokwenda pale wanakwenda ku-*register trade marks*, kampuni na kufanya maboresho ya kila mwaka na ku-*submit* zile ripoti za kila mwaka. Kwa hivyo basi, iboreshwe ili kukidhi haja ya kuwa kweli ni pahala pa urajisi wa *investors* sio kama kurajisi kampuni yangu mimi au mtu mwengine. Lakini wanakuja *investors* kutoka nchi za nje wanakwenda pale hivyo lile jengo liwe na hadhi.

Kama tulivyolipa hadhi jengo la *ZIPA* tukahama Mji Mkongwe tukawajengewa kule Maruhubi, basi na hawa vile vile nao walikuwa wapewe kwa sababu *investors* wengi sana wanatembelea jingo hili na wageni wanakuja kusajili *trade mark* zao. Kwa hivyo, nahisi ipo haja ya kuboresha jengo lile na kuboresha elimu ya wale wafanyakazi katika idara ile.

Mhe. Spika, vile vile nataka nimpongeze waziri kutokana na hii Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mimi niko kwenye Kamati ya *PAC* na ripoti zake Mhe. Spika, tunazipitia na ni nzuri. Kwa hivyo, naomba wapelekewe kila aina ya msaada na *motivation* ya hali ya juu ili wazidi kufanya kazi zao vizuri.

Vile vile nampongeza kwa Afisi ya *DPP* ni nzuri na kazi yake *Alhamdulillah.* Akiendelea hivi, akipandisha *speed,* nafikiri tutakuwa *number one*. Kwa hayo machache Mhe. Spika, ningeomba nimalizie hapa na niwashukuru wenzangu wote kwa kunisikiliza ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Nassor Mazrui kwa mchango wako huo ingawa kuna majibu mengine umeshayapata hapa hapa, huu ni utaratibu mpya kabisa. Kwa sababu ukimtizama Mhe. Waziri basi anakupa jibu hapo hapo. (*Kicheko*)

**Mhe. Zakiya Omar Juma:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi za mwanzo mwanzo kuwa mchangiaji katika Wizara hii ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kama wenzangu na mimi baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kitabu chake kizuri na hotuba yake vile vile pamoja na utaratibu wa uwasilishaji ambao alikuwa ametuwasilishia katika Baraza hili.

Mhe. Spika, sina mchango mrefu sana lakini nina mawili matatu ambayo ninataka na mimi nipate faida pengine na wenzangu ikiwezekana hata mwenyewe Mhe. Waziri na yeye labda inaweza ikaleta faida ya hapa na pale.

Mhe. Spika, napenda nianze katika ukurasa wa 22 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kifungu cha 54. Kifungu kinasema, pamoja na shughuli nyengine afisi imepokea majalada 260 kutoka polisi kuhusiana na makosa mbali mbali ya kiwemo taarifa za kifo, shambulio, wizi, ubakaji na kutoroshwa. Sasa mimi suala langu ninalotaka kulifahamu zaidi liko katika kipengele cha kutoroshwa na suala zima la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, ni juzi tu, hukuwepo lakini taarifa utakuwa unazo kwamba tuliwasilishiwa taarifa ya mtoto katika Baraza. Miongoni mwa maelezo ambayo yamo mle ni miongoni mwa haki ambazo anatakiwa mtoto kupata au anastahiki ni pamoja na haki ya kulindwa. Zilipokuja hizi taarifa za kutoroshwa hapa kwamba kuna kesi tatu hizi, napenda nijue kuna kesi moja ambayo Mhe. Spika, ilikuwa maarufu katika Baraza lako lakini imenyamazwa kwa muda mrefu.

Kwa sababu kuna taarifa hii ningependa nijue katika hizi kesi za kutoroshwa kuna mtoto Maryam Farid alitoroshwa mwaka 2006 na mpaka leo kama Baraza ni hili chombo kikubwa tungependa kujua nini kimeendelea kwa mtoto yule, hatujui taarifa zozote. Sijui katika kesi hizi tatu na kesi hii imo na kama haimo labda imefikia wapi habari hii mpaka leo hatujui mtoto wetu kaishia wapi.

Sasa kwa sababu hii ni haki ya huyu mtoto kama raia wa nchi hii lakini sijui utaratibu unakwendakwenda vipi, lakini katika mikataba ambayo tunasaini kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar tukiwa tunahusika, sijui utaratibu unakwendaje jinsi ya kuwa watoto wanatakiwa kulindwa na kama wanapata mashaka kama haya ya kutoroshwa inakuwa vipi mpaka tunawesa kupata haki ya mtoto huyu. Sijui ni nchi yenyewe husika inatakiwa kufanya hivyo au kwa sababu tumesaini mikataba ya kimataifa, mataifa yanahusikaje kuhakikisha wanatuletea mtoto wetu. Hili limenirudisha kule mwaka 2006 Mhe. Spika, na ningependa kujua hatiuma ya utoroshwaji wa mtoto huyu.

Lakini pia nilitaka kujua habari ya kesi za madawa ya kulevya ambazo ziko kesi 61. Mhe. Spika, juzi wakati nakuja katika Baraza nilipita njia ya katikati Kisimamajongoo. Katika jambo ambalo limenihudhunisha sana ni wale watu ambao nilipishana nao aidha wanatembea au wamekaa kitako. Asilimia kubwa ni watoto wetu vijana, vdugu zetu, kwa kweli haihitaji tochi, unaemuona anakupita unajua hiyo kesi ni unga. Sasa kwa kuwa hapa pana hizi kesi 61 nilitaka kujua vipi inaendelea kesi hii na labda na namna ya udhibiti ukoje. Kwa sababu hali bado ni mbaya sana.

Mhe. Spika, nataka nipate maelezo hapa kidogo na pengine labda kama ambavyo tulishauri katika hotuba zilizopita kuwa sasa mkazo uwekwe katika hawa watu wanaoleta na hata wanaouza. Kwa sababu kama itakuwa haipo kidogo itakuwa mashaka kupata, lakini kama kitu kipo, biashara inaendelea na hatujui mambo yanakwenda kwendaje kidogo inakuwa ni matatizo sana kwa vijana wetu ambao itakuwa ndio nguvu kazi ya taifa hili. Tutakapokuwa sisi tumeondoka tunatarajia wao ndio waendeleze hili gurudumu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka nizungumzie katika Afisi ya Mufti na hapa nianzie katika kifungu hiki cha 80 ukurasa wa 31 kinachozungumzia kwamba jukumu kubwa la hii ofisi miongoni mwa majukumu yake ni kutatua migogoro mbali mbali ya kidini kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Hapa Mhe. Spika, nilitarajia nikiendelea kumsikiliza Mhe. Waziri au nitakapoendelea kusoma hiki kitabu nikute na mambo mengine. Kama Mhe. Waziri Kivuli alivyosema ni kwamba kuna kesi mbili kubwa hapa ambazo zinahitaji kupata ufumbuzi wa haraka kabla hali haijawa mbaya zaidi, nalo ni ongezeko kubwa la mabaa katika mji wetu. Jambo ambalo hata mashekhe wanasema kwamba “Ulevi ndio mama wa maasi”. Ukishalewa tena utafanya kila kitu.

Lakini ukiacha mabaa kuna biashara ya ukahaba ambayo kwa kweli haileti picha nzuri kwa nchi yetu. Hata kama ni jambo ambalo linasemwa lilikuwa likifanywa au linaendelea kufanywa basi ilikuwa kuna heshima. Ukisikiliza hadithi za wazee wanapozungumza vitu kama hivi basi ilikuwa kila jambo linafanywa kwa stara pamoja na kwamba ni jambo ambalo kidini na kijamii halikubaliki lakini sasa likifanywa katika hali ya ustaarabu mkubwa.

Mhe. Spika, leo tunajionea hali ilivyokuwa mbaya katika majia ya mji wetu, inafika pahala njia nyengine inabidi wazee au baadhi ya watu ambao wana heshima zao wanaacha kupita njia fulani fulani inapokuwa jua linazama hakupitiki. Sasa hii afisi nadhani hili pia ni jukumu ambalo labda Mhe. Waziri atakapokuja hapa angelitueleza basi ni hatua zipi tunachukua. Kwa sababu pamoja na mambo ambayo yanafanyika katika shughuli hii ni jambo ambalo limepigwa vita sana katika dini yetu.

Lakini ukiacha hilo Mhe. Spika, kuna suala zima la ukiukwaji mkubwa wa maadili. Hali si nzuri Mhe. Spika, wakati mwengine ni kivazi tu lakini jinsi kinavyokuwa kimevaliwa kinapelekea tena mkondo mzima kwenda ikawa hali inaharibika jambo ambalo nadhani Afisi hii ya Mufti ina jukumu na dhima ya kubeba katika hili. Kwa hiyo, tungeona basi jinsi gani Afisi ya Mufti inachukua nafasi yake.

Mhe. Spika, miaka miwili mitatu pengine iliyopita binafsi nimewahi kutoa kauli kwamba wakati wa Mhe. Mzee Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amrehemu yeye aliweka hasa utaratibu wa namna ya kivazi. Walikuwepo wale askari wanaoitwa valantia wakati ule sio valantia wa sasa hivi, wao walikuwa wakilishughulikia sana suala hili la kuwa watu wanavaa ovyo ovyo, wanakwenda uchi ilikuwa hili halikubaliki.

Hata wageni waliwekewa vitenge wanapoteremka ndege au wanaposhuka meli kama ni kitu cha kuweka stara kwa kuwa umeingia katika mji wa watu ambao na wao wenyewe wako katika hali hizo na wewe unatakiwa usiende kinyume na wao. Hili limeachwa kwa muda mrefu sijui tunakwenda na wakati, sijui kama ndio maendeleo. Lakini nadhani maendeleo makubwa zaidi ni kuchunga heshima ya nchi yetu, pia kuhakikisha kwamba hatuendi kinyume na yale mafundisho ambayo Mtume wetu Muhammad (SAW) ametuletea ambayo ni matakwa ya Mwenyezi Mungu mtukufu mwenyewe.

Hili ni jukumu ambalo nadhani bado Afisi hii ya Mufti ina dhima ya kubeba na tungependa kusikia kauli kutoka kwa Mhe. Waziri kuhusiana na suala zima la hali hii ya kuporomoka kwa maadili kwa kiasi hiki.

Mhe. Spika, katika ukurasa huo huo nikiingia katika kipengele cha 82 kumeelezwa hapa suala la kuendeleza mashirikiano ya jumuia za kidini za nje na ndani ya nchi. Imeelezwa hapa nchi mbali mbali Misri, Iran na kadhalika.

Mhe. Spika, nimevutiwa wakati nikiangalia televisheni na muda mrefu huwa napenda kuangalia kipindi hicho ukiacha vipindi vyengine vya taarifa za habari na vipindi vya siasa ambavyo pia navipenda basi kuna *channel* inaitwa *Peace Television*. Hiyo ni *pure* mambo ya dini na inatoa maelezo mengi, ufafanuzi mkubwa wa shughuli nyingi na hii jina lake wanaita *Islamic Research Foundation*.

Mhe. Spika, napenda kujua kwa ile hamu ambayo napata kwa kusikiliza kipindi kile kama labda Afisi yetu hii ya Mufti kupitia Wizara yake kama labda ina mahusiano yoyote na wenzetu hawa. Kwa sababu kwa mujibu wao hata hivi juzi tu walikuwa wana safari ya kwenda Uingereza kuendeleza shughuli hii lakini kwa bahati mbaya wamezuiliwa viza na ninaifuatilia sijui mwisho wake itafikia wapi. Lakini huwa wanakwenda maeneo mbali mbali kwa ajili ya taaluma hizi na watu wanakuja pale kujifunza na kuna mafunzo mengi, kuanzia watoto, watu wazima wanaofuatilia kwa kusoma na kuslimu na vitu kama hivyo.

Sasa ningependa nipate maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri kama labda wanaifahamu hii taasisi na kama kuna namna yoyote ya kuwa na mahusiano nayo au vyenginevyo.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa ajili ya afisi yake hii Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli kazi waliyofanya Mhe. Spika, pamoja na kwamba mapungufu hayaachi lakini nazungumzia kazi ambayo imefanywa ni kazi kubwa, nzuri na ya kupigiwa mfano na kiasi kwamba sasa imefika inakwenda na wakati. Kwa sababu miaka ya nyuma labda miaka mitano mpaka kumi iliyopita tulikuwa tunaona ripoti inayowasilishwa katika chombo hiki au pengine katika maelezo ambayo yanakuja kwenye vitabu ilikuwa ni ya miaka kiasi mitatu minne nyuma lakini sasa hivi inakwenda na wakati kabisa.

Mhe. Spika, tumeelezwa hapa kwamba wameshamaliza ile ya mwaka 2008/2009 na wanataka kufanya ya mwaka 2009/2010 kwa hiyo ni suala la kupongezwa na ni hatua nzuri. Tungeomba waendelee na kasi hiyo hiyo na ari hiyo hiyo na wasirudi nyuma. Maana Mhe. Spika, Waswahili wanasema "Mgema akisifiwa tembo hulitia maji". Lakini nadhani kwa hili hawatofanya hivyo, wataendelea kufanya vizuri ili kila mwaka unapomalizika basi na ripoti yake inapatikana inafanyiwa kazi na tunakuwa tunakwenda kwa wakati na shughuli zinakwenda kama kawaida.

Mhe. Spika, nizungumze kidogo kuhusu suala la rushwa. Mhe. Spika, mimi naogopa kidogo au nina wasi wasi kwamba sasa suala la rushwa itafika pahala tutalitungia sheria ya kuona kwamba linahalalika. Wakati wa enzi za Mwalim Julius Kambarage Nyerere yeye alikuwa akisema kwamba "Rushwa ni adui wa haki" na ni kweli. Kwa sababu Waswahili wanasema "Penye uzia penyeza rupia". Sasa hiki ni kitendo cha rushwa, lakini unapofanya hivyo mwenye haki anakosa haki anapata asiye haki.

Mhe. Spika, kinachonishtua na kinachonitisha ni hili suala zima la rushwa kuwa sasa linatafutiwa namna na siajabu baadae Mwenyezi Mungu asitupeleke tukatunga na sheria ya kuhalalisha. Tumeanza kubadilisha maneno mara inaitwa takrima, mara wengine wanazungumza kwamba takrima sasa ni halali, ilimradi inazongwa zongwa hiyo takrima unaambiwa aaa maana yake ikiwa ni hivi basi hiyo si takrima. Sasa jinsi inavyoviringishwa viringishwa hii rushwa ikabadilishwa majina ikisha ukaambiwa ikiwa umetoa kiasi kidogo hiyo sio, ukitoa kingi ndio hivi, sijui wengine mamilioni wanayaita vijisenti, nina wasi wasi tutafika pahala tutaihalalisha rushwa.

Mhe. Spika, napenda nitahadharishe kwamba bado tuone kama rushwa ni adui wa haki kama ambavyo muasisi wa nchi hii Baba wa Taifa alivyoiacha na alivyokuwa akiichukia na kuikemea kila siku. Lakini pia tuone kwamba ni suala ambalo tunahitaji kulipiga vita kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, baada ya haya machache sina maneno mengi kwa suala hili la rushwa. Napenda nimalizie sasa mchango wangu kwa suala zima la ile Sheria ya Mtoto ambayo kwa bahati mbaya Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati alipokuwa akitoa ripoti yake na mchango wake aliona kitu tofauti na sisi wengine ambapo pengine tumepokea.

Mhe. Spika, suala la Sheria hii ya Mtoto ambayo mashekhe Ijumaa iliyopita nadhani takriban misikiti yote walipiga kelele ni kweli kwamba hiyo sheria haitufai. Mimi binafsi Mhe. Spika, nilishiriki ilipoletwa hiyo sheria kama kufanyiwa mapitio au vipi, lakini tuliwaeleza wahusika waliokuja pale kwa sababu walikuwepo wenyewe wazungu wale watu wa *UNICEF* kama sikosei walibadilika rangi kwa michango ambayo ilitoka pale.

Tuliwaambia kama hii sheria pamoja na yote ni lazima iendane na hali halisi ya nchi yetu ilivyo. Sisi ni waislam kiitikadi, kiutamaduni, desturi na kila kitu. Kuna mambo mengi ikiwemo na hadithi za Mtume Muhammad (SAW) kwamba ndani ya nyumba yenye watoto ni lazima kuwe na bakora na vitu kama hivi zilitolewa.

Haina maana kwamba mtoto apigwe lakini kuna vitu ambavyo kwa kweli kuvitoa tu tukakataa kama wanavyokataa mataifa ya magharibi wanavyopenda wao tutakuwa tunakwenda kinyume na maadili ya dini yetu, tunakwenda kinyume na maagizo ya Mtume wetu Muhammad (SAW). Lakini pia tutakuwa tunayakiuka yale ambayo Mwenyezi Mungu mtukufu ametaka sisi tuyafanye kwa ajili ya watoto wetu ili tuweze kupata watoto wema ambao baadae na wao watakuwa ni wazee wema kwa watoto wao.

Sasa Mhe. Spika, tusione kama mashekhe labda wamekosea au vipi. Ni kweli hii sheria haifai na tulisema sana siku hiyo na walitufahamu wale wazungu waliokuwepo pale. Maana kuna waliokuwa wakisikia na kuna waliokuwa hawasikii wakawa wanaelezwa wanafahamishwa kile ambacho tunakisema.

Mhe. Spika, mwisho nataka nimalizie kwa kusema kwamba sheria hii wala tusiifanyie masihara kwa sababu sisi ni waumini na uumini wetu kila mtu anaelewa. Hatukatai sheria hii lakini ni lazima iendane na maadili yetu kwanza, vyenginevyo irudi huko huko kwao na sisi tuachwe twende na maadili yetu kwa ajili ya hatima zetu tunakokwenda *inshaallah*. Mwenyezi Mungu atatupa salama na watoto wetu, nchi yetu na vizazi vyetu. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Mhe. Spika, naomba nianze kwa kuiunga mkono hoja. Naanza hivi kwa sababu hii wizara ina mashekhe wengi, kwa hiyo ukianza hivi huenda mambo huko mbele yakawa mazuri. Mhe. Spika, namshauri sana sahibu yangu Mhe. Ame Mati Wadi kwa sababu yeye mchakato hajaanza aanze na gia hii hii pengine watu wa Matemwe ikawa mambo mazuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nimeshtuka kidogo kusikia kama Zanzibar sasa tuna mabaa yanayofikia 173. Kwa kweli hii ni idadi kubwa kwa waislam asilimia zaidi ya 90 kwa Zanzibar. Maana yake ukipiga mahesabu kila wilaya tuna mabaa yanayozidi 17, sasa hii ni hatari kubwa kwa kweli. Mhe. Spika, ningemshauri Mhe. Waziri ashauriane na wengine kuona namna gani tunajaribu kuyapunguza. Kwa sababu sisi Zanzibar kama nilivyosema kwamba uislam si dini tu lakini pia ni utamaduni wetu. Sasa kuacha hali ikafika hivi na kama hakutakuwa na *regulatory organ* ya kudhibiti hii hali tutafika pahala kila baada ya nyumba mbili patakuwa na baa itakuwa mtihani mkubwa.

Mhe. Spika, jengine ni suala Mahkama. Mhe. Spika, kiambatanisho Nam. 6 (a) ukurasa wa 62 kesi za rufaa zilizokatwa mwaka jana ni 14, lakini ni 4 tu ambazo zimetolewa uamuzi, sasa hii kasi inaonekana si nzuri. Kwa hivyo, ningeomba mrengo huu wa Mahkama ijitahidi kidogo kuona kwamba

kunakuwa na kasi nzuri ya usikilizwaji wa kesi. Hata hizi nyengine ukiziangalia zinazofunguliwa na zinazotolewa uamuzi ile kasi yake kwa kweli hairidhishi sana. Ni kweli kumekuwa na mafanikio kidogo lakini tunahitaji kuongeza kasi zaidi.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba nilizungumze kidogo niipongeze sana Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli Mhe. Spika, inafanya kazi nzuri sana. Kazi nzuri ni kwamba sasa tunakaribia kwamba ile ripoti yao ya mwaka uliopita tuwe tunaijadili sasa hii ni hatua nzuri sana. Huko nyuma sisi kama Baraza tulikuwa tunazingatia ripoti ya miaka mitatu minne nyuma.

Lakini pongezi zaidi ni kwamba wamekuwa na mashirikiano mazuri na Kamati ya Baraza la Wawakilishi hii ya *PAC*. Sasa hili ni jambo la kupigiwa mfano kwa sababu sisi na wao tunafanya kazi pamoja. Kwa hiyo, vyombo viwili katika nchi kama havina mashirikiano mazuri katika suala hili tunaweza tukawa tunavutana, lakini bahati nzuri tumekuwa na mashirikiano mazuri.

Mhe. Spika, ila naomba jambo moja tu walitilie mkazo na hili ningeishauri sana serikali isaidie kwa sababu vyenginevyo tutakuwa tuko nyuma sana, ni suala la ukaguzi wa *value for money*. Hili ni jambo ambalo tunahitaji kulishughulikia kwa nguvu kubwa sana, vyenginevyo itakuwa pesa nyingi zinapotea bila ya kujua hali inavyokwenda.

Mhe. Spika, nilitoa mfano juzi Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi ilijenga kipande cha njia pale Wete kinaitwa *Kilo Road*. Walikuja wakandarasi wakajenga lakini baada ya miezi sita tu tayari barabara yote imechimbuka. Mhe. Spika, ukifanya uchambuzi wa *value for money* utajua kwamba pale tumeibiwa, sasa hii ni taaluma ambayo bado wakaguzi wetu hawajaifanya.
Mhe. Spika, ningeishauri serikali kwa makusudi kabisa ione kwamba hapa utawala wetu bora una kasoro kubwa. Tulipokwenda Malaysia na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tuliambiwa kwamba nchi ile ilipata uhuru mwaka 1957. Lakini kuanzia mwaka 1978 wao wanafanya *value for money auditing*, sasa kwa kweli katika masuala hayo wamepiga hatua kubwa.

Mhe. Spika, sisi tumepata uhuru mwaka 1964 lakini hadi leo bado hili suala hatujalianza. Kwa kweli ningeshauri Mhe. Spika, serikali kwa makusudi kabisa imsaidie Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujenga uwezo wa vijana wake ili kuona kwamba hatua hii tumeifikia vyenginevyo tutakuwa na hali ngumu sana.

Mhe. Spika, nimeona hapa katika kitabu chake Mhe. Waziri ukurasa wa 104 kifungu 2500 Uimarishaji wa Uchunguzi wa Hesabu *(Audit Capacity Building)* kwa kweli mna pesa haba sana. Mhe. Spika, kuingiza fedha zile ndogo hatuwezi kujenga uwezo wa wakaguzi na kwa hiyo kufikia katika *target* ambayo tumefika. Ushauri ni kwamba serikali na waziri asaidie kuongeza fedha katika mafungu haya na hasa *Audit Capacity Building*, kuona kwamba vijana wetu wana uwezo wa ku-*across size* hii *performance auditing* ili nchi yetu ipige hatua sana katika masuala haya ya utawala bora.

Mhe. Spika, jengine ni Afisi ya Mrajis Mkuu, naungana na wenzangu kwamba hii afisi ni muhimu sana katika nchi yetu, sasa inahitaji kuimarishwa sana. Tulikwenda pale na Kamati yetu ya *PAC* kuna matatizo mengi, lakini nizungumzie lile ambalo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amelizungumza Mrajis kukosa hata gari kwa kweli hatumfanyii haki. Ikiwa kuanzia siku ile mpaka leo hajapata hata usafiri basi tunafanya dhihaka sana katika baadhi ya mambo. Haiwezekani kwamba Mrajis Mkuu wa Serikali audunde mitaani haileti picha nzuri. Nilipoangalia katika malengo ya mwaka huu ukurasa wa 407 fungu la mrajis kifungu kidogo 1800 Ununuzi wa Magari, Honda na Matrekta kwa Unguja hakuna kilichotengwa kwa ajili ya ununuzi wa kipando cha Mrajis.

Sasa hili naomba maelezo ya Mhe. Waziri, pamoja na kelele zote zile tunazopiga hili kwa mwaka huu atalifanyaje. Pengine kuna gari amewekewa na Waziri wa Fedha pale, siku nyengine Wizara ya Fedha huwa wanapata pata magari. Kwa hiyo, akija akinijibu mimi sina tatizo, lakini kama hali ndio hii kwa kweli hapa pana mtihani kidogo.

Mhe. Spika, jengine katika fungu hilo hilo la Mrajis Afisi ya Pemba ukurasa wa 410, fungu 1800, kifungu kidogo 1802 Ununuzi wa Gari imetengewa shilingi 2,450,000. Sasa nilikuwa najiuliza Mhe. Waziri anakusudia kununua bajaji ile ya maringi matatu au vipi. Pengine itafaa lakini kwa bei hii sidhani kwamba kuna gari ambayo anaweza kununua. Kwa milima ile ya Pemba sijui bajaji itakuwaje Mhe. Spika, isije kufika siku moja nikaiona bajaji ya Mhe. Waziri miguu juu pale Kilimandege. Kwa hiyo, nahisi kwamba hii fedha iliyowekwa ni ndogo sana na haiwezi kununua gari kwa ajili ya Afisi ya Mrajis Pemba.

Mhe. Spika, katika eneo hilo la Afisi ya Mrajis tuna tatizo kidogo la vyeti vya kuzaliwa, sijui ni nchi nzima lakini pale Wete tuna tatizo kidogo. Unaweza kukaa miezi minane tangu mtoto azaliwe hujapata cheti chake cha kuzaliwa. Sasa wananchi siku hizi wameraghibika sana kuona kwamba vijana wao wanapata vyeti vya kuzaliwa. Kwa hiyo, pamoja na kuraghibika huko kwa wananchi bado suala hili linazorota tunamuomba Mhe. Waziri alishughulikie kidogo.

Mhe. Spika, jengine utendaji wa kazi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka unaridhisha lakini kuna mambo mawili matatu ningemuomba ashirikiane na serikali kuona kwamba *weakness* iliyoko haizoroteshi utoaji wa haki.

La kwanza ni udhaifu wa Maabara Kuu ya Serikali kwa kweli inaonekana inahitaji kuimarishwa ili yale mambo yanayokamatwa baada ya muda wa siku mbili tatu yasije kugeuka kuwa mambo mengine. Hata hivyo Mhe. Spika, hii haiko chini ya wizara ya Mhe. Waziri lakini ni eneo moja ambalo linasababisha haki kutofanyika vizuri ule udhaifu wa maabara ile. Kwa hiyo, ningemuomba Mhe. Waziri yeye kama *custodian* wa utawala bora katika nchi yetu ashirikiane na serikali kuona kwamba Maabara Kuu ya Serikali imeimarishwa na ina uwezo wa kufanya shughuli zake kwa wepesi na haraka ili kuona kwamba haki inatendeka kwa mujibu ambavyo inatakiwa.

Lakini jengine ambalo ni muhimu sana ni upatikanaji wa mashine ya *DNA* na hapa ni tatizo kubwa. Kwa sababu siku hizi tabia ya watu kufanya mambo yasiyokuwa sio yako mengi, mtu akishafanya mambo yake anaruka anasema mtoto si wake, sasa inakuwa tabu sana Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuona kwamba haki inatendeka. Kwa sababu mashine hapa Zanzibar hapana, iliyoko ni ghali, kwa hiyo nayo inazorotesha upatikanaji wa haki, matokeo yake ni kwamba watoto wetu, dada zetu wanabebeshwa mizigo ambayo haistahiki kubebeshwa.

Mhe. Spika, hili ni jukumu la Mhe. Waziri kama mlezi wa utawala bora katika nchi kuona kwamba mashine hii imepatikana japokuwa ni ghali sana lakini haki ina gharama zake. Sasa tukisema tu ni ghali huku wananchi wetu wanaendelea kudhalilika kwa sababu ya ughali ni mtihani kidogo. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba tujaribu kukata pua tuunge wajihi, tukate maeneo mengine lakini hatimaye Zanzibar iwe na kifaa hichi ambacho kingeweza kujua damu ya baba na mtoto ili hatimaye haki kuhusiana na suala hili ijulikane.

Mhe. Spika, ningeomba nimalizie katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, ukurasa kwa 19 wa kitabu cha Mhe. Waziri alionesha kwamba kuna masuala ya kanuni ambazo Afisi ya Mwanasheria Mkuu inashughulika nazo. Sasa hili ni jambo zuri, lakini kwanza nataka kujua kanuni ambazo zinatungwa na wizara baada ya sisi wawakilishi kutoa ruhusa kwa mawaziri kutunga kanuni, Afisi ya Mwanasheria Mkuu inahusikanaje. Inawasaidia vipi mawizara kutunga zile kanuni na wanaangaliaje kuona kwamba kanuni zinazotungwa hazipingani na sheria mama au na katiba.

Lakini la pili na muhimu ni kwamba huwa tunatunga sheria hapa Barazani na tukawapa uwezo mawaziri husika kutunga kanuni, halafu mawaziri wakachukua muda mrefu miaka miwili, mitatu, minne kanuni zenyewe

hazijatungwa na hilo huzorotesha utekelezaji mzuri wa ile sheria. Sasa pia nilitaka kujua Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika hili nalo lina mkono wake vipi.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ni suala la rushwa. Mhe. Spika, naomba kunukuu katika ukurasa wa 35 kifungu cha 96. "Katika hili wizara yangu bado inaendelea na jitihada za kuona kwamba sheria ya rushwa inakamilika na kuwa moja ya nguzo kuu za kuimarisha utawala bora hapa nchini na ililipangia suala hilo kufikishwa katika ngazi mbali mbali za maamuzi likiwemo Baraza lako tukufu.

Hata hivyo, suala hili ilibidi kusitishwa kutokana na uamuzi wa wajumbe wa Baraza lako tukufu wa kupitisha maamuzi ya kufanya suala la utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi lisiwe suala la Muungano". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, naona haya mambo hayana *relevance* hata kidogo, kwa maoni yangu. Sisi tulitegemea kutoka kwa Mhe. Waziri, alete sheria inayohusiana na rushwa katika Baraza la Wawakilishi. Lakini sisi tunashughulikia masuala ya mafuta na gesi kulitoa katika orodha ya kero za Muungano, yeye amelihusisha na kwamba ndio sababu ambayo Baraza hili limekosa kuletewa sheria inayohusiana na suala la rushwa. Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba hayo mambo mawili hayafanani.

Kwa hivyo, ningemshauri Mhe. Waziri suala la rushwa tulishughulikie kabla halijaifikisha nchi yetu pahala pabaya.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza mwanzo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono hoja. Nakushukuru.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kufunga kikao hiki. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai, akatubakisha wazima hadi saa hii.

Mhe. Spika, namshukuru sana na ninampongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea hotuba ambayo aliisoma kwa ufanisi na kwa muda kama ulivyomsifu wewe mwenyewe. Hata kitabu chake Mhe. Spika, kina kava ya aina yake, kwa hivyo napenda nimpongeze.

Mhe. Spika, tulikuwa tumezoea zile *plan colors*, lakini *Alhamdulillah* yeye katuletea vitu kidogo vilivyochanganyika changanyika. Kwa hivyo, vinaburudisha moyo.

Mhe. Spika, wizara hii ni muhimu sana na kwa lugha ya kisasa ndio inaitwa Wizara Mtambuka. Kwa maana kazi yake inaunganisha sehemu nyingi katika maendeleo ya binadamu. Mbali ya ile kazi ambayo huko mwisho huwa inatajwa ya muhimili wa tatu wa dola yaani mahakama. Lakini kazi ya kushughulikia katiba na utawala bora ni kitu cha uhai, ni kitu ambacho kinakuwa siku hadi siku.

Kwa hivyo, sio kitu ambacho ni cha kwenda ukafanya halafu ukarudi, kila siku ni lazima usuguwe kichwa na uone ni kitu gani ambacho utakifanya baadae. Mhe. Spika, kwa sababu huu utawala bora ni kitu ambacho ni cha kuendelea ni *live*. Kwa hivyo, mimi ninaitaja hii Idara ya Uratibu wa Utawala Bora kwamba ni idara muhimu sana. Sijui Mhe. Waziri ni kwa muda gani idara hii inafanya tathmini ya hali inavyoendelea katika mawizara tofauti, angalau katika utendaji wa serikali. Ni namna gani wizara zinavyobadilika katika kushughulikia suala zima la utawala bora.

Mhe. Spika, vigezo vingi vimetolewa sio pahala pake hasa kwa muda tulionao. Lakini mimi nasema kwamba lazima kuwe na muda Idara hii ya Uratibu wa Utawala Bora, ni lazima kuwe na muda ambao itafanya tathmini na kuziharifu wizara au taasisi namna gani inavyoendesha shughuli zake kwa utaratibu wa utawala bora.

Kwa mfano, Mhe. Spika, kuna suala ambalo limejitokeza hivi karibuni, linaitwa PPP yaani *Public Private Partnership* ni sera ambayo tunakwenda nayo sasa hivi. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba bado wale *private* ambao tunawataka washiriki kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi, basi wanakuwa hawajapewa fursa ya kutosha ya kufanya shughuli zao.

Mhe. Spika, mimi nimewasikia wanasikitika sana kwamba kuna makampuni kwa mfano, ya ujenzi yamejisajili, yanalipa ada zao. Lakini wakipeleka tenda wanapewa mawizara ya serikali au vikosi, ambao wale hawamo kabisa katika utaratibu mzima wa ujenzi. Kwa sababu tumeamua sasa hivi. Wakati wa nyuma ilikuwa hakuna makampuni yale, kwa hivyo Idara ya Ujenzi ndio ilikuwa ikijenga majengo yote. Lakini tulipoamua kuchukua sasa utaratibu huu wa sera ya ushirikiano na sekta binafsi, basi inabidi ni lazima sasa tuangalie kwamba kweli utekelezaji wake unafanyika au haufanyiki.

Kwa bahati mbaya wanasema hawa makampuni kwamba hata wao wakipeleka zile tenda, wakati mwengine wanaambiwa aah! Sisi tunawaona, lakini wakubwa wanatuambi tuwape hawa. Kwa hivyo, hapo pana tatizo. Ni lazima twende na mtizamo ule ule kwamba tumewaambia makampuni yetu wafanye usajili, wanalipa ada zote kama kawaida, wanatoa kwa ZRB michango yao, lakini baadae tenda inapelekwa upande wa serikali.

Kwa hivyo, nasema kwamba haiko tu katika upande wa kisiasa tu labda kusema kwamba utawala bora utizame katika nyendo za kisiasa tu, lakini hata katika uendeshaji wa uchumi wetu tuutizame ni namna gani tuna *perform* katika utawala bora. Kwa hivyo, kwa ufupi nilikuwa nazungumza kwamba lazima kuwe na utaratibu wa tathmini katika kila nyanja, ili tuone ni namna gani tunakwenda katika utawala bora.

Suala la pili, Mhe. Spika, nije katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Kama ilivyozungumzwa na wajumbe wengine, sitaki niyarudie. Mim nina agizo nililopewa na wananchi kutoka katika jimbo langu na majimbo mengine. Mhe. Spika, wao wanasikitishwa sana na utendaji mdogo na mbovu uliopo wa utoaji wa vyeti vya kuzaliwa. Wengine wanafika miaka mitatu mtoto wake hajapata cheti cha kuzaliwa.

Sasa Mhe. Spika, hebu angalia wewe mwananchi ambaye anakwenda afisini, tokea yule mtoto kazaliwa mpaka atakuja mwengine hajapata cheti cha kuzaliwa. Kwa sababu kwa miaka mitatu kwa uzazi wetu keshaletwa mwengine, wakati kile cha yule wa mwanzo hajakipata. Mhe. Waziri nakumbuka mimi nilikuuliza swali hili hili katika bajeti iliyopita na majibu yako yalikuwa mazuri sana, lakini uzuri wake umekatika. Kwa hivyo, naomba na mwaka huu nikuulize tena.

Je, vipi marekebisho haya ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa, mbona kompyuta ziko nyingi? Tunaona kwamba mashine za kutengeneza vitambulisho vya Mzanzibari, vitambulisho vya upigaji kura na leseni za magari, vyote hivyo ukipeleka tu unapewa pale pale. Basi hiki cheti hakuna kompyuta hizo duniani za kutengeneza cheti. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunataka uje kutujibu hasa kiuwazi wazi. Ni lini utaanza mkakati wa kuona kwamba wote waliopeleka karatasi au maombi yao sasa ikifika tarehe hii watakuwa wameshapata na utaratibu mpya utaanza.

Mhe. Spika, nikija kwenye Afisi ya Mufti. Kwanza natoa pongezi zangu kwa kutoa miongozo tofauti katika kila hali na bado nchi yetu inakwenda katika hali ya usalama na migogoro hii ya kidini. Kama alivyozungumza Mhe. Waziri Waziri Kivuli mambo yale mawili. Kwanza mimi nataka kusema kwamba sisi tunazungumza Uislamu, lakini hata hizo nchi ambazo hazina hata Uislamu suala la mabaa ni suala ambalo linapewa udhibiti mkubwa sana. Kwa sababu huruhusiwi kuuza ulevi nje, huruhusiwi kuuza ulevi mitaani, kuna udhibiti mkubwa, seuze hapa ambapo tunazungumza kwamba hili ni tatizo katika jamii yetu ya Kiislamu. Kwa hivyo, ni bora tufanye uchunguzi hasa ni kitu gani kilichokosekana hata ikawa hali imefikia hivyo.

Suala jengine Mhe. Spika, ni la kubambikiza sheria. Mimi binafsi bahati mbaya unajua ukizisikia zile habari hujui kama litatokezea nyumbani. Lakini nimeona kabisa *documentary* inayoeleza kwamba wenyewe watu wa Uingereza na wengine wanaanza kurudi nyuma kuhusu malezi ya watoto wao. Vile walivyokuwa wakitarajia kuwa watawalea na wanavyojitokeza wao wale watoto, basi ni tofauti kabisa na matarajio yao. Kwa hviyo, wanarudi nyuma ndio maana wanaanza kusema tuwe na watoto wengi kidogo na tuwalee hivi. Sasa sisi wakija kutuambia yale waliyokuwa wakiyafanya miaka 20 na 30 iliyopita tuyafanye sisi sasa hivi, nastaajabu sana kwamba sisi tutayachukua. Wakati wao wanarudi nyuma katika malezi yao, halafu sisi wanakuja kutupa yale ambao wao wamekwisha wafika rohoni.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba tuitizame sana kabla haijaja hapa. Kama ni Wizara inayoshughulikia Katiba na Utawala Bora, basi itizame kupitia Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ambayo ndio inayoandaa sheria hii, kuona kwamba je, hii haitoleta migongano katika jamii.

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti naiomba kitu kimoja. Ukenda katika Miskiti mara nyingi utaona kuna watu wanakuja na barua wanasema wamepitia Afisi ya Mufti, kwa hivyo wanakwenda kupata ruhusa ya kuomba Misikitini. Wizara nyingi tunaziona hapa zinatafuta misaada mbali mbali nchi za nje. Kuna GBS hiyo, *budget support* na kuna misaada ya kimiradi. Basi hiyo Afisi ya Mufti pamoja na shughuli yote hii iliyopewa, haina fursa ya kuomba misaada nje isipokuwa watowe vipande tu watu wapite Misikitini kuomba ili kuzisaidia hizi madrasa zetu za hapa, naona wangefanya kazi hiyo. Wangefanya kazi ya kwenda nje na wakaandika *project report* hizi na kuzipeleka nje.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba dakika tano zangu nizipate asubuhi kesho tukijaaliwa. Mhe. Spika, naunga mkono hoja na ninamuomba Mhe. Waziri airuhusu hii Afisi ya Mufti iende nje ikatutafutie misaada, hawaendi kujiunga na *OIC* asiwe na wasi wasi.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Rashid Seif Suleiman, kwa mchango wako huo. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa. Sasa naahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 24/06/2010, saa 3:00 barabara za asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 24/06/2010 saa 3:00 za asubuhi)*